# Kiswahili

## kwa

## Shule za Rwanda

## Kidato cha Kwanza

## Kitabu cha Mwanafunzi

© 2020 Bodi ya Elimu Rwanda

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Elimu Rwanda.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Elimu Rwanda wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# Dibaji

Mwanafunzi mpendwa,

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kwa kutoa kitabu cha Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza katika ngazi ya chini ya sekondari.

Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri maisha yake na kumpa fursa ya kujipatia ajira au kuandaa miradi mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii anamoishi.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza kuhusu umuhimu wa kufungamanisha shughuli za ujifunzaji na ufundishaji pamoja na zana na mitaala ili kufanikisha mchakato mzima wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale yanayofundishwa na uwezo waupatao wanafunzi. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Hivyo basi, kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza unaokuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti ya kibinafsi na yale utakayofanya katika makundi kwa msaada wa walimu ambao huwajibika kufanikisha ufundishaji. Aidha, utapata stadi muhimu zitakazokuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha mbalimbali ya maisha halisi ili uweze kuonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Mwelekeo uliozingatiwa katika kitabu hiki unatofautiana na ule uliotiliwa maanani katika mfumo wa zamani ambapo mchakato wa kujifunza ulifanywa kwa kutilia mkazo upataji wa maarifa kutoka kwa mkufunzi ambaye pia alifikiriwa kumzidi mwanafunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi. Kwa hiyo, dhana huanzishwa aghalabu kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na kupata maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya ujifunzaji hujihusisha na shughuli mbalimbali zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri kuhusu yale anayoyafanya, kuonyesha uzoefu wake halisi na maarifa aliyo nayo katika mchakato huo wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, utakuwa na majukumu yafuatayo ili uweze kutumia kitabu hiki kwa ufanisi:

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi au mazoezi yanayolenga kwenye mada;
- Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kupitia mawasilisho, mijadala, kazi za makundi na mbinu nyingine za ufundishaji kama vile michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, mitandao na hata nje ya shule;
- Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa /mtandaoni, wataalamu na kuwasilisha matokeo ya utafiti;
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi ulizopewa kupitia maelezo na majadiliano kila unapoongea hadharani;
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi yako ya ujifunzaji.

Mwishowe, ningependa kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki na kutoa mchango wao kwa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioongoza mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu kutoka shule tofauti kwa kuendeleza na kufanikisha kazi hii. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata.

**Dkt. Irénée NDAYAMBAJE**

**Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Elimu Rwanda**

# Shukrani

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki, jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziwaendee viongozi wa shule mbalimbali walioruhusu walimu wao kufanya kazi na Bodi ya Elimu Rwanda katika mradi wa ukamilishaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu ambao juhudi zao na uandikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, shukrani ziwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

# Yaliyomo


***Mada Kuu:* Kuelewa Mazungumzo na Kujieleza Kimazungumzo..... 1**
***Mada Ndogo:* Maamkizi na Utambulisho.................................. 1**

*Somo la Kwanza*
**Maana ya Maamkizi.....................................................................2**
Vifungu mbalimbali vya maamkizi ...............................................2
Msamiati wa maamkizi..................................................................5
Mazungumzo yenye maamkizi mbalimbali ..................................7
Sarufi...............................................................................................9
Matamshi na tahajia bora ............................................................. 11

*Somo la Pili*
**Aina Mbalimbali za Maamkizi............................................... 15**
Msamiati wa maamkizi mbalimbali ............................................ 19
Mazungumzo yenye maamkizi...................................................... 21
Sarufi............................................................................................. 22
Matamshi na tahajia bora ............................................................ 25
Mjadala/Mazungumzo.................................................................. 26

*Somo la Tatu*
**Matumizi ya Nafsi na Viwakilishi vya Nafsi katika Maamkizi ................27**
Maamkizi yenye nafsi katika umoja na wingi............................... 27
Msamiati wa viwakilishi vya nafsi................................................ 28
Sarufi............................................................................................. 29
Matamshi ya konsonanti na tahajia bora..................................... 31
Maswali ya Marudio ..................................................................... 32
*Faharasa .................................................................................... 34*

***Mada Kuu:* Matumizi ya Lugha Katika Mazingira Mbalimbali ...... 36**
***Mada Ndogo:* Msamiati Katika Mazingira ya Shule...................... 36**

*Somo la Kwanza:*
**Mazungumzo Shuleni.................................................................37**
Mazingira ya darasani................................................................... 37
Msamiati wa mazingira ya shuleni................................................ 39
Shughuli za siku za mwanafunzi................................................... 41

*Somo la Pili*
**Mazungumzo Kati ya Wanafunzi ...............................................46**
Mazungumzo ya wanafunzi ........................................................... 46
Msamiati wa shuleni ..................................................................... 48
Sarufi............................................................................................. 49
Kusikiliza na Kuzungumza ........................................................... 51

*Somo la Tatu*

**Viongozi Wetu Shuleni ........................................ 52**

Mahusiano ya watu wanaopatikana shuleni ........................................ 52

Msamiati kuhusu viongozi wa shuleni ........................................ 54

Majina ya watu mbalimbali na kazi zao ........................................ 56

*Somo la Nne*

**Shule Yangu ........................................ 58**

Ufahamu ........................................ 58

Kifungu cha ratiba ya masomo shuleni ........................................ 61

Kusikiliza na kuzungumza ........................................ 62

Sarufi ........................................ 62

*Somo la Tano*

**Usafi Shuleni ........................................ 65**

Kifungu kuhusu usafi shuleni ........................................ 65

Msamiati kuhusu usafi shuleni ........................................ 66

Sarufi ........................................ 67

Kusikiliza na kuzungumza ........................................ 70

*Faharasa ........................................ 71*

***Mada Kuu:* Matumizi ya Lugha Katika Mazingira Mbalimbali....... 75**

***Mada Ndogo:* Msamiati Katika Mazingira ya Nyumbani .............. 75**

*Somo la Kwanza:*

**Aina za Nyumba, Watu Wanaoishi Humo na Ujenzi Wake ...................... 76**

Michoro na mazungumzo kuhusu aina za nyumba na watu wanaoishi humo.... 76

Msamiati wa nyumbani ........................................ 78

Sarufi ........................................ 82

Matamshi na tahajia bora ........................................ 83

*Somo la Pili*

**Vifaa Mbalimbali Vinavyopatikana Nyumbani ........................................ 84**

Vifaa vya nyumbani ........................................ 84

Mjadala kuhusu dhima ya vifaa vya nyumbani ........................................ 86

Msamiati wa vifaa na sehemu za nyumba ........................................ 87

Sarufi ........................................ 88

Tahajia na matamshi bora ........................................ 90

*Somo la Tatu*

**Mifugo Wanaopatikana Nyumbani na Vivumishi vya Ngeli ya A–WA...... 91**

Michoro ya mifugo mbalimbali ........................................ 91

Msamiati kuhusu mifugo na vivumishi vya ngeli ya A-WA........................................ 92

Sarufi ........................................ 93

Tahajia na matamshi bora ........................................ 95

*Somo la Nne*
**Majina Yanayohusishwa na Watu na Uhusiano Wao Kijamii Pamoja na Vivumishi vya Ngeli ya A-WA ..... 97**
Mazungumzo ..... 98
Msamiati wa vifaa vya nyumbani ..... 99
Sarufi ..... 100
Tahajia na matamshi bora ..... 103

*Somo la Tano*
**Uhusiano wa Kifamilia Pamoja na Vivumishi vya Ngeli ya A–WA ..... 104**
Michoro ya watu katika jamii ..... 104
Kifungu kuhusu uhusiano wa kifamilia ..... 105
Kusikiliza na kuzungumza ..... 106
Msamiati wa familia ..... 109
Sarufi ..... 109
Tahajia na matamshi bora ..... 111
*Faharasa ..... 112*

***Mada Kuu:* Msamiati wa Mazingira Mbalimbali ..... 114**
***Mada Ndogo:* Msamiati wa Mazingira ya Utawala ..... 114**

*Somo la Kwanza*
**Nchi Yangu ..... 115**
Ramani ya nchi ya Rwanda ..... 115
Msamiati mpya kuhusu nchi ya Rwanda ..... 116
Dira ya dunia ..... 119
Sarufi ..... 123
Mazoezi ya marudio ..... 125

*Somo la Pili*
**Ofisi ya Tarafa Yangu ..... 127**
Msamiati kuhusu ofisi za kiutawala ..... 129
Sarufi: Ngeli ya U-I ..... 131

*Somo La Tatu*
**Utawala Bora ..... 136**
Msamiati wa utawala ..... 138
Sarufi: Ngeli ya U-I na vivumishi vya sifa ..... 140
Kusikiliza na kuzungumza ..... 143
*Faharasa ..... 144*

***Mada Kuu:* Msamiati wa Mazingira Mbalimbali ..... 147**
***Mada Ndogo:* Msamiati wa Mazingira ya Sokoni ..... 147**

*Somo la Kwanza*
**Mnunuzi na Muuzaji ..... 148**
Mazungumzo kati ya muuzaji na mnunuzi ..... 148

Msamiati wa uuzaji na ununuzi ........ 150
Kuhesabu tarakimu ........ 152
Vipimo na matumizi yake katika hesabu ........ 154
Alama za hesabu ........ 156

*Somo la Pili*
**Biashara Mbalimbali ........ 157**
Msamiati wa biashara ........ 158
Tarakimu ........ 161
Kusikiliza na kuzungumza ........ 162

*Somo la Tatu*
**Mazingira ya Sokoni ........ 164**
Msamiati wa sokoni ........ 165
Matumizi ya lugha ya sokoni ........ 167
Sarufi: Vivumishi vya idadi ........ 168
*Faharasa ........ 172*

***Mada Kuu:* Matumizi ya Lugha Katika Mazingira Mbalimbali ........ 174**
***Mada Ndogo:* Matumizi ya Msamiati Kuhusu Usafi wa Mwili ........ 174**

*Somo la Kwanza*
**Maana ya Usafi wa Mwili ........ 175**
Kusikiliza na kuzungumza ........ 177
Msamiati wa usafi wa mwili ........ 178
Wimbo kuhusu sehemu za mwili wa binadamu ........ 179
Sarufi ........ 181
Magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa usafi ........ 183

*Somo la Pili*
**Msamiati wa Mwili na Mazingira ........ 185**
Kusikiliza na kuzungumza ........ 186
Msamiati wa mwili na mazingira ........ 188
Sarufi ........ 189
Matamshi na tahajia bora ........ 189

*Somo la Tatu*
**Usafi wa Mwili na Mazingira ........ 191**
Kuzikiliza na kuzungumza ........ 192
Msamiati wa usafi wa mwili na mazingira ........ 193
Msamiati wa magonjwa ........ 194
Sarufi ........ 195
Matamshi na tahajia bora ........ 197
*Faharasa ........ 199*

# Utangulizi

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake wa kutumiwa kama lugha rasmi miongoni mwa lugha nyingine zinazotumiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari. Zaidi ya hayo, mbali na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa katika mchepuo wa Fasihi, Kinyarwanda na Kiswahili, lugha hii hufundishwa pia katika michepuo mingine. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kimatumizi nchini Rwanda na hata katika jamii mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni. Nchi kama vile Marekani, Ujerumani na nchi nyingi za Ulaya, hufundisha Kiswahili na kukitumia katika mazingira tofauti.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuwalenga wanafunzi wa kidato cha kwanza katika ngazi ya chini ya sekondari nchini Rwanda.

Kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki imegawanywa katika masomo. Masomo haya yamegusia vipengele vifuatavyo:

- Kusoma na ufahamu
- Matumizi ya msamiati wa msingi
- Sarufi
- Kusikiliza na kuzungumza
- Kuandika.

Masomo yaliyopendekezwa katika kitabu hiki yamezingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda kwa sababu Kiswahili kinahitajika kutumiwa katika mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kujifunza hatua kwa hatua masomo yote yaliyopendekezwa ili aweze kujijengea na kujifungulia milango ya kujiendeleza na kuliendeleza taifa lake kwa ujumla.

Uwezo utakaopatikana kupitia masomo hayo, utamwezesha mwanafunzi kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha yake ya kila siku: kutunza mazingira, elimu kuhusu uzalishaji mali au ujasiriamali, usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, elimu kuhusu ujinsia na elimu jumuishi.

Ni vyema mwanafunzi ajitahidi kufanya kazi zilizotolewa kwa kila somo. Vilevile, ni jambo muhimu kusoma kwa makini na kufanya uchunguzi wa mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki. Kazi nyingi zilizopendekezwa zitamwezesha mwanafunzi kukuza uwezo wake katika kiwango cha utafiti, ushirikiano na utawala binafsi na stadi za maisha na kuendeleza ujifunzaji wa muda mrefu. Vilevile, kazi za mijadala ya kibinafsi na ya makundi zote zitasaidia kumjenga mwanafunzi kwa kumpa uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia Kiswahili fasaha.

Kazi za makundi zilizopendekezwa zitamsaidia mwanafunzi kuelewa nafasi yake katika kujenga desturi ya heshima kwa wengine, uvumilivu, upendo na amani, haki, umoja na mshikamano na demokrasia.

## Mada Kuu:

# Kuelewa Mazungumzo na Kujieleza Kimazungumzo

## Mada Ndogo:

# Maamkizi na Utambulisho

**Somo la Kwanza:** Maana ya maamkizi

**Somo la Pili:** Aina mbalimbali za maamkizi


**Somo la Tatu:** Matumizi ya nafsi katika maamkizi: Viwakilishi vya nafsi

Somo la Kwanza

# Maana ya Maamkizi


## A. Vifungu mbalimbali vya maamkizi

**Tazama michoro ifuatayo kwa makini kisha kwa ushirikiano na wenzako tathmini maana ya maamkizi kwa kutumia maswali yanayoambatana nayo.**



**Babu na mjukuu:**

Shikamoo babu! Marahaba Jeni.



**Baba na mtoto:**

Umeshindaje mwanangu? Vyema baba.



### Mwanafunzi na mwanafunzi mwenzake:

U hali gani Juma? Njema Aisha.



### Kaka na dada:

Hujambo dada? Sijambo kaka.



### Muuzaji na mnunuzi:

Habari za asubuhi mteja wangu! Nzuri.

### Tathmini

a) Michoro iliyo hapo juu inahusu nini?

b) Unaweza kuwaeleza wenzako kinachoendelea katika michoro hiyo?

Baada ya kuwaeleza wenzako, jigawe katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili kisha muigize mifano hiyo ya michoro.

### Maelezo muhimu

- Maamkizi ni kujuliana hali. Pia huitwa **salamu**.
- Maamkizi huleta amani baina ya watu na pia huwaunganisha. Maamkizi pia huondoa uadui miongoni mwa watu.

### Mifano zaidi ya maamkizi

Linganisha mifano ifuatayo na mawazo yako kuhusu michoro iliyotangulia:

| Maamkizi | | Jibu |
|---|---|---|
| 1. Hujambo? | - | Sijambo. |
| 2. Habari za jioni? | - | Nzuri/Njema. |
| 3. Shikamoo! | - | Marahaba. |
| 4. Hamjambo? | - | Hatujambo. |
| 5. U hali gani? | - | Njema/Nzuri. |
| 6. Kwaheri! | - | Ya kuonana. |
| 7. Sabalheri! | - | Akheri. |
| 8. Masalheri! | - | Akheri. |
| 9. Pole! | - | Nishapoa. |
| 10. Umeamkaje? | - | Vyema. |

## Maigizo ya maamkizi mbalimbali

Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, igizeni maamkizi mbalimbali kutokana na mifano mliyopewa kwa kuzingatia ufasaha wa kujieleza na matamshi bora. Jaribuni kutatua matatizo yoyote ya kimatamshi.

*Zoezi la 1*

**Waamkie wenzako kwa salamu zifuatazo kisha fanyeni igizo la kuamkiana.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Habari za jioni? | - | Njema/Nzuri. |
| 2. Umeshindaje? | - | Vyema/Salama/Vizuri. |
| 3. Hujambo? | - | Sijambo. |
| 4. U hali gani? | - | Njema/Nzuri. |
| 5. Shikamoo! | - | Marahaba. |
| 6. Hamjambo? | - | Hatujambo. |
| 7. Salama? | - | Salmini. |
| 8. Habari za asubuhi? | - | Njema/Nzuri. |
| 9. Sabalheri! | - | Akheri. |
| 10. Kwaheri! | - | Ya kuonana. |

*Zoezi la 2*

**Fanya utafiti kutoka kwa wenzako kupitia mahojiano kisha uwaeleze wanafunzi wenzako ugunduzi wako kuhusu sababu za kuamkia mtu na umuhimu wake.**

## B. Msamiati wa maamkizi

Rejelea mifano ya maamkizi uliyosoma na kisha uorodheshe maneno yote mapya na yanayotatiza kuelewa. Jaribu kuyatolea maana kutokana na yalivyotumiwa. Fanya utafiti kwenye kamusi ya Kiswahili kwa maneno yanayotatanisha zaidi.

**Mifano:**

| Neno | Maana | Sentensi |
|---|---|---|
| **Jirani** | Mtu anayepatikana karibu na mahali ulipo ama unapoishi. | Hujambo jirani! |
| **Baba** | Mzazi wa kiume. | Shikamoo baba! |
| **Mama** | Mzazi wa kike. | U hali gani mama? |
| **Mwalimu** | Mtu anayewasomesha wengine. | Hujambo mwalimu! |
| **Muuzaji** | Mtu anayeuza vitu. | Asante sana muuzaji. |
| **Mnunuzi** | Mtu anayenunua vitu kutoka kwa muuzaji. | Karibu mnunuzi. |

***Zoezi la 1***

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi katika daftari lako kwa kuteua jawabu sahihi kutoka maneno yafuatayo:**

Marahaba    Sijambo    Njema    Ya kuonana    Asante

**Mfano:**

Sabalheri - ____________

**Jibu:** Akheri

1. Hujambo? - ____________________
2. Shikamoo! - ____________________
3. Kwaheri! - ____________________
4. Habari za mchana? - ____________________
5. Karibu! - ____________________

### *Zoezi la 2*

Tunga maamkizi yako binafsi na majibu yake kisha ujadiliane na wenzako kuhusu usahihi wake.

**Mfano:**

Habari za leo? - Njema/Nzuri.

## C. Mazungumzo yenye maamkizi mbalimbali

Soma kwa sauti na kwa zamu maamkizi yafuatayo baina ya wazazi na watoto wao.



**Baba:** Hujambo mwanangu?


**Aisha:** Sijambo baba. Shikamoo?

**Baba:** Marahaba mwanangu. U hali gani?

**Aisha:** Njema baba.

**Baba:** Salama?

**Aisha:** Salmini.



**Mama:** Umeamkaje Juma?

**Juma:** Salama mama. Shikamoo?

**Mama:** Marahaba mwanangu. Habari za kushinda?

**Juma:** Njema mama.

**Mama:** Je, umemaliza kazi niliyokupa?

**Juma:** Ndio mama.

**Mama:** Sawa. Naenda sokoni kununua mboga na matunda.

**Juma:** Sawa mama.

**Mama:** Kwaheri Juma.

**Juma:** Ya kuonana mama.

***Zoezi***

Tunga mifano zaidi ya maamkizi kwa kufuata mifano uliyopewa.

**Tathmini**

Baada ya kusoma mifano uliyopewa na kutunga maamkizi yako, kwa ushirikiano na wenzako, jaribu kueleza:

a) Maana ya kuamkiana

b) Lengo la kuamkiana

c) Uhusiano wa wanaoamkiana

Je, majibu yako yanalingana na haya?

**a) Maana ya kuamkiana ni:**

- Kujuliana hali

**b) Lengo la kuamkiana ni:**

1. Kuonyesha adabu.
2. Kuonyesha kuna amani na upendo.
3. Kufahamu hali za watu wengine.

**c) Uhusiano wa kimaamkizi ni:**

| Uhusiano | Wakati | Mfano |
|---|---|---|
| Umri mkubwa | Wowote | Shikamoo! |
| | Wowote | Habari? |
| | Asubuhi | Umeamkaje? |
| | Mchana | Umeshindaje? |

## D. Sarufi

### Umoja na wingi wa maamkizi

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni sentensi zifuatazo kwa zamu katika umoja na wingi.**

| | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kwaheri Maria! | - | Kwaherini kina Maria. |
| 2. | Hujambo mwalimu? | - | Hamjambo walimu? |
| 3. | Shikamoo mama! | - | Shikamoo kina mama! |
| 4. | Habari yako? | - | Habari zenu? |
| 5. | Sijambo. | - | Hatujambo. |
| 6. | U hali gani? | - | M hali gani? |

7. Umelalaje? - Mmelalaje?
8. Pole! - Poleni!
9. Karibu. - Karibuni.
10. Sabalheri! - Sabalheri!

**Tathmini**

**Gundua tofauti inayobainika katika maamkizi katika umoja na wingi. Zingatia mifano iliyopo hapa chini katika nafsi mbalimbali.**

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| 1. Habari? (yako) | - | Habari? (zenu) |
| 2. Hujambo? (wewe) | - | Hamjambo? (nyinyi) |
| 3. Sijambo. (mimi) | - | Hatujambo. (sisi) |
| 4. Shikamoo! (baba) | - | Shikamoo! (kina baba) |
| 5. Shikamoo! (mama) | - | Shikamoo! (kina mama) |
| 6. U hali gani? (wewe) | - | M hali gani? (nyinyi) |
| 7. Kwaheri! (wewe) | - | Kwaherini! (nyinyi) |
| 8. Ameamkaje? (yeye) | - | Wameamkaje? (wao) |
| 9. Pole. (wewe) | - | Poleni. (nyinyi) |

***Zoezi la 1***

Kwa ushirikiano na wenzako, waulize maamkizi kwa umoja kisha nao wajibu kwa wingi. Tumia mifano iliyopo hapo juu.

***Zoezi la 2***

Jibu kwa usahihi kwa kuteua jawabu sahihi la wingi wa kila salamu na neno la adabu.

**Mfano:** Hujambo? - Sijambo.

1. Sijambo. - (Hatujambo, Jambo)
2. Hajambo. - (Hawajambo, Habari zenu)
3. Kwaheri! - (Kwaherini, Nzuri)
4. U hali gani? - (Njema, M hali gani?)
5. Karibu. - (Karibuni, Asante)

## E. Matamshi na tahajia bora

### Matamshi ya konsonanti

#### i) Soma kwa sauti.

a) Konsonanti za Kiswahili

| **Konsonanti Kubwa** | B | CH | D | DH | F | G | GH | H | J | K | L | M | N | NG |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Konsonanti Ndogo** | b | ch | d | dh | f | g | gh | h | j | k | l | m | n | ng |

| **Konsonanti Kubwa** | NG' | NY | P | R | S | SH | T | TH | V | W | Y | Z |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Konsonanti Ndogo** | Ng' | ny | p | r | s | sh | t | th | v | w | y | z |

b) Soma silabi zifuatazo kwa sauti:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Ba | Be | Bi | Bo | Bu |
| Cha | Che | Chi | Cho | Chu |
| Da | De | Di | Do | Du |
| Dha | Dhe | Dhi | Dho | Dhu |
| Fa | Fe | Fi | Fo | Fu |
| Ga | Ge | Gi | Go | Gu |
| Gha | Ghe | Ghi | Gho | Ghu |
| Ha | He | Hi | Ho | Hu |
| Ja | Je | Ji | Jo | Ju |
| Ka | Ke | Ki | Ko | Ku |
| La | Le | Li | Lo | Lu |
| Ma | Me | Mi | Mo | Mu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Na | Ne | Ni | No | Nu |
| Ng’a | Ng’e | Ng’i | Ng’o | Ng’u |
| Nga | Nge | Ngi | Ngo | Ngu |
| Nya | Nye | Nyi | Nyo | Nyu |
| Pa | Pe | Pi | Po | Pu |
| Ra | Re | Ri | Ro | Ru |
| Sa | Se | Si | So | Su |
| Sha | She | Shi | Sho | Shu |
| Ta | Te | Ti | To | Tu |
| Tha | The | Thi | Tho | Thu |
| Va | Ve | Vi | Vo | Vu |
| Wa | We | Wi | Wo | Wu |
| Ya | Ye | Yi | Yo | Yu |
| Za | Ze | Zi | Zo | Zu |

**ii) Soma konsonanti ambatano zifuatazo kwa sauti.**

**1. [mw]**

**Matumizi katika maneno:**

Mwalimu, mwangaza, mweupe, mweusi, mwanafunzi, mwisho, mwokozi, mwezi, mwizi, mwiko

**Matumizi katika sentensi:**

1. Ni muhimu kuzima mwangaza mchana.
2. Uwe mweusi, mnene au mwembamba, sote tuko sawa!

**2. [bw]**

Bwana, bwalo, kubwa, bwaga, bweka

**Matumizi katika sentensi:**

1. Habari bwana!
2. Wanyarwanda wote wana jukumu kubwa la kulipa ushuru.

**3. [kw]**

Kweza, kwenda, kwikwi, kwaheri, kwangu, kwako, kwote

**Matumizi katika sentensi:**

1. Karibu kwangu.
2. Kwaherini wageni.

**4. [vy]**

Vyakula, vyangu, vyombo, vyema

**Matumizi katika sentensi:**

1. Karibuni tule vyakula vitamu.
2. Asante kwa kunipa vyombo safi.

**5. [tw]**

Twiga, tweza, twanga

**Matumizi katika sentensi:**

1. Tafadhali nitwike mzigo huu.
2. Twanga nafaka hizi.

***Zoezi la 1***

Kwa ushirikiano na wenzako, tumia kamusi ya Kiswahili kutafiti na kuandika maneno ya sauti ambatano zifuatazo: (mifano mitatu kwa kila sauti)

| Sauti | Mifano wa maneno |
|---|---|
| [nj] | njoo, njiwa, njugu |
| [pw] | pweta, pwagu, pweza |
| [nz] | funza, nzito, enzi |
| [sw] | swara, swila, sweta |
| [mb] | mbuga, mbinja, mboga |

### *Zoezi la 2*

Kwa msaada wa wenzako na kamusi ya Kiswahili, eleza mbele ya wanafunzi wenzako maana ya maneno uliyopata yenye sauti [nj], [pw], [nz], [sw] na [mb].

**Mifano:**

**Njoo:** Tamko la kumwita mtu aliye mbali aje karibu na pale ulipo.

**Pweta:** Ona haya baada ya kutenda kitendo cha aibu.

### *Zoezi la ziada*

**Chagua jibu moja sahihi kati ya majibu yaliyo katika mabano ili kuelezea maelezo uliyopewa.**

**Mfano:** Neno linaloonyesha adabu na kujali. (Hodi, Pole)

**Jibu:** Pole

1. Hutumiwa na kila mtu asubuhi, mchana na usiku.

   (Salamu, Chuki)

2. Neno ambalo hutumiwa na mtu anayeagana na mtu mwingine.

   (Kwaheri, Karibu)

3. Hutumiwa na mdogo kwa mkubwa tu!

   (Marahaba, Shikamoo)

4. Jibu langu ni ‘Sijambo’.

   (Jambo, Hujambo)

5. Jibu la ‘Sabalheri’.

   (Akheri, Habari)

# Aina Mbalimbali za Maamkizi

**Tazama picha zifuatazo kwa makini pamoja na maandishi yaliyo chini yake kisha utathmini maana inayojitokeza**

|  |  |
|---|---|
| Hodi! - Karibu. | Umeshindaje? - Vyema/salama. |

## Mifano mingine ya maamkizi:

1. Waambaje? - Vyema/vizuri.
2. Makiwa! - Tunayo.
3. Masalkheri! - Akheri.

## Maswali ya kutathmini

a) Picha zilizo hapo juu zinazungumzia nini?

b) Waeleze wanafunzi wenzako maana ya maelezo yaliyomo.

## Maelezo muhimu

- Hizi ni aina za salamu/maamkizi. Maamkizi huenda na umri, wakati na hali.

**Tazama mchoro ufuatao kisha usome kwa sauti salamu zinazoambatana na mchoro huo.**

### a) Umri




**Kijana na kijana mwenzake**

**Kijana wa kiume:** Waambaje?

**Kijana wa kike:** Vyema.

**Mifano zaidi:**

**1. Mwalimu na mwanafunzi**

**Mwanafunzi:** Shikamoo mwalimu!

**Mwalimu:** Marahaba!

**2. Nyanya na babu**

**Nyanya:** Habari mwenzangu!

**Babu:** Njema sana mwenzangu.

## b) Hali


### i) Huzuni

| Maamkizi | Jibu |
|---|---|
| Makiwa! | Tunayo. |
| Pole! | Nishapoa. |



### ii) Furaha

| Maamkizi | Jibu |
|---|---|
| Pongezi! | Asante. |
| Hongera! | Nimehongera/Asante. |



### c) Nyakati mbalimbali

#### i) Wakati wa jioni

| Maamkizi | Jibu |
|---|---|
| Usiku mwema! | Nawe pia/Majaliwa. |
| Tuonane kesho! | Majaliwa. |
| Habari za jioni? | Njema/Nzuri. |
| Masalheri! | Akheri. |

#### ii) Wakati wa asubuhi

| Maamkizi | Jibu |
|---|---|
| Habari za asubuhi? | Njema. |
| Sabalheri! | Akheri. |

#### iii) Wakati wowote

| Maamkizi | Jibu |
|---|---|
| Kwaheri! | Ya kuonana. |
| Hodi! | Karibu. |
| Alamsiki! | Binuru. |
| Salama? | Salmini. |

#### Tathmini

Je, umegundua kwamba salamu na maamkizi hutegemea umri, hali na wakati? Kama hujagundua hivyo, hebu soma tena maamkizi hayo kwa makini huku ukizingatia michoro uliyopewa.

### Maigizo ya maamkizi mbalimbali

Soma tena kimyakimya aina mbalimbali za salamu zilizo hapo juu. Kisha kwa makundi ya wanafunzi wanne wanne someni kwa sauti kwa njia ya kubadilishana kwa kuzingatia matamshi bora.

#### Tathmini

a) Ni maneno gani yalikutatanisha kutamka?

b) Je, wenzako pia wana matatizo kama yako?

c) Wewe na wenzako mliyatatua vipi matatizo hayo?

Sasa jadiliana na wenzako jinsi ya kuyatatua matatizo hayo yote ya matamshi.

### Kazi ya makundi

Igizeni aina mbalimbali za maamkizi yaliyo kwenye ukurasa uliotangulia.

**KUMBUKA:** Salamu zinaweza kumfanya mtu apate kitu ama akikose, apendwe ama akataliwe.

## A. Msamiati wa maamkizi mbalimbali

*Rejelea tena maelezo na mifano ya aina mbalimbali za maamkizi. Orodhesha maneno yote mapya na kuyatolea maana. Fanya utafiti kwa kutumia kamusi ya Kiswahili. Kwa mfano:*

**Nyanya** - Mzazi wa kike wa baba au mama.

***Matumizi katika sentensi:*** Shikamoo nyanya!

**Babu** - Mzazi wa kiume wa baba au mama.

***Matumizi katika sentensi:*** Kwaheri babu!

**Kijana** - Mtu wa umri wa kubalehe, mvulana ama msichana.

***Matumizi katika sentensi:*** Waambaje kijana mwenzangu?

**Buriani** - Maagano ya kuachana kwa muda mrefu.

***Matumizi katika sentensi:*** Buriani Juma. Tuonane mwaka ujao.

**Makiwa** - Tamko la kumpa pole mtu aliyepata msiba wa kufiwa.

***Matumizi katika sentensi:*** Makiwa jirani kwa kumpoteza mwanao.

**Alamsiki** - Neno la kuagana wakati wa usiku.

***Matumizi katika sentensi:*** Alamsiki Aisha.

**Hongera** - Neno la kupongeza mtu.

***Matumizi katika sentensi:*** Hongera kwa serikali yetu kwa uongozi bora.

## *Zoezi la 1*

**Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua na kuandika katika daftari lako jibu sahihi.**

**Mfano:**

Tamko la kuagana wakati wa usiku.

(Alamsiki, Kwaheri)

**Jibu:** Alamsiki

1. Jibu la: Makiwa. ______________________

   (Tunayo, Salama)

2. Jibu langu ni: Nishapoa. ______________________

   (Pole, Makiwa)

3. Neno la kupongeza. ______________________

   (Kwaheri, Hongera)

4. Jibu la: Buriani. ______________________

   (Tunayo, Buriani dawa)

5. Salamu ya mtoto kwa mtu mzima. ______________________

   (Shikamoo, Karibu)

## *Zoezi la 2*

**Kwa ushirikiano na mwenzako aliye karibu nawe, tafuta majibu ya maamkizi yafuatayo:**


1. Waambaje? - ______________________
2. Hodi! - ______________________
3. Pole! - ______________________

4. Salama? - ____________________

5. Kwaheri! - ____________________

## B. Mazungumzo yenye maamkizi

**Soma kwa sauti salamu baina ya Daktari na Gasore.**



**Gasore:** Shikamoo daktari!

**Daktari:** Marahaba Gasore. Karibu.

**Gasore:** Asante.

**Daktari:** Habari ya leo?

**Gasore:** Njema, lakini mimi naugua.

**Daktari:** Unaugua wapi Gasore?

**Gasore:** Midomo yangu imevimba. Nashindwa hata kula. Nahisi uchungu sana.

**Daktari:** Pole sana Gasore.

**Gasore:** Nishapoa.

**Daktari:** Nitakupima kisha nitakupa dawa ya kupunguza uchungu huo.

**Gasore:** Asante sana daktari.

**Daktari:** Karibu.

### *Zoezi la makundi*

1. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, igizeni maamkizi baina ya Gasore na Daktari.
2. Kwa ushirikiano na wenzako darasani, eleza maamkizi wanayoyatumia kwa kuyataja.

### *Zoezi la ufahamu*

1. Gasore anazungumza na nani?
2. 'Marahaba' ni jawabu la salamu gani?
3. Ni kwa nini Gasore anazungumza na Daktari?
4. Ili kumpa Gasore moyo, Daktari alimwambia nini?
5. Gasore alitumia neno 'Asante'. Unadhani ni kwa nini alitumia neno hilo?

### *Zoezi la ziada*

Igiza maamkizi mengine kati ya watu wawili kwa vikundi vya wanafunzi wawili wawili. Zingatia mazungumzo yaliyopo hapo juu.

## C. Sarufi

### Nafsi za Kiswahili

Simama mbele ya wanafunzi wenzako kisha uwaamkie na ujitambulishe.

### Tathmini

a) Ulianzaje kujitambulisha?

b) Unajua lugha ya Kiswahili ina nafsi ngapi? Waambie wenzako.

### Maelezo muhimu

- Kila binadamu ana lugha, utamaduni na hulka yake lakini pia kila binadamu anawahitaji wenzake.
- Lugha ya Kiswahili ina nafsi tatu ambazo zinajitokeza katika umoja na wingi.

• MIMI, WEWE, YEYE, SISI, NYINYI, na WAO ndizo nafsi za Kiswahili.

## Mifano ya kujitambulisha kwa kutumia nafsi za Kiswahili

| | |
|---|---|
|  |  |
| 1. Ninaitwa Sonia. (Mimi) | Tunaitwa Sonia. (Sisi) |
|  |  |
| 2. Unaitwa Mugisha. (Wewe) | Mnaitwa Mugisha. (Nyinyi) |
|  |  |
| 3. Anaitwa Gatete. (Yeye) | Wanaitwa Gatete. (Wao) |

**Jitambulishe kisha uwatambulishe wenzako ukitumia nafsi zilizo hapo juu.**

1. Mimi ninaitwa ___________________.
2. Wewe unaitwa ___________________.
3. Yeye anaitwa ___________________.
4. Sisi tunaitwa ___________________.
5. Nyinyi mnaitwa __________________.
6. Wao wanaitwa ___________________.

**Waambie wenzako nao wajitambulishe kwa kufuata mfano uliopo hapo juu.**

## Maelezo muhimu

- Nafsi za Kiswahili hujitokeza katika umoja na wingi kama ifuatavyo:

| Umoja (A) | Wingi (B) |
|---|---|
| Mimi | Sisi |
| Wewe | Nyinyi |
| Yeye | Wao |

## Matumizi katika sentensi:

**Umoja** — **Wingi**

1. Mimi ninapenda amani. - Sisi tunapenda amani.
2. Wewe unafunga mfereji. - Nyinyi mnafunga mifereji.
3. Yeye anaokota uchafu. - Wao wanaokota uchafu.

*Zoezi la 1*

**1. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, linganisha nafsi za umoja (A) na zile za wingi (B) kwa usahihi.**

| | A | B |
|---|---|---|
| a) | Mimi | Wao |
| b) | Wewe | Sisi |
| c) | Yeye | Nyinyi |

**2. Sasa kwa kujitegemea, tunga sentensi sahihi kwa kutumia nafsi zote tatu katika umoja na wingi.**

**Mfano:**

Mimi ni mzalendo. - Sisi ni wazalendo.

## D. Matamshi na tahajia bora

1. **Kwa ushirikiano na mwenzako, soma kwa sauti na kwa zamu sauti ambatano za konsonanti za Kiswahili zifuatazo:**

[**Gh**]

**Gh**ala, **gh**amidha, lu**gh**a, **gh**ulamu

[**Nd**]

**Nd**ani, **nd**imu, **nd**oano, **nd**oa, **nd**imi

[**Ng**]

**Ng**eli, ke**ng**ele, **ng**eni, **ng**ao, **ngamia**

[**Mb**]

**Mb**uzi, **mb**ilikimo, **mb**ili, tu**mb**ili, **mb**u

**2. Andika kwa hati nzuri maneno yenye sauti ambatano ambayo utasomewa na mwenzako kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu.**

## E. Mjadala/Mazungumzo

Kwa kutumia nafsi za Kiswahili kwa usahihi, zungumza na wenzako juu ya 'Umuhimu wa kuamkiana'.

# Matumizi ya Nafsi na Viwakilishi vya Nafsi katika Maamkizi

## A. Maamkizi yenye nafsi katika umoja na wingi

**Soma maamkizi yafuatayo yenye viwakilishi vya nafsi.**

| | A | | B | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Mimi:** | *Sijambo.* | **Sisi:** | *Hatujambo.* |
| 2. | **Wewe:** | *Hujambo?* | **Nyinyi:** | *Hamjambo?* |
| 3. | **Yeye:** | *Hajambo.* | **Wao:** | *Hawajambo.* |
| 4. | **Mimi:** | *Habari yangu ni njema.* | **Sisi:** | *Habari zetu ni njema.* |
| 5. | **Wewe:** | *U hali gani?* | **Nyinyi:** | *M hali gani?* |
| 6. | **Yeye:** | *Ameshindaje?* | **Wao:** | W*ameshindaje?* |

Baada ya kusoma kwa makini maamkizi katika A na B, eleza wenzako unachogundua katika kila kikundi.

### Maelezo muhimu

- Haya ni maamkizi.
- **A** ni maamkizi katika umoja na **B** ni wingi wa maamkizi katika **A.**
- Nafsi mbalimbali zimetumika.

**Sasa unaweza kukumbuka tulichosema kuhusu nafsi? Tumia maswali yafuatayo kukumbuka.**

a) Kiswahili kina nafsi ngapi?

b) Unaweza kuzitaja nafsi hizo katika umoja na katika wingi? Shirikiana na wenzako kupata jawabu.

**Baada ya kutoa maoni yako, angalia mifano ifuatayo kisha uisome kimyakimya kwa makini.**

1. Mimi naitwa Iragena. - Sisi tunaitwa Iragena.
2. Wewe unaitwa Gahigi. - Nyinyi mnaitwa Gahigi.
3. Yeye anaitwa Nirere. - Wao wanaitwa Nirere.

### Kusoma mifano ya salamu kwa matamshi sahihi

Soma kimyakimya mifano ya salamu iliyo katika utangulizi uliopo hapo juu. Kisha kwa ushirikiano na wenzako, soma tena kwa sauti na kwa kubadilishana kwa kuzingatia matamshi bora. Tatueni kila tatizo la matamshi linalotokea. Fanya utafiti katika kamusi ya Kiswahili.

## B. Msamiati wa viwakilishi vya nafsi

Soma tena maandishi yaliyo mwanzoni mwa somo hili. Andika maneno yote mapya kisha utambue maana yake kwa kuzingatia jinsi yalivyotumika.

### *Zoezi la 1*

**Andika majibu katika daftari lako kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwa majibu yaliyo mabanoni.**

**Mfano:** ______________ ninaitwa Nshuti. (Wewe, Mimi)

**Jibu:** Mimi ninaitwa Nshuti.

1. Wewe ______________. (Unanikumbuka, ninakumbuka)
2. ______________ anaitwa Samantha. (Yeye, Wewe)
3. ______________ mnaitwa. (Nyinyi, Wao)
4. ______________ wanasoma. (Wao, Wewe)
5. ______________ tunalima. (Sisi, Nyinyi)

### *Zoezi la 2*

**Kwa msaada wa wenzako, tunga sentensi sahihi kwa kutumia:** mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi na wao.

**Mfano:** Sisi ni wanafunzi.

### *Zoezi la ziada*

**Kwa ushirikiano na wenzako, jibu maswali yafuatayo kutokana na uliyosoma kuhusu nafsi:**

1. Mfano wa nafsi ni ____________ na ______________.
2. Umoja wa 'Hatujambo' ni ____________.
3. Jibu kwa kuteua neno sahihi.
   a) Habari, hujambo; ni maamkizi. (Ndio, La)
   b) Mimi, nyinyi, yeye; ni nafsi (Ndio, La)
   c) Mimi, wewe, yeye ni umoja wa (Sisi, Wao, Nyinyi) ama (Sisi, Nyinyi, Wao) ama (Wao, Nyinyi, Wao)?
4. Rwanda ni nchi ____________. (yetu, sisi)
5. Andika kwa umoja kwa kuteua jawabu sahihi kati ya yale yaliyo kwenye mabano.

| Wingi | Umoja |
|---|---|
| Sisi | |
| Nyinyi | |
| Wao | |

## C. Sarufi

### Nafsi za Kiswahili

Kwa kutumia maarifa uliyopata mwanzoni mwa somo hili, tambua wingi wa nafsi za Kiswahili zifuatazo:

**Tumia jedwali hili:**

| Wingi | Umoja |
|---|---|
| Mimi | |
| Wewe | |
| Yeye | |

Tunga sentensi kwa kutumia nafsi hizi katika umoja na wingi.

**Mfano:** *Mimi ni Mnyarwanda.* - *Sisi ni Wanyarwanda.*

## Kazi ya kikundi

**Unakumbuka somo kuhusu kujitambulisha?**

a) Ninaitwa Mugisha.

b) Unaitwa Munezero.

c) Anaitwa Mushikiwabo.

**Unaweza kuwaelezea wenzako kwa nini ulianza na 'ni', 'u' na 'a'?**

1. Ninaitwa (mimi) - Tunaitwa (sisi)
2. Unaitwa (wewe) - Mnaitwa (nyinyi)
3. Anaitwa (yeye) - Wanaitwa (wao)

**Kumbuka**

- 'ni', 'u', 'a' 'tu', 'm' na 'wa' ni viambishi vya nafsi mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi na wao mtawalia.

*Zoezi la 1*

**Kwa ushirikiano na wenzako, onyesha nafsi zinazochukua viambishi vya nafsi vilivyotajwa.**

**Mfano:** Ni - __________
**Jibu:** Mimi

1. a - __________
2. tu - __________

3. wa - __________

4. u - __________

5. m - __________

*Zoezi la 2*

**Kamilisha maamkizi yafuatayo kwa kutumia nafsi katika umoja ama wingi.**

**Mfano:** __________ sijambo.

**Jibu:** Mimi

1. __________ hatujambo.
2. __________ hawajambo.
3. __________ m hali gani?
4. __________ waambaje?
5. __________ ni mzima.

*Zoezi la mjadala*

**Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadili kauli hii:**

**'Nafsi inaweza kutugawanya ama kutuunganisha kijinsia na kama nchi.'**

## D. Matamshi ya konsonanti na tahajia bora

**1. Soma maneno yafuatayo kwa sauti kwa kutamka konsonanti kulingana na utaratibu wa sauti husika. Sikiliza kwa makini namna wenzako wanavyoyatamka.**

**[k]**

Kaka, kalamu, keti, korti, kazi, baki

**Matumizi katika sentensi:**

a) Kalamu hii ni ya mwalimu.

b) Koti la baba limepigwa pasi.

**[b]**

Baba, barua, babu, bodi, bati

Matumizi katika sentensi:

a) Barua ile ilitumwa jana.

b) Baba amenunua gazeti.

**[p]**

Pesa, peni, penseli, pasha, pisha

Matumizi katika sentensi:

a) Pesa zake ni nyingi.

b) Hii ni penseli ya mtoto wangu.

### 2. Zoezi la Imla:

Andika kwa hati nzuri na ukamilifu maneno ambayo utasomewa na mwalimu wako.

## E. Maswali ya Marudio

### 1. Katika daftari lako, andika katika umoja.

**Mfano:** Mwaambaje? – Waambaje?

| Wingi | Umoja |
|---|---|
| M wazima? | |
| M hali gani? | |
| Hamjambo? | |
| Hawajambo? | |

**2. Kwa zamu, jitambulishe na uwatambulishe wenzako.**

**Mfano**: Ninaitwa Maria.

a) Ninaitwa _______________.

b) Anaitwa _______________.

c) Unaitwa _______________.

**3. Jibu kwa maneno bora ya kuagana.**

**Mfano:** Kwaheri – Ya kuonana

a) Tuonane kesho _______________.

b) Buriani _______________.

c) Lala salama _______________.

d) Alamsiki _______________.

**4. Shirikiana na wenzako darasani kugundua maneno yanayofaa zaidi kujazia nafasi zilizoachwa wazi.**

_______________ mwalimu! Tafadhali _______________ kalamu yako. _______________, nimechelewa. _______________ mwalimu. Mzazi pia _______________.

**5. Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno haya:**

**Mfano:** Mama ananiamkia.

a) Pole b) Asante c) Tafadhali

d) Naomba e) Habari

**6. Onyesha viambishi vya nafsi zilizotajwa.**

**Mfano:** Mimi - ni

a) Sisi - ____________

b) Wewe - ____________

c) Nyinyi - ____________

d) Yeye - ____________

e) Wao - ____________

## Faharasa

**Maamkizi:** Salamu; maneno ya kujuliana hali

**Kiwakilishi:** Neno linalochukua nafasi ya nomino ama kiwakilishi kingine

**Baba:** Mzazi wa kiume

**Mama:** Mzazi wa kike

**Mwalimu:** Mtu anayempa mtu mwingine elimu ama maarifa

**Nafsi:** Mtu mwenyewe, binafsi

**Mwanafunzi:** Mtu aliye chini ya mwalimu kwa lengo la kupata elimu na maarifa

**Jirani:** Mtu aliye karibu nawe; anayeishi karibu nawe

**Muuzaji:** Mtu anayeuza bidhaa kwa watu wengine kwa kubadilisha hasa kwa pesa

**Mnunuzi:** Mtu anayetoa pesa ama kitu kingine ili kupata bidhaa kutoka kwa muuzaji

**Msamiati:** Maneno mapya ambayo yanapatikana katika taarifa/kifungu

**Hujambo?:** Huna jambo?

**Sijambo:** Sina jambo

**Habari:** Taarifa, ujumbe; salamu (kujuliana hali)

**Shikamoo:** Salamu ya heshima inayotolewa kwa mtu mwenye umri mkubwa kukuliko

**Marahaba:** Kiitikio cha salamu iliyotolewa kwa neno 'shikamoo'

**Makiwa:** Salamu kwa mtu aliyepatwa na msiba hasa wa kifo

**Tunayo:** Kiitikio cha salamu iliyotolewa kwa mtu aliyepata msiba hasa wa kufiwa

**Sabalheri:** Salamu ya kujulia mtu hali wakati wa asubuhi

**Masalheri:** Salamu za jioni

**Pole:** -enye utulivu, taratibu. Salamu za kutakia mtu utulivu.

**Waambaje:** Wasemaje? Unasema nini?

**Twika:** Wekea kichwani, begani; bebesha; twisha

**Buriani:** Salamu za kumuaga mtu ambaye hamtaonana kwa muda mrefu

**Msichana:** Mtoto wa kike

**Mvulana:** Mtoto wa kiume

**Alamsiki:** Salamu za kuagana usiku

**Shirikiana:** Fanya pamoja na wenzako. Kuwa katika kikundi

## Mada Kuu:
# Matumizi ya Lugha Katika Mazingira Mbalimbali

## Mada Ndogo:
# Msamiati Katika Mazingira ya Shule

**Somo la Kwanza:** Mazungumzo shuleni

**Somo la Pili:** i) Mazungumzo kati ya wanafunzi

ii) Ratiba ya mwanafunzi ya wiki

**Somo la Tatu:** Viongozi wetu shuleni

**Somo la Nne:** Shule yangu


**Somo la Tano:** Usafi shuleni

# Mazungumzo Shuleni

## A. Mazingira ya darasani

**Tazama picha hizi:**






**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazama picha hizi halafu tunga sentensi kwa kueleza kile kinachoendelea. Tanguliza sentensi yako kwa:**

Mimi ninaona…

**Mfano:** Mimi ninaona wanafunzi.

**Soma mazungumzo yafuatayo baina ya wanafunzi na mwalimu wao.**

**Mutoni:** Habari za asubuhi Musafiri?

**Musafiri:** Nzuri.

**Mutoni:** Umefanya zoezi la Kiswahili ?

**Musafiri:** Ndiyo.

**Mutoni:** Na mimi pia nimefanya zoezi hilo.

**Musafiri:** Lakini, swali la kwanza ni gumu.

**Mutoni:** Hapana. Swali la kwanza ni rahisi sana.

**Musafiri:** Kila siku, mwalimu wetu hutupatia mazoezi ya kufanyia nyumbani.

**Mutoni:** Ndiyo. Ni mwalimu mzuri sana. Yeye anatufundisha vizuri na anatupenda.

**Musafiri:** Ndiyo. Eh! Kengele inalia.

**Mutoni:** Twende…twende haraka tusichelewe. Mwalimu anaweza kutupa adhabu.

**Musafiri:** Ndiyo. Twende haraka. Wenzetu wanajipanga mbele ya darasa letu.

*(Mutoni na Musafiri wanajiunga na wanafunzi wenzao. Wanafunzi wote na mwalimu wao wanaingia darasani.)*

**Mwalimu:** Hamjambo wanafunzi?

**Wanafunzi:** Hatujambo. Shikamoo mwalimu.

**Mwalimu:** Marahaba. Ketini. Mutoni, umefanya zoezi la Kiswahili?

**Mutoni:** Ndiyo Mwalimu.

**Mwalimu:** Leta daftari lako hapa. Hum! Mbona umeharibu daftari lako? Hujui kuwa unapaswa kutunza vizuri daftari lako?

**Mutoni:** Samahani mwalimu! Mvua ilininyeshea.

**Mwalimu:** Sawa. Kumbukeni…ni muhimu sana kutunza vizuri madaftari na vitabu vyenu.

**Wanafunzi:** Sawa mwalimu.

**Mwalimu:** Sasa ni wakati wa kufanya jaribio. Wekeni vitabu na madaftari katika madawati yenu.

**Wanafunzi:** Ndiyo mwalimu.

**Mutoni:** Samahani mwalimu! Mimi sielewi swali la kwanza.

**Mwalimu:** Swali la kwanza… Kila mwanafunzi anachagua jibu sahihi kati ya A, B na C.

**Mutoni:** Sawa mwalimu.

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma mazungumzo hapo juu kati ya wanafunzi na mwalimu, kisha ujibu maswali yanayofuata kwa kuchagua jibu sahihi kati ya yale yaliyopendekezwa mabanoni.**

1. Musafiri amefanya _______________ (zoezi/daftari) la Kiswahili.
2. Swali la kwanza ni_______________ (gumu/rahisi) kwa Musafiri.
3. Swali la kwanza ni _______________ (gumu/rahisi) kwa Mutoni.
4. Mwalimu huwapa wanafunzi _______________ (daftari/kazi ya nyumbani) kila siku.
5. Mutoni na Musafiri wanaenda haraka kwa sababu _______________ (mwanafunzi/kengele) inalia.
6. Wanafunzi _______________ (wajambo/hawajambo).
7. Daftari la Mutoni _______________ (limeharibika/linanyesha).
8. Mutoni _______________ (amenyeshewa/ameharibiwa) na mvua.
9. Wanafunzi wanaweka vitabu na madaftari katika madawati yao. Sasa ni wakati wa kufanya _______________ (kazi ya nyumbani/jaribio).
10. Kila mwanafunzi anachagua _______________ (jibu/kiti) sahihi.

## B. Msamiati wa mazingira ya shuleni

### *Zoezi la 1*

**Jipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili msome sentensi zifuatazo na kujadiliana. Husisha sentensi hizi na shughuli mbalimbali katika darasa lako.**

**Mfano:**

a) Wanafunzi wamo darasani na mwalimu wao amesimama mbele ya darasa.

b) Kalisa ananyosha mkono ili ajibu swali la mwalimu.

c) Mwanafunzi anampatia mwenzake kalamu ili aandike zoezi la Kiswahili.

d) Kengele inalia. Sasa ni wakati wa kuingia darasani.

e) Wanafunzi wote wanajipanga mbele ya darasa lao.

f) Mvua inawanyeshea wanafunzi.

g) Vitabu na madaftari yanaharibika.

h) Ni muhimu kutunza madaftari yetu. Sasa ninafunika daftari langu ili lisiharibike.

i) Mwalimu anaandika zoezi ubaoni.

j) Jibu sahihi la moja kuongeza mbili ni tatu.

k) Mutoni anaweka madaftari yake juu ya meza.

### *Zoezi la 2*

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kamilisha sentensi zinazofuata kwa kutumia msamiati unaofaa kati ya huu uliopewa:**
*Kiti, ninatunza, adhabu, madawati, gumu, ubaoni, jaribio, Samahani, anatupenda, muhimu*

1. Kiswahili ni somo _______________ kwa wanafunzi.
2. Mwalimu anauliza swali _______________ kwa wanafunzi.
3. Mwalimu anaandika _______________.
4. _______________ cha mwalimu kiko mbele ya darasa.
5. Wanafunzi wanaweka vitabu katika _______________ yao.
6. Mimi _______________ vifaa vya shule; vitabu, madaftari na kalamu.
7. Mutesi ameharibu daftari lake. Mwalimu atampatia _______________.
8. Sisi tumeshinda _______________la Kiswahili.
9. _______________ ! Mwalimu. Ninaomba ruhusa ya kuenda haja.
10. Mwalimu _______________ sana kwa sababu tunasoma vizuri.



*Zoezi la 3*

**Kwa kutumia mshale, husisha vifaa katika sehemu A na matumizi yake katika sehemu B.**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. Kifutio | A. Kukaa |
| 2. Kitabu | B. Kuweka vitabu |
| 3. Kiti | C. Kufuta maandishi daftarini |
| 4. Kabati | D. Kuchora mistari |
| 5. Dawati | E. Kufuta ubao |
| 6. Raba | F. Kusoma |
| 7. Penseli | G. Kuandika masomo na mazoezi |
| 8. Rula | H. Kuonyesha wakati |
| 9. Saa | I. Kuchora picha |
| 10. Chaki | J. Kuandika ubaoni |
| 11. Daftari | K. Kuandika, kukaa, kuweka vitabu na madaftari ya wanafunzi |

## C. Shughuli za siku za mwanafunzi

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni picha zilizochorwa hapa chini, kisha mueleze kile kinachoendelea kwa kuhusisha sentensi zilizotolewa chini yake:**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
|  |  |  |  |  |

| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|
|  |   |  |  |  |

## Ratiba ya siku ya Kalisa

| **Saa** | **Shughuli** |
|---|---|
| **12:00 alfajiri:** | Kalisa anaamka. |
| **12:10 alfajiri:** | Kalisa anaenda bafuni kuoga. |
| **12:30 asubuhi:** | Baada ya kuvaa sare, kuchana nywele na kupiga mswaki, Kalisa anapata kifungua kinywa kwa kunywa chai kwa kiazi kitamu na ndizi iliyoiva. |
| **12:35 asubuhi:** | Kalisa anaenda shuleni. Mama yake anamuaga. |
| **12:40 asubuhi:** | Kalisa anakutana na Gatete na Akaliza njiani. |
| **1:00 asubuhi:** | Kalisa, Gatete na Akaliza wanaenda shuleni pamoja. |
| **1:35 asubuhi:** | Kalisa, Gatete na Akaliza wanafika shuleni na kukutana na wanafunzi wenzao. |
| **1:45 asubuhi:** | Kengele inalia. Ni wakati wa kuingia darasani. |
| **1:50 asubuhi:** | Wanafunzi wote wanajipanga kwa msururu mbele ya darasa lao. |
| **2:00 asubuhi:** | Wanafunzi wanaingia madarasani. |
| **2:00 - 2:40 asubuhi:** | Somo la Hisabati linaanza. |

## Shughuli zinazofuata:

| | |
|---|---|
| **2:50 - 3:30 asubuhi:** | Somo la Hisabati linaendelea. |
| **3:40 - 4:20 asubuhi:** | Somo la Kiswahili linaanza. |

| | |
|---|---|
| **4:20 - 4:40 asubuhi:** | Pumziko fupi. Wanafunzi wengine wanakimbia msalani, wengine wanacheza nje ya madarasa yao. |
| **4:40 -5:20 asubuhi:** | Somo la Historia linaanza. |
| **5:30 -6:10 adhuhuri:** | Somo la Historia linaendelea. |
| **6:20 -7:00 adhuhuri:** | Somo la Bayolojia linaanza. |
| **7:00 - 8:00 adhuhuri:** | Wanafunzi wanaenda bwaloni ili kupata chamcha. |
| **8:00 - 8:40 alasiri:** | Somo la Jiografia linaanza. |
| **8:50 -9:30 alasiri:** | Somo la Fizikia linaanza. |
| **9:40 - 10:20 jioni:** | Somo la Kiingereza linaanza. |
| **10:30 - 11:20 jioni:** | Wanafunzi wanaenda uwanjani kushirki katika michezo mbalimbali kama vile kandanda, mpira wa vikapu, riadha na voliboli. Ifikapo saa kumi na moja u nusu wanafunzi wote huruhusiwa kwenda nyumbani. |

*Zoezi*

**Kwa ushirikiano na wenzako, zungumzieni shughuli zenu kuanzia kuamka, kufika darasani hadi kurudi nyumbani jioni.**

## Maigizo ya shughuli za mwanafunzi

Katika makundi ya wanafunzi watano, jaribu kuigiza mazungumzo hapo juu kati ya  wanafunzi na mwalimu.

## Ratiba ya mwanafunzi ya wiki

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni ratiba ifuatayo.**

Gasimba ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule ya Bwiza. Yeye ni mwanafunzi mwenye bidii na huwa hachelewi shuleni.Jumatatu, Gasimba huamka saa kumi na moja na nusu alfajiri na kuanza kujiandaa kwenda shuleni. Yeye husali kwa dakika ishirini kisha huenda bafuni kukoga. Baadaye, yeye hupiga meno yake mswaki, huchana nywele zake na kuvaa sare yake.

Mamake Gasimba huamka mapema zaidi ili kumwandalia mwanawe kiamsha kinywa. Gasimba hunywa chai kwa mkate kisha hubeba mkoba wake wenye madaftari na vitabu vyake kuelekea shuleni. Gasimba humuaga mamake na kuondoka. Gasimba hufika shuleni saa kumi na mbili u nusu na kuingia darasani na kuanza kusoma. Yeye huwatangulia wanafunzi wengine.

Saa mbili kasorobo kengele hulia na wanafunzi wote huenda kwenye gwaride ambapo wao husali kisha huimba nyimbo za kumsifu Mungu, na baadaye hupandisha bendera huku wakiimba wimbo wa taifa la Rwanda. Mwalimu mkuu huwahutubia wanafunzi kisha kumpisha mwalimu wa zamu kuwapa wanafunzi matangazo yoyote muhimu.

Saa mbili kamili kwa somo la kwanza. Baada ya masomo mawili wanafunzi hupewa dakika ishirini za mapumziko. Chakula cha mchana huliwa saa saba kamili. Masomo huendelea kuanzia saa nane alasiri.Saa kumi na dakika ishirini masomo ya siku huwa yamekamilika. Wanafunzi wote huenda uwanjani kwa michezo mbalimbali kama kandanda, voliboli na kuruka kamba. Ifikapo saa kumi na moja u nusu wanafunzi wote kuelekea nyumbani.

Gasimba afikapo nyumbani, yeye humsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani kisha hapo baadaye yeye hufanya kazi zake za ziada za shuleni kabla ya kulala ifikapo saa tatu u nusu usiku.

Kila siku ya wiki huhusisha matukio haya ila siku ya Alhamisi jioni ambapo kina Gasimba hufanya mazoezi ya kuogelea katika dimbwi lao. Ijumaa jioni wanafunzi hushiriki katika mjadala kuhusu mada ambazo walimu wao huwa wamewachagulia. Jumamosi, Gasimba humsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani. Jumapili wao huenda kanisani. Baadaye, Gasimba hupumzika. Kisha hujitayarisha kwa ajili ya kwenda shuleni Jumatatu.

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena kifungu kilicho hapo juu kisha ujibu maswali yafuatayo.**

1. Gasimba anasoma katika shule gani?
2. Je, Gasimba yuko katika kidato cha tatu?
3. Gasimba hufanya nini anapoamka kabla ya kustaftahi?
4. Baina ya Gasimba na mamake, nani huamka mapema zaidi?
5. Gasimba hufanya nini afikapo shuleni kabla wanafunzi wengine wafike?

6. Nani huwahutubia wanafunzi kwenye gwaride?
7. Gasimba na wanafunzi wenzake hufanya nini Alhamisi na Ijumaa jioni baada ya masomo yao?
8. Gasimba hufanya nini Jumamosi?
9. Taja shughuli za Gasimba za siku ya Jumapili?
10. Eleza maana ya msamiati ufuatao:
    a) Kiamsha kinywa
    b) Sare
    c) Mjadala
    d) Kandanda

# Mazungumzo Kati ya Wanafunzi

## A. Mazungumzo ya wanafunzi

**Tazama picha hii:**




Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni picha hii halafu tungeni sentensi kwa kueleza kile kinachoendelea.

**Mfano:** Wanafunzi wanacheza kandanda.

**Soma kifungu cha mazungumzo kinachofuata kati ya Kalisa, Mutoni na Birasa.**

**Kalisa**: Mimi ninapenda mchezo wa kandanda. Je, wewe unapenda mchezo gani?

**Mutoni:** Mimi ninapenda mchezo wa voliboli. Je, Birasa pia anapenda mchezo wa voliboli?

**Kalisa:** Ndio. Yeye pia anapenda mchezo wa voliboli.

**Mutoni:** Ooh! Wewe na Birasa mnapenda mchezo wa voliboli.

**Kalisa:** Kweli! Mimi na Birasa tunafurahia mchezo huo sana.

**Mutoni:** Na Muhire hufurahia mchezo upi?

**Kalisa:** Muhire hupenda kucheza mchezo wa vikapu. Urefu wake unamfaa sana katika mchezo huo.

**Mutoni:** Lakini, Muhire ni mwanafunzi mbaya. Yeye hupiga kelele darasani.

**Kalisa:** Ndiyo. Yeye ni mwanafunzi mtukutu na kila siku, yeye huchelewa kufika shuleni.

*(Birasa anajitokeza na Kalisa anamwita.)*

**Kalisa:** Birasa! Njoo hapa. *(Birasa anawakaribia)* Wewe unatoka wapi?

**Birasa:** Mimi ninatoka zahanatini.

**Kalisa:** Kwani wewe unaumwa?

**Birasa:** Ndiyo. Mimi ninaumwa…niliumia nilipokuwa nikicheza mchezo wa voliboli. . . ninataka kuomba ruhusa ya kuenda bwenini.

**Kalisa:** Pole sana! *(Akimuonyesha kwa kidole)* Mwalimu wa zamu amesimama karibu na uwanja wa kuchezea kandanda.

**Birasa:** Asante! Naenda kumuomba ruhusa ya kupumzika.

*(Birasa anaelekea upande aliko mwalimu wa zamu).*

**Mutoni:** Sasa twende tujiunge na wenzetu katika mchezo wa kandanda.

**Kalisa:** Ndiyo. Twende. Twende haraka.

*Zoezi la ufahamu*

**Soma tena mazungumzo yaliyo hapo juu, kisha ujibu maswali yafuatayo.**

1. Kalisa anapenda mchezo gani?
2. Mutoni anapenda mchezo gani?
3. Birasa anapenda mchezo gani?
4. Je, Birasa anapenda mchezo wa vikapu?
5. Tambua majina ya wanafunzi wanaopenda mchezo wa voliboli.
6. Ni mwanafunzi gani hupenda kupiga kelele darasani?
7. Mwalimu wa zamu yuko wapi?
8. Kwa nini Birasa anataka kumwona mwalimu wa zamu?
9. Birasa anatoka wapi?
10. Kwa nini Birasa anataka kuomba ruhusa?

## B. Msamiati wa shuleni

Jipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mtafute msamiati mpya katika kifungu cha mazungumzo hapo juu. Tafuta maana ya msamiati huo kulingana na matumizi yake katika kifungu hicho. Tumia kamusi ya Kiswahili pale panapohitajika.

*Zoezi*

**Tunga sentensi zako mwenyewe kwa kutumia maneno yafuatayo yaliyokolezwa rangi.**

1. Issa ni mwanafunzi mtukutu. Yeye anachelewa kila siku na anapenda kudanganya mwalimu.
2. Mimi ninatoka shuleni, ninaenda nyumbani.
3. Mwanafunzi huyu ni mgonjwa. Yeye anaumwa kichwa.

4. Mwanafunzi huyu ni mgonjwa. Yeye anaenda zahanatini kutibiwa.

5. Wanafunzi wanalala katika mabweni.

6. Mutesi anaanguka chini. Amina anampa pole.

**Msamiati wa ziada:**

- Mchezo wa vikapu
- Kandanda/Kabumbu
- Mchezo wa voliboli
- Riadha

## C. Sarufi

### Umoja na wingi wa vitenzi, viambishi na viwakilishi nafsi

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni sentensi zinazofuata katika umoja na wingi kisha mfanye zoezi linalofuata.

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| **Mimi nina**soma vizuri. | **Sisi tuna**soma vizuri. |
| **Wewe una**soma vizuri. | **Nyinyi mna**soma vizuri. |
| **Yeye ana**soma vizuri. | **Wao wana**soma vizuri. |

**Zoezi la 1**

a) Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi moja moja kwa kutumia kitenzi **cheza** katika nafsi zifuatazo: *mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi* na *wao*.

b) Linganisha sentensi zako na zile zilizotolewa hapo juu kuhusu kitenzi **soma**.

**Tafakari:**

- Sehemu zinazorudiwa ni **soma** na **cheza**. Hivi ni vitenzi. Som' katika kitenzi 'soma' na chez' katika kitenzi 'cheza' ndiyo mizizi ya vitenzi

hivyo. '-a-' ni kiambishi tamati.

- Katika umoja, **ni** inatumiwa kuwakilisha nafsi **mimi,** **u** inatumiwa kuwakilisha nafsi **wewe** na **a** inawakilisha nafsi **yeye**.
- Katika wingi, **tu** inatumiwa kuwakilisha nafsi **sisi,** **m** inatumiwa kuwakilisha nafsi **nyinyi** na **wa** inawakilisha nafsi **wao.**

### *Zoezi la 2*

**Katika daftari lako, jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia nafsi inayofaa.**

**Mfano:** _____________ anatembea haraka.

**Jibu:** Yeye anatembea haraka.

1. _____________ ninakimbia.
2. _____________ wanafundisha.
3. _____________ unatunza mazingira yako.
4. _____________ anaenda shuleni.
5. _____________ mnatumia pesa zenu vizuri.
6. _____________ tunafurahia usawa wa kijinsia.
7. _____________ wanalala mabwenini.
8. _____________ ninaingia darasani.
9. _____________ anachunguza nidhamu.
10. _____________ tunajali maslahi ya wanafunzi walemavu.

### *Zoezi la 3*

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andikeni sentensi zifuatazo katika umoja au wingi.**

**Mfano:** Yeye analipa kodi.
**Jibu: Wao wana**lipa kodi.

1. Wewe unacheza kandanda.
2. Yeye anakuja darasani.

3. Sisi tunaandika barua.
4. Mimi ninaketi kwenye kiti.
5. Nyinyi mnachoma majani.
6. Wao wanatembea njiani.
7. Wewe unaandika kwenye ubao.
8. Wao wanazungumza Kiswahili.
9. Mimi ninasimama mbele ya darasa.
10. Yeye anaimba wimbo wa taifa la Rwanda.

## D. Kusikiliza na Kuzungumza

***Zoezi la kuigiza***

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, igizeni mazungumzo kati ya wanafunzi yaliyotolewa hapo awali.**

***Zoezi la imla***

**Funga kitabu chako, kisha katika daftari lako, andika kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno utakavyosomewa na mwalimu wako**

## Somo la Tatu

# Viongozi Wetu Shuleni


## A. Mahusiano ya watu wanaopatikana shuleni




Mwalimu mkuu na tarishi



Mwalimu wa darasa na wanafunzi



Viranja wa shule



Walimu majilisini

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni picha zilizopo hapo juu, kisha mueleze kile kinachoendelea: Tangulizeni sentensi zenu kwa kutumia: **Mimi ninaona…**

**Mfano:** Mimi ninaona ofisi ya mwalimu mkuu.

**Soma kifungu cha habari kinachofuata kuhusu viongozi wetu shuleni.**

***(Kwizera ni mwanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Gikondo. Yeye ni mwanafunzi mzuri na anapenda viongozi wa shule yake.)***

Mimi ninaitwa Kwizera. Mimi ninasoma katika kidato cha kwanza. Shule yetu inaitwa shule ya Sekondari ya Gikondo. Kayitare ni kiranja wa darasa letu. Yeye hutuwakilisha katika mikutano mingi ya shule. Katika mikutano na mkuu wa shule, yeye huuliza maswali mazuri kwa sababu yeye ni mwanafunzi hodari sana. Mimi ninaelewa vizuri masomo yote; Kiswahili, Kinyarwanda, Kiingereza, Hisabati, Jiografia, Historia na mengine.

Shule yetu ina viongozi wazuri. Baadhi ya viongozi wa shule yetu ni mkuu wa shule, naibu wa mkuu wa shule, mwalimu wa mitaala ambaye ni mwalimu wa taaluma, mwalimu wa nidhamu, mhasibu na mkutubi anayesimamia maktaba ambapo vitabu vyetu huhifadhiwa. Shule yetu ina vitabu vingi.

Kila asubuhi, mkuu wa shule hutukagua ikiwa tumevaa sare. Yeye pia hutushauri kupenda masomo yetu, kusaidiana na kufanya kazi kwa bidii. Mwalimu wa mitaala hupanga masomo ya kila muhula. Mwishoni mwa kila muhula sisi hufanya mitihani. Mhasibu wa shule hupokea karo za wanafunzi. Mwalimu wa nidhamu huwaadhibu wanafunzi wanaofanya makosa: wanafunzi watukutu, wanafunzi wanaotoroka shuleni na wale wanaopiga kelele darasani.

Mwalimu mshauri wa wasichana, huchunguza nidhamu ya wasichana. Yeye hutatua shida zao shuleni, hutushauri kuwa na mienendo mizuri, huchunguza wakati wa kuingia mabwenini na kadhalika. Mwalimu mshauri wa wavulana huchunguza nidhamu ya wavulana na kupanga michezo shuleni kwa kushirikiana na mwalimu mshauri wa wasichana. Wakati wa chakula cha mchana na chakula cha jioni, walimu wa zamu huingia bwaloni kuchunguza chakula chetu na kutushauri kuheshimiana wakati wa kula. Mimi ninapenda sana viongozi wetu shuleni.

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena kifungu cha habari kilicho hapo juu kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Kwizera anasomea wapi?
2. Yeye anasoma katika kidato gani?
3. Kiranja wao ni nani?

4. Kwizera anaelewa vizuri masomo gani?
5. Viongozi wao ni nani?
6. Mwishoni mwa kila muhula wanafunzi hufanya nini?
7. Katika mikutano na mkurugenzi, kiranja wao hufanya nini?
8. Mkuu wa shule anaitwa nani?
9. Mkuu wa nidhamu huwaadhibu wanafunzi gani?
10. Walimu washauri huingia bwaloni kufanya nini?

## B. Msamiati kuhusu viongozi wa shuleni

Soma tena kifungu cha habari kilicho hapo juu na katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafuta maana ya maneno mapya yaliyojitokeza. Tumia kamusi ya Kiswahili pale panapohitajika.

***Zoezi la 1***

**Jipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili msome kwa sauti na matamshi sahihi sentensi zifuatazo. Maana za maneno yaliyokolezwa rangi zielezwe kwa kutumia kamusi panapohitajika.**

**Mfano:**

a) Sisi **tunavaa** **sare.** Kila asubuhi tunafanya **mkutano** na **mkuu wa shule**. Yeye anatushauri kupenda masomo yetu.

b) Mukamwiza ni **hodari** katika michezo ya riadha. Yeye huwa wa kwanza katika mbio za mita mia moja.

c) Mimi **ninalipa** **karo** ya shule yangu kupitia Benki ya SACCO na kuletea mhasibu wa shule **hati ya malipo** yangu.

d) **Kiranja wa darasa** na wanafunzi wenzake wanazungumza kuhusu masomo yao.

## *Zoezi la 2*

**Katika daftari lako, jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia moja kati ya maneno haya:** *muhula, Kiranja, mtihani, Mkuu, sare, wanatushauri, wavulana, mabwenini, bwaloni, mchana, anachunguza.*

**Mfano:** Walimu washauri ___________ kuheshimiana na wenzetu.

**Jibu:** Walimu washauri **wanatushauri** kuheshimiana na wenzetu.

1. Huu ni ___________ wa kwanza wa mwaka wa shule.
2. Tunafanya ___________ wa Kiswahili. Mwalimu wetu ametupa maswali rahisi.
3. Wanafunzi wote wa shule yangu wanavaa ___________.
4. ___________ wa darasa letu anaitwa Kagabo. Yeye anasimamia wanafunzi wenzake.
5. ___________ wa shule yetu ni mzuri sana. Yeye anaongoza shule vizuri.
6. Mwalimu mshauri wa wasichana ___________ nidhamu ya wasichana.
7. Mwalimu mshauri wa ___________ anapanga michezo shuleni.
8. Wanafunzi wanalala ___________.
9. Walimu washauri wanaingia ___________ kuchunguza chakula chetu.
10. Wakati wa chakula cha ___________ tunaenda bwaloni.

## *Zoezi la 3*

**Kwa kutumia mshale, husisha majina katika sehemu A na maelezo yaliyopo katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mkuu wa shule | A) Kufundisha wanafunzi |
| 2. Mhasibu | B) Kupokea karo ya shule |
| 3. Kiranja | C) Kutunza vitabu maktabani |

| | |
|---|---|
| 4. Mwalimu wa nidhamu | D) Kuchunguza nidhamu ya wanafunzi |
| 5. Mwalimu wa mitaala | E) Kuchunguza nidhamu ya wasichana na kuwashauri |
| 6. Mwalimu mshauri wa wasichana | F) Kuchunguza nidhamu ya wavulana na kuwashauri |
| 7. Mwalimu mshauri wa wavulana | G) Kusoma |
| 8. Walimu | H) Kusimamia wanafunzi |
| 9. Wanafunzi | I) Kupanga masomo ya wanafunzi |
| 10. Mkutubi | J) Kuongoza shule |

## C. Majina ya watu mbalimbali na kazi zao

Soma majina yafuatayo ya watu mbalimbali pamoja na maelezo ya kazi zao.

Kiranja: Kiongozi wa wanafunzi shuleni. Aghalabu huwa mwanafunzi.

Mwalimu: Mtu anayewapa wanafunzi elimu au maarifa.

Daktari: Mtu anayewatibu wagonjwa kwa kuwachunguza na kuwapa dawa.

Dereva: Mtu anayeendesha vyombo vinavyosafiri kwenye nchi kavu kama vile gari, baiskeli na pikipiki.

Kandawala: Mtu anayeendesha garimoshi.

Nahodha: Mtu anayeendesha vyombo vya majini kama vile meli.

Seremala: Mtu anayetengeneza vifaa vya mbao.

Mwashi: Mtu anayejenga nyumba za mawe.

Dobi: Mtu anayefua nguo na kuzipiga pasi kwa malipo.

Rubani: Mtu anayeendesha ndege.

Mkunga: Mtu anayesaidia kina mama kujifungua.

Rais: Kiongozi wa nchi iliyo Jamhuri.

Hakimu: Mtu anayeamua kesi mahakamani.

Mfinyanzi: Mtu anayefinyanga vyombo vya udongo.

Msusi: Mtu anayefanya kazi ya kusuka nywele, mikeka n.k.

### *Zoezi*

1. Jigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha mjadiliane kuhusu majina ya watu mbalimbali yaliyo hapo juu pamoja na kazi zao.
2. Tafiti kuhusu kazi za watu wafuatao:
    a) Mhariri
    b) Malenga
    c) Msasi
    d) Sogora
    e) Mhandisi

### *Zoezi la kutamka*

**Tamka maneno katika sentensi zifuatazo kwa usahihi.**

| | |
|---|---|
| 1. Viongozi wa shule | 6. Wanaingia bwaloni |
| 2. Chakula cha mchana | 7. Anatushauri |
| 3. Chakula cha jioni | 8. Mkurugenzi |
| 4. Anawachunguza | 9. Mkutano |
| 5. Anaingia bwenini | 10. Mwalimu mkuu |

*Somo la Nne*

# Shule Yangu

## A. Ufahamu

**Soma kwa makini kifungu cha habari kinachofuata kuhusu 'Shule Yangu.'**

***(Kamali ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mugano. Shule yake ni nzuri sana. Watu waliosomea kwenye shule yake sasa hivi ni watu wakubwa. Shule yake ina wanafunzi wazuri na walimu wazuri. Yeye anajivunia shule yake.)***

Mimi ninaitwa Kamali. Mimi ni mwanafunzi. Mimi ninasoma katika Shule ya Sekondari ya Mugano. Shule yangu ina madarasa mazuri sana. Madarasa ya shule yangu ni sawa na madarasa ya Shule ya Sekondari ya Kimya. Lakini shule yangu ina viongozi wazuri kuliko viongozi wa shule ya Kimya.

Mimi ninasoma katika kidato cha kwanza. Darasa letu ni kubwa sana na lina wanafunzi wazuri. Ndugu zangu Kagabo na Mutesi wanasoma katika kidato cha tatu lakini darasa letu ni kubwa kuliko darasa lao. Wao wana darasa dogo. Mimi ninapenda shule yangu.

Kayitare, Mulisa na Munyana walisomea katika shule yangu. Sasa Mulisa ni daktari katika hospitali kuu ya Kigali. Kayitare anajenga maghorofa marefu mjini Musanze na Munyana ni mwimbaji maarufu sana. Yeye ana wafuasi wengi mjini Kigali.

Kayitare, Mulisa na Munyana wanapenda kuja hapa mara nyingi kutembelea wanafunzi. Wao wanapenda sana wanafunzi wa shule yangu. Kwa kweli, shule yangu ina wanafunzi wazuri, werevu na wenye nidhamu. Sisi sote tunaelewa masomo yetu na tunasoma kwa bidii sana. Wasichana wanavaa marinda marefu na wavulana wanavaa suruali na mashati mazuri. Walimu wetu nao ni wazuri. Wao wanatufundisha masomo muhimu. Mimi ninajivunia shule yangu.

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena kifungu cha habari kilicho hapo juu kisha ujibu maswali yanayofuata:**

1. Mimi ninaitwa nani?
2. Mimi ninasoma wapi?
3. Ndugu zangu ni nani?
4. Wao wanasoma wapi?
5. Mimi ninasoma katika kidato gani?
6. Je, darasa la kagabo na Mutesi ni kubwa?
7. Munyana anafanya nini?
8. Kayitare anajenga nyumba wapi?
9. Je, Kalisa, Kayitare na Munyana walisomea wapi?
10. Wasichana na wavulana wanavaa nini?

### Msamiati kuhusu 'Shule yangu'

Soma tena kifungu cha habari kilichotangulia kisha katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafuta maana za maneno mapya yaliyojitokeza. Tumia kamusi ya Kiswahili pale panapohitajika.

**Kwa mfano:**
Shule - mahali ambapo wanafunzi hupata elimu au maarifa kutoka kwa walimu

***Zoezi la 1***

**Jipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha msome sentensi zifuatazo.**

a) Nyumba ya Kagabo ni **kubwa kuliko** nyumba ya Bugingo. Bugingo ana nyumba **ndogo.**

b) Shati langu ni **zuri kuliko** shati lako.

c) Kanziga ni **mwimbaji maarufu** sana. Yeye ana **wafuasi** wengi; watoto na watu wakubwa wanampenda.

d) Mwizere **anajenga ghorofa** mjini Nyamata.

e) Mugabo ni **fundi** mkubwa katika uchoraji. Yeye anaweza kuchora picha za wanyama, watu na hata ndege.

## Zoezi la 2

**Kwa kutumia mshale, husisha maneno katika sehemu A na maelezo yaliyopo katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Daktari | A. Mtu anayefanya kazi kama uashi, uchoraji, useremala, na kadhalika. |
| 2. Fundi | B. Mtu anayeimba |
| 3. Ghorofa | C. Mtu anayetibu wagonjwa |
| 4. Bidii | D. Mahali ambapo wagonjwa huenda kupata dawa |
| 5. Mwimbaji | E. Nguvu, jitihada au juhudi katika kutenda jambo |
| 6. Hospitali | F. Ninafurahia |
| 7. Ninajivunia | G. Watu wanaopenda kitu kama nyimbo, michezo, na kadhalika. |
| 8. Wafuasi | H. Nyumba ndefu |

## Zoezi la 3

**Kamilisha sentensi zinazofuata kwa kutumia maneno haya: *mwerevu, maarufu, ndefu, nzuri, wabaya, mwimbaji, fundi, mdogo, kuliko, sawasawa, bidii.***

**Mfano:** Wanafunzi wa shule yangu wanasoma kwa ______________. Wao wamejibu mazoezi yote ya Kiswahili.
**Jibu:** Wanafunzi wa shule yangu wanasoma kwa **bidii**. Wao wamejibu mazoezi yote ya Kiswahili.

a) Nyumba hii ni ______________. Nyumba hii ni safi sana.
b) Bagabo ni______________ wa uchoraji. Yeye anaweza kuchora picha za vitu vingi sana.
c) Mtoto huyu ni ______________ sana. Ana miaka mitatu.
d) Yeye alijenga nyumba ______________ sana. Nyumba yake inapendeza.

e) Kalisa ni mchoraji ______________ sana. Picha zake zinapendwa na watu wengi.

f) Mwanafunzi huyu ni ______________ kabisa. Yeye anafaulu masomo yote.

g) Yeye ni ______________ mzuri sana. Anaimba nyimbo za Mungu.

h) Mtoto huyu ni mdogo ______________ Amina. Yeye hatembei vizuri.

i) Kitabu hiki ni ______________ na kitabu changu. Vitabu vyote vinazungumzia somo la Kiswahili.

j) Watoto ______________ hawapendi kufanya mazoezi yao. Wao wanapiga kelele darasani.

## B. Kifungu cha ratiba ya masomo shuleni

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni picha zifuatazo na kueleza kinachoendelea:

**Soma kifungu kinachofuata kuhusu ratiba ya masomo ya wanafunzi.**

Mimi ninafurahia masomo yangu. Katika darasa letu, sisi tuna vipindi viwili vya somo la Kiswahili kwa wiki. Leo ni Jumatatu. Leo tunasoma Kiswahili, Hisabati na Bayolojia. Kesho ni siku ya Jumanne. Jumanne tunasoma Fizikia, Kemia na Historia. Jumatano tunasoma tena Kiswahili, Kiingereza na Kemia pia. Alhamisi tunasoma Kifaransa na Sanaa. Ijumaa tunasoma Kiingereza, Historia na Kifaransa pia.

Jumamosi na Jumapili ni siku za kupumzika; lakini mimi hurudia masomo yangu na kufanya mazoezi ya ziada. Mimi ninapenda sana somo la Kiswahili. Mwishoni mwa kila muhula tunafanya mtihani na mimi hufaulu.

**Baada ya kusoma kifungu hiki, orodhesha majina ya siku za wiki. Anzia Jumatatu hadi siku ya mwisho ya wiki. Bainisha shughuli za kila siku katika sentensi fupifupi kama zinavyozungumziwa hapo juu.**

**Mfano:** *Jumatatu* tunasoma Kiswahili, Hisabati na Bayolojia.

## C. Kusikiliza na kuzungumza

### 1. Tamka maneno yafuatayo kwa usahihi.

1. Jumatatu
2. Jumanne
3. Jumatano
4. Alhamisi
5. Ijumaa
6. Jumamosi
7. Jumapili
8. bidii
9. sawasawa
10. ninaitwa
11. mimi ninajivunia
12. maarufu
13. daktari
14. wafuasi
15. hospitali
16. kuliko
17. mwimbaji

### 2. Zungumzia shughuli unazozifanya nje ya darasa kuanzia Jumatatu hadi Jumapili.

## D. Sarufi

### Vivumishi vya sifa

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tungo zifuatazo. Baada ya kusoma, andikeni katika madftari yenu vifungu vya maneno vilivyokolezwa rangi katika kila sentensi.

1. Mwalimu wetu ana kiti kizuri.
2. Huyu ni mtoto mzuri sana. Yeye anaheshimu wazazi wake.
3. Kagabo ana nyumba mbaya lakini Muhire ana nyumba nzuri.
4. Huyu ni mtu mzima. Mimi ni mtoto mchanga.
5. Mtu huyu ana mkono mchafu. Mwambie aende kunawa.
6. Mwanafunzi huyu ana viatu vizuri.
7. Wanafunzi wa darasa langu wanavaa mashati mazuri.
8. Darasa langu lina madirisha makubwa.

9. Darasa la Kayitesi lina mlango mrefu.

10. Mwanafunzi anasoma kitabu kizuri.

### *Zoezi la 1*

**Linganisha maneno yaliyopigiwa mstari katika kila kifungu cha sentensi hapo juu.**

**Mfano:** Mwalimu wetu ana **kiti kizuri**.

**Jibu:** kiti kizuri: **ki** katika neno **kiti** ni sawa na **ki** katika neno **kizuri**.

**Tafakari:**

Kila kifungu kilichopigiwa mstari katika mifano hapo juu kina maneno mawili yenye viambishi mwanzoni vinavyofanana. Neno la pili linaeleza zaidi au linaongeza sifa na maana kwa neno la kwanza. Neno hili la pili ndilo kivumishi cha sifa.

**Mifano:**

a) **ki**ti **ki**zuri (kiti kina sifa ya kuwa kizuri; **kizuri** ni kivumishi cha sifa)

b) **m**toto **m**zuri (mtoto ana sifa ya kuwa mzuri; **mzuri** ni kivumishi cha sifa)

c) **m**kono **m**chafu (mkono una sifa ya kuwa mchafu; **mchafu** ni kivumishi cha sifa)

d) **m**lango **m**refu (mlango una sifa ya kuwa mrefu; **mrefu** ni kivumishi cha sifa)

### *Zoezi la 2*

a) Kwa kujitegemea, soma tena kifungu cha habari kilichotangulia, kisha uandike vifungu vyote vya maneno vyenye kuhusisha jina na kivumishi cha sifa.

**Mfano:** madarasa mazuri

b) Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, linganisheni shule mbili mnazozifahamu kwa kutumia vivumishi vya sifa.

**Mfano:** Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Yohana ina walimu wazuri kuliko shule ya Sekondari ya Kimisagara.

**Kivumishi ni neno linalotoa maelezo zaidi kuhusu nomino**

## Somo la Tano

# Usafi Shuleni

## A. Kifungu kuhusu usafi shuleni

Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tazameni picha zinazofuata na mweleze mnachokiona.







**Soma kifungu cha habari kifuatacho kuhusu usafi shuleni.**

***(Mutoni ni mwanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Bwiza. Shule yake ina wanafunzi wanaojali umuhimu wa usafi kushinda wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kimira. Shule ya Sekondari ya Kimira ni chafu sana.)***

Mimi ni Mutoni. Shule yangu inaitwa Bwiza. Sasa ni wakati wa kufanya usafi shuleni. Wanafunzi wa darasa la kwanza wanachukua majembe na kutengeneza bustani iliyo karibu na shule. Mimi na Kayitare tunasafisha vyoo. Aisha, Kabera na Marita wanafagia darasani. Mutesi na Muhire wanasaidia wengine kusafisha darasa letu. Shule yangu ina wanafunzi wavulana na wasichana. Wote husaidiana katika shughuli zote za usafi. Wakati wa mvua tunapanda miti na maua karibu na shule.

Mugabe na Musa wanasoma katika shule ya Kimira. Shule yao ni chafu sana.

Shule hii ina wanafunzi wavivu sana. Wao hutupa takataka popote. Wao hawasafishi madarasa yao na hawafui sare zao za shule. Wao hawachunguzwi vizuri na walimu wao na hawajali umuhimu wa usafi. Kweli, magonjwa huwashika mara kwa mara.

***Zoezi la ufahamu***

Soma tena kifungu cha habari kilicho hapo juu kuhusu 'Usafi Shuleni' kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Mutoni anasomea wapi?
2. Ni nani wanaofagia darasani?
3. Mutoni na Kayitare wanafanya nini?
4. Ni nani wanaosafisha vyoo?
5. Mugabe anasomea wapi?
6. Je, shule ya Kimira ni safi?
7. Shule ya Kimira inazungukwa na nini?
8. Je, wanafunzi wa shule ya sekondari ya Kimira wanajua umuhimu wa usafi?
9. Wanafunzi wa Kimira wanatupa wapi takataka?
10. Ni wanafunzi gani wanaofaulu katika masomo yao?

## B. Msamiati kuhusu usafi shuleni

**Soma tena kifungu cha habari kuhusu usafi shuleni na katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, tafuteni maana za maneno mapya yanayojitokeza. Tumia kamusi ya Kiswahili panapohitajika.**

**Kwa mfano:**

Bustani: Sehemu ya kupandia miti, maua, matunda au mboga

***Zoezi***

**Kwa kuzingatia mifano ya sentensi iliyobainishwa hapa chini, tunga sentensi nyingine kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari na kutiwa rangi.**

1. Nyumba yangu ni **safi**. Nyumba yangu ina rangi nzuri na huisafisha kila

asubuhi.

2. Si vizuri kutupa **takataka** karibu na nyumba yako. Takataka huharibu mazingira.

3. Kalisa ni **mchafu**. Yeye haogi kila siku.

4. Mama yangu ana **bustani** nzuri nyumbani. Bustani yake ina maua mazuri sana.

5. Mimi ninatoka **chooni.** Mimi ninanawa mikono yangu.

6. Kalisa anafagia darasani, yeye anapenda sana **usafi.**

7. Kila mwisho wa wiki, mimi hufua nguo zangu na **kusafisha** nyumba yetu.

8. Kamana na ndugu yake **wanasaidiana** kufanya kazi zote za nyumbani.

9. Lugha ya Kiswahili ni **muhimu** sana. Kiswahili kinazungumzwa Afrika ya Mashariki.

10. Wanafunzi **wavivu** hawafaulu katika masomo yao. Wao hawapendi kufanya kazi.

## C. Sarufi

### Tungo yakinishi na tungo kanushi

Soma sentensi zifuatazo, kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. a) **Mimi nina**soma kitabu cha Kiswahili.

   b) **Mimi si**som**i kitabu** cha Kiingereza.

2. a) **Wewe una**andika ubaoni. **Wewe hu**andik**i** daftarini.

   b) Kayitesi anaingia darasani. **Yeye ha**ingi**i** kanisani.

3. a) **Mimi na Kayitare tuna**cheza **kabumbu.**

   b) **Sisi hatu**chez**i** karata.

4. a) **Wewe na Mutesi mna**penda kuimba.

   b) **Nyinyi hampendi** kucheza.

5. a) **Kalisa na Mugabe wana**fagia darasani.

b) Wao **hawa**futi ubao.

## Zoezi la sarufi

1. Je, mimi ninasoma kitabu cha Kiingereza? Hapana, mimi ______________.
2. Je, mimi ninasoma kitabu cha Kiswahili? Ndiyo, mimi ______________.
3. Je, wewe unaandika daftarini? Hapana, wewe ______________. Wewe ______________.
4. Je, Kayitesi anaingia kanisani? Hapana, yeye ______________. Yeye ______________.
5. Je, mimi na Kayitare tunacheza kandanda? Ndiyo, sisi ______________.
6. Je, mimi na Kayitare tunacheza karata? Hapana, sisi ______________.
7. Je, wewe na Mutesi mnapenda kuimba? Ndiyo, nyinyi ______________.
8. Je, wewe na Mutesi mnapenda kucheza? Hapana, nyinyi ______________.
9. Je, Kalisa na Mugabe wanafuta ubao? Hapana, wao ______________.
10. Je, Kalisa na Mugabe wanafagia darasani? Ndiyo, wao ______________.

### Tafakari:

Katika majibu hapo juu, unaweza kukubaliana na tendo linaloelezwa katika kitenzi kwa kutumia **tungo yakinishi** (angalia sentensi zenye kutumia neno **ndiyo**). Unaweza pia kukana (kukanusha) tendo hilo kwa kutumia **tungo kanushi** (angalia sentensi zenye kutumia neno **hapana**).

### Kazi ya makundi

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, andika sentensi sita (tumia nafsi zote tatu katika umoja na wingi) katika tungo yakinishi, halafu ziandike pia katika tungo kanushi.

**Mfano:**

**Umoja:**

| Tungo yakinishi | Tungo kanushi |
|---|---|
| 1. Mimi ninapenda kucheza kandanda. | Mimi sipendi kucheza kandanda. |
| 2. Wewe unapenda kucheza kandanda. | Wewe hupendi kucheza kandanda. |
| 3. Yeye anapenda kucheza kandanda. | Yeye hapendi kucheza kandanda. |

**Wingi:**

| Tungo yakinishi | Tungo kanushi |
|---|---|
| 1. Sisi tunapenda kucheza kandanda. | Sisi hatupendi kucheza kandanda. |
| 2. Nyinyi mnapenda kucheza kandanda. | Nyinyi hampendi kucheza kandanda. |
| 3. Wao wanapenda kucheza kandanda. | Wao hawapendi kucheza kandanda. |

### *Zoezi la 1*

**Andika sentensi hizi katika tungo yakinishi au kanushi.**

1. Yeye anaimba vizuri.
2. Yeye hazungumzi Kiswahili sanifu.
3. Mimi ninapenda somo la Kiingereza.
4. Sisi tunapuuza masomo haya.
5. Mimi situngi sentensi.
6. Wao wanashika madaftari.
7. Nyinyi hamjitambulishi mbele ya wanafunzi wengine.
8. Wewe unaazima kitabu.
9. Wao hawachoti maji.
10. Nyinyi mtaenda mjini Kigali.

### *Zoezi la 2*

**Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia kitenzi sahihi katika wakati uliopo, tungo yakinishi na tungo kanushi.**

**Mfano:** Wewe (kupanga) michezo ya wanafunzi (Tungo yakinishi)
**Jibu:** Wewe **unapanga** michezo ya wanafunzi.

1. Kalisa (kucheza) mpira. (Tungo kanushi)
2. Mimi na wewe (kuimba) vizuri. (Tungo yakinishi)
3. Sisi (kuingia) darasani. (Tungo kanushi)
4. Mama na baba (kulima) shamba. (Tungo kanushi)
5. Mimi (kufanya) mtihani. (Tungo yakinishi)
6. Wewe (kusikiliza) redio. (Tungo kanushi)
7. Kayitesi na wewe (kuigiza) mazungumzo mbele ya wanafunzi. (Tungo yakinishi)
8. Wewe na Aisha (kukimbia) haraka sana. (Tungo kanushi)
9. Wao (kuweza) kushinda vizuri. (Tungo kanushi)
10. Mutoni na Bwiza (kupenda) somo la Kiswahili. (Tungo yakinishi)

## D. Kusikiliza na kuzungumza

### *Zoezi la imla*

**Funga kitabu chako, kisha katika daftari lako, andika kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno utakayosomewa na mwalimu wako.**

### *Zoezi la makundi*

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, zungumzieni vitu vinavyosafishwa shuleni.**

## Faharasa

**Adhabu:** jambo analofanya mtu au kufanyiwa kutokana na kuvunja sheria au kanuni iliyowekwa, mateso anayopata mtu kutokana na makosa yake

**Adhibu:** tesa mtu kutokana na makosa yake, kumfanyia mtu jambo linalomuudhi kwa makosa aliyoyafanya

**Alama:** maksi za mwanafunzi baada ya kufanya zoezi au mtihani

**Bustani:** sehemu ya kupandia miti ya maua, matunda au mboga

**Bwalo:** chumba kikubwa kinachotumiwa kulia chakula hasa shuleni

**Bweni:** chumba kikubwa kinachotumiwa na wanafunzi kulalia

**Choo kidogo:** mkojo

**Choo kikubwa:** kinyesi; mavi

**Choo:** mahali pa kuenda haja, msala

**Elewa:** fahamu, kuwa na ufahamu wa jambo

**Fua:** safisha nguo kwa maji

**Fuata:** kuwa makini na kuelewa kile unachofundishwa, kuiga, kuja nyuma au baadaye, kuandama

**Fundi:** mtu mwenye ujuzi fulani, mtu anayefanya kazi za maarifa fulani kama vile seremala, mwashi, na kadhalika.

**Gorofa:** nyumba ndefu

**Gumu:** kitu kisicho rahisi, kitu kisichoeleweka

**Haribu:** fanya kitu kiwe katika hali mbaya, kuchafua, kuangamiza kitu

**Hodari:** mtu anayeweza kufanya kitu kinachowashinda watu wengine

**Jaribio:** tendo linalofanywa ili kuona kama jambo limefanywa vizuri au kama jambo linafaa

**Jenga:** simamisha nyumba kwa kutumia miti, udongo, matofali, saruji na kadhalika

**Jibu:** itikia kwa maneno, maandishi au kwa ishara

**Jivunia:** furahia kuwa kitu chako ni bora

**Karo:** ada ya shule inayotolewa na mwanafunzi, pesa zinazolipwa shuleni

**Kelele:** sauti kubwa hasa isiyokuwa na maana yoyote, ghasia, fujo, ugomvi

**Kiranja:** kiongozi wa darasa

**Kumbuka:** kuwa tena na fikira ya jambo lililofanywa, lililopita au lililotokea

**Maktaba:** nyumba yenye mkusanyiko wa vitabu vingi

**Mbaya:** kitu kisichopendeza, kitu chenye hitilafu, kinyume cha 'nzuri'

**Mchafu:** kitu chenye uchafu, kinyume cha 'safi'

**Mfuasi:** mtu mwenye kupenda sana jambo fulani

**Mkubwa:** kitu chenye umbo linalopita kiasi au linalopita umbo la kawaida, kilichokwisha kua, kinyume cha 'mdogo'

**Mkuu wa shule:** kiongozi mkuu wa shule

**Mkutano:** mkusanyiko wa watu wengi kwa ajili ya kuzungumzia jambo maalumu, kusikilizana au kujadiliana

**Mlango:** nafasi au uwazi wa kuingilia na kutokea nyumbani

**Mtihani:** mpango unaowezesha kufahamu uwezo au ujuzi wa mtu

**Muhimu:** kitu chenye maana, kitu chenye matumizi makubwa, kitu kinachohitajika sana

**Mvivu:** mtu asiyependa kazi, mwenye tabia ya ulegevu wa kutenda jambo

**Mwerevu:** mwenye akili timamu, mtu asiye mjinga, mjuzi wa

mambo mengi

**Ndugu:** watu waliozaliwa tumbo moja, baba na mama mmoja, au baba mmoja au mama mmoja

**Nidhamu:** adabu

**Nyesha:** anguka kwa matone ya maji yanayotoka mawinguni (mvua inanyesha)

**Onyesha:** fanya kitu kionekane, kusababisha kitu kionekane

**Panga:** weka vitu kwa utaratibu mzuri

**Pendeza:** vutia kwa uzuri

**Piga magoti:** weka magoti chini wakati wa kusali au kuomba Mungu; salimu amri

**Ratiba:** mpango wa masomo yanayofundishwa katika wiki moja

**Refu:** chenye kipimo kilichozidi kitu kingine kutoka chini kuenda juu, kutoka upande mmoja hadi mwingine, kinyume cha fupi

**Safi:** kitu kisicho na uchafu, kisicho na taka

**Sahihi:** kitu kisichokuwa na makosa, kitu kilicho sawasawa

**Shauri:** kuambia mtu afanye jambo lililo zuri, kutoa maoni au nasaha ili mtu aweze kuwa na adabu, kuelekeza mtu ili afanye vizuri, kunasihi, kuonya

**Shinda:** kuwa wa kwanza, kupata alama ya kutosha

**Takataka:** vitu vibovu, vitu vilivyotupwa, vitu visivyohitajika, vitu vinavyokaa bila mpango na ambavyo havifai kwa matumizi

**Tunza:** weka kitu mahali penye usalama, kuhifadhi, kuweka kitu chini ya uangalizi ili kisiharibiwe

**Ubao:** kitu kilichotengenezwa na kuwekwa kwenye ukuta ili kitumike kuandikiwa kwa chaki

**Usafi:** tabia ya kutokuwa na uchafu

**Vaa sare:** vaa kwa namna moja inayofanana, vaa sawasawa

**Zoezi:** tendo la kupima ujuzi wa mtu

**Zuri:** kitu chenye kupendeza, kitu kisicho na hitilafu

## Mada Kuu:
# Matumizi ya Lugha Katika Mazingira Mbalimbali

## Mada Ndogo:
# Msamiati Katika Mazingira ya Nyumbani


| | |
|---|---|
| **Somo la Kwanza:** | Aina za nyumba, watu wanaoishi humo na ujenzi wake |
| **Somo la Pili:** | Vifaa mbalimbali vinavyopatikana nyumbani |
| **Somo la Tatu:** | Mifugo wanaofugwa nyumbani na vivumishi vya ngeli ya A – WA. |
| **Somo la Nne:** | Majina yanayohusishwa na watu na uhusiano wao kijamii pamoja na vivumishi vya ngeli ya A-WA |
| **Somo la Tano:** | Uhusiano wa kifamilia pamoja na vivumishi vya ngeli ya A-WA |

## Somo la Kwanza:

# Aina za Nyumba, Watu Wanaoishi Humo na Ujenzi Wake

## A. Michoro na mazungumzo kuhusu aina za nyumba na watu wanaoishi humo

Tazama michoro ifuatayo kwa makini kisha utoe maelezo yako kwa wenzako kuhusu unachokiona.




### Tathmini

Makao ni mahali wanakoishi watu. Makao ni muhimu kwa mwanadamu. Hueleza utamaduni wa watu, shughuli zao za kiuchumi na mazingira yao.

Kwa kutumia sentensi fupifupi, eleza unachokiona.

**Mifano:** 1. Mimi ninaona nyumba ya…

2. Mimi ninaona baba, …

**Soma mazungumzo yafuatayo baina ya baba na mama nyumbani.**

**Baba:** Habari ya kuamka mke wangu?

**Mama:** Njema mume wangu.

**Baba:** Naona nyasi zimepungua kwenye nyumba yetu.

**Mama:** Kweli. Tunafaa tutoke kwenye huu msonge tujenge nyumba ya mabati au mawe.

**Baba:** Kweli. Kama tutapata pesa tutajenga nyumba ya matofali na vigae.

**Mama:** Watoto wetu watafurahi sana.

**Baba:** Ndiyo. Hata nyanya na babu yao watafurahia.

**Mama:** Nitawaalika watoto wa shangazi yao. Pia binamu wao nitawaalika.

**Baba:** Nampenda jirani yetu. Amejenga kasri kubwa.

**Mama:** Tunampongeza kwa bidii. Kasri lake lina vyumba vingi.

**Baba:** Umemkama ng'ombe?

**Mama:** La hasha! Nimeanza na mbuzi.

**Baba:** Basi acha niwafungulie kuku, paka, kondoo na bata.

**Mama:** Na pia ukumbuke kumfungia mbwa.

*(Wanaendelea na shughuli zao mbalimbali)*

**Tathmini**

Je, nyumba zilizotajwa katika mazungumzo yaliyo hapo juu hujengwa kwa vifaa gani?

*Zoezi la ufahamu*

Kwa kujitegemea, soma tena mazungumzo baina ya baba na mama kimyakimya. Kisha kwa ushirikiano na wenzako, jibu kwa usahihi maswali yanayofuata.

1. ____________ za kuamka mke wangu?
2. Baba pia angemwamkia mama vipi? ____________.
3. Mama aliitikia salamu za baba kwa kusema ____________.
4. Mama alitaka watoke kwenye ____________ na kujenga nyumba ya ____________ na ____________.
5. ____________ wetu watafurahi sana.
6. Wazazi wa baba na mama tunawaitaje? ____________ na ____________.
7. Ninampenda ____________ yetu.
8. Acha niwafungulie __________, ___________, __________ na ___________.
9. Na umfungie ____________.
10. Kichwa mwafaka kwa mazungumzo haya ni: ____________.


    a) Mazungumzo baina ya baba na mama


    b) Mazungumzo baina ya mama na watoto

## B. Msamiati wa nyumbani

**Kwa ushirikiano na wenzako, taja msamiati wote wa nyumbani uliosoma katika mazungumzo baina ya baba na mama. Tumia tathmini ifuatayo.**

1. Aina ngapi za nyumba zimetajwa?
2. Nyumba hizo zimejengwa kwa kutumia nini?
3. Je, ni watu wangapi wanaopatikana nyumbani?
4. Ni mifugo gani wa nyumbani wametajwa?





## Kazi ya makundi

Jipange katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili. Elezaneni kama mnawajua wanyama, ndege na vifaa ama sehemu za nyumba zilizotajwa katika mazungumzo yaliyo hapo juu. Pia elezaneni faida na hasara za wanyama waliotajwa.

## Maelezo muhimu

Wanyama ni muhimu kwa binadamu. Wanatupa maziwa, nyama, mayai, ngozi, ulinzi, urafiki, mali na utajiri. Wengine wanatupa mbolea.

Wanyama na ndege wanaotunzwa na binadamu nyumbani huitwa mifugo.

### *Zoezi la msamiati wa nyumbani*

**Fanya zoezi hili katika daftari lako.**

1. Unawajua wanyama wanaofugwa nyumbani? Wataje wanyama wanne kwa kuwaandika kwenye daftari lako.

2. Hawa ni wanyama ama ndege?

a) Bata

b) Kuku

c) Njiwa

d) Ngamia

3. _____________ hutupa ulinzi usiku nyumbani.

4. Anatupa maziwa, nyama na ngozi. Yeye ni _____________.

5. Anayetaga mayai na kuangua ni _____________.

6. Naona _____________ imepungua kwenye nyumba yetu.

7. Tutoke kwenye huu _____________ tujenge nyumba ya _____________ na _____________

8. Umekama _____________?

***Zoezi la ziada***

Linganisha maelezo na mchoro kwa kutazama na kusoma sentensi ulizopewa baada ya mchoro. Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, mmoja asome sentensi na mwingine aonyeshe mchoro unaolingana nayo.



1.



2.



3.



4.

1. Mama anamkama ng'ombe.
2. Kasri la jirani lina paa la vigae.
3. Mbwa anabweka uwanjani.
4. Baba anafinyanga vyungu.

### *Zoezi la 1*

**Tunga sentensi katika umoja kuonyesha kuwa unaelewa maana ya msamiati ufuatao uliotumika katika mazungumzo baina ya baba na mama.**

*Baba, mama, jirani, nyasi, vigae, mabati, matope, mbwa, kuku, msonge*

**Mfano:** Binamu – mtoto wa ami, yaani ndugu wa baba

Matumizi katika sentensi: Binamu yangu ataalikwa kwetu.

### *Zoezi la mjadala*

**Jadiliana na wenzako kuhusu namna nyumba mbalimbali hujengwa:**

a) Taja vifaa vinavyotumika

b) Wajenzi wa aina mbalimbali za nyumba

c) Muda unaohitajika kukamilisha ujenzi

d) Faida za aina mbalimbali za nyumba


### Kazi ya makundi: Mjadala

Linganisha nyumba za jadi na za kisasa. Toeni maoni na maelezo yenu huru kuonyesha mnayoyafahamu kuhusu nyumba hizo.

## C. Sarufi

### Umoja na wingi katika ngeli ya A–Wa

Tazama michoro ifuatayo kwa makini, kisha uwaeleze wenzako ulichogundua.



1. Kuku (mmoja) - Kuku (wengi)
2. Bata (mmoja) - Mabata (watatu)
3. Ng'ombe (mmoja) - Ng'ombe (watatu)

### Maelezo muhimu

Ngeli ya A–Wa ni ngeli ya viumbe hai kama binadamu, ndege na wanyama. Katika umoja, kiambishi cha kitenzi ambacho hutumika ni '***a***' na katika wingi kiambishi ambacho hutumika ni '***wa***'.

### Mifano katika sentensi

| | | |
|---|---|---|
| 1. Kuku anaatamia mayai. | - | Kuku wanaatamia mayai. |
| 2. Bata anakunywa maji. | - | Mabata wanakunywa maji. |
| 3. Mzazi anajenga nyumba. | - | Wazazi wanajenga nyumba. |
| 4. Mbwa anabweka. | - | Mbwa wanabweka. |
| 5. Baba anafyeka nyasi. | - | Kina baba wanafyeka nyasi. |
| 6. Mama anamlisha ng'ombe. | - | Kina mama wanawalisha ng'ombe. |
| 7. Nyanya anafua nguo. | - | Kina nyanya wanafua nguo. |
| 8. Binamu anafagia nyumba. | - | Kina binamu wanafagia nyumba. |
| 9. Shangazi anapiga deki. | - | Kina shangazi wanapiga deki. |
| 10. Punda anabeba mzigo. | - | Punda wanabeba mizigo. |

*Zoezi la 1*

**Kwa vikundi vya wanafunzi wawili wawili, funga kitabu cha mwenzio kisha mwulize akupe umoja ama wingi wa sentensi zilizo hapo juu.**

*Zoezi la 2*

**Watungie wenzako sentensi kwa umoja na wingi kwa kutumia ngeli ya A–WA. Tumia majina ya watu pamoja na wanyama wanaopatikana nyumbani.**

## D. Matamshi na tahajia bora

Kwa ushirikiano na mwenzako, someni kwa zamu na kwa sauti maneno yafuatayo. Zingatieni matamshi sahihi ya maneno hayo.


| | | | |
|---|---|---|---|
| a) Mlango | b) Dirisha | ch) Dari | d) Paa |
| e) Chumba | f) Ng'ombe | g) Maziwa | h) Kuku |
| i) Nyumba | j) Bibi | k) Dada | l) Kaka |
| m) Mama | n) Baba | | |


Somo la Pili

# Vifaa Mbalimbali Vinavyopatikana Nyumbani

## A. Vifaa vya nyumbani

Tazama michoro ifuatayo kwa makini kisha uwaeleze wenzako vitu unavyoviona.




**Je, unafahamu kazi au manufaa ya vifaa hivi?**

**Tathmini**

1. Michoro inazungumzia nini?
2. Unaweza kuvitambua vifaa vinavyoonyeshwa kwenye michoro?
3. Kwa maoni yako, vifaa hivyo huwa na kazi gani? Waeleze wenzako.

Baada ya kutoa maoni yako binafsi, wewe na wenzako imbeni wimbo ufuatao wa vifaa vya nyumbani.

**Wimbo**

*Mimi ni stuli, watu hunikalia*

*Mimi ni mwiko, mama hunipikia*

*Mimi ni mto, nyote hunilalia*

*Mimi ni dari, sakafu ya juu ya nyumba*

*Mimi ni mlango, nafungwa ili kulinda wanaoingia*

*Mimi ni dirisha, hewa safi kuleta*

*Mimi ni kijiko, kupakua chakula*

*Mimi ni sebule, wageni kukaribisha*

*Mimi ni chumba cha malazi, mwenye nyumba njoo*

*Mimi ni veranda, keti hapo nje*

*Mimi ni kochi, kukalia ama kuketia*

*Mimi ni karai, ukitaka kuoga*

*Mimi ni paa, nakaa juu ya nyumba*

*Mimi ni sahani, chakula kulia hapo*

*Kikombe cha kunywa chai*

*Kitanda kulalia*

*Kabati kuweka vitu*

*Uma kumegea chakula*

*Runinga kupata habari*

*Redio dada ya runinga*

*Zulia kupamba nyumba*

*Vitambaa kurembesha nyumba*

*Nyumba ina mengi.*

### *Zoezi la ufahamu*

Soma kimyakimya wimbo wa vifaa vya nyumbani kisha ujibu maswali haya ya ufahamu.

1. Kazi ya dirisha ni ____________ hewa safi ndani ya nyumba. (kuleta, kutoa)
2. Kifaa kinachotumiwa kulala juu yake ni ____________. (kitanda, chumba cha malazi)
3. Ukitaka kuoga unatumia ____________. (karai, kikombe)
4. Veranda inapatikana ____________ ya nyumba. (ndani, nje)
5. Huonyesha picha na kutoa taarifa. Hicho ni kitu gani? _________ (redio, runinga)
6. Mimi ni ____________, watu hulalia ama kuketia. (meza, kochi)
7. ____________ hutumika jikoni. (Mwiko, Kochi)
8. Chumba cha malazi ni ____________. (sebule, chumba cha kulala)
9. Zulia hupatikana ____________. (sebuleni, nje ya nyumba)
10. ____________ hutumika kulia chakula. (Kijiko, Kiti)

### *Zoezi*

1. Kwa usaidizi wa wenzako, orodhesha vifaa vyote vya nyumbani vilivyozungumziwa katika wimbo.
2. Tambua majina ya vitu vilivyorejelea sehemu za nyumba.

## B. Mjadala kuhusu dhima ya vifaa vya nyumbani

### Mazungumzo na wenzako

Kwa ushirikiano na wenzako, zungumzia dhima (kazi na faida) ya vifaa vya nyumbani. Zingatia vifaa kama vile runinga, redio, kochi na sebule. Pia rejelea vyombo kama vile sahani, kikombe, uma, sufuria, kijiko, na kadhalika. Vilevile zungumzia sehemu za nyumba kama vile ukuta, dari, sakafu, sebule, mlango, dirisha, na kadhalika.

## C. Msamiati wa vifaa na sehemu za nyumba

**Kwa ushirikiano na wenzako, rejelea wimbo mlioimba. Sasa orodhesheni msamiati unaojitokeza kulingana na mwelekeo huu:**

a) Vifaa vinavyopatikana jikoni.

b) Vifaa vinavyopatikana sebuleni.

c) Sehemu za nyumba.

d) Vifaa vinavyopatikana katika vyumba vya kulala.

### *Zoezi la 1*

**Andika majibu sahihi kwa maelezo haya. Tumia msamiati kulingana na majibu ya *a)* hadi *d)* hapo juu.**

1. Vifaa vinavyopatikana jikoni pekee.
2. Vifaa viwili vinavyopatikana katika chumba cha kulala.
3. Vifaa vinavyopatikana sebuleni pekee.
4. Ni kama sanduku la kuweka vyombo ama nguo.
5. Kinaonyesha picha na kutangaza habari.
6. Ni sehemu ya juu ya nyumba.
7. Tunafungua ili wageni waingie ndani.
8. Hupitisha hewa safi ndani ya nyumba, na sio mlango.
9. Tunaweza kulalia na pia kuketi hapo.
10. Kinatumika kama vidole vya mkono kumega chakula.

*Zoezi la 2*

**Kwa kujitegemea, kamilisha sentensi zifuatazo. Andika majibu katika daftari lako.**

1. Mimi ni ____________, watu hunikalia.
2. Mimi ni ____________, kazi yangu ni kupakulia chakula.
3. Mimi hutumiwa kupamba nyumba ____________.
4. Hutumiwa kunywea chai ____________.
5. Hutumiwa ukitaka kuoga ____________.
6. Mimi ni ____________ , kazi yangu ni kukaribisha wageni.
7. ____________ni dada ya runinga.
8. Tunalala kwenye ____________.
9. Mimi ni ____________ nakaa juu ya nyumba.

## D. Sarufi

### Umoja na wingi wa majina katika ngeli ya A-WA

### Sentensi zinazotumia majina ya mifugo

**Soma sentensi zifuatazo kwa makini.**

1. Ng'ombe anakamuliwa. - Ng'ombe wanakamuliwa.
2. Punda anavuta gari. - Punda wanavuta magari.
3. Kuku anataga yai. - Kuku wanataga mayai.
4. Mbwa anabweka. - Mbwa wanabweka.
5. Bata anaogelea. - Mabata wanaogelea.
6. Mbuzi anakula nyasi. - Mbuzi wanakula nyasi.
7. Kondoo ananyonyesha. - Kondoo wananyonyesha.

8. Paka analala. - Paka wanalala.

9. Ngamia anabeba mtu. - Ngamia wanabeba watu.

10. Njiwa anapaa angani. - Njiwa wanapaa angani.

### *Zoezi la 1*

**1. Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, tunga sentensi zenye majina ya mifugo mbalimbali katika umoja naye mwenzako aiandike katika wingi.**

**Mfano:**

Wewe: Kuku anataga yai.

Yeye: Kuku wanataga mayai.

**2. Tumia msamiati ufuatao pamoja na ngeli ya A–WA kutunga sentensi sanifu za Kiswahili.**

Punda, ng'ombe, mbuzi, paka, mbwa

### *Zoezi la 2*

**Andika sentensi hizi ndani ya daftari lako katika umoja bila kushirikiana na wenzako.**

**Mfano:** Mbwa waliwauma watu.

**Jibu:** Mbwa alimuuma mtu.

1. Paka watawala panya.
2. Punda walivuta magari.
3. Ng'ombe wanakula nyasi.
4. Kuku wanataga mayai.
5. Bata wanaogelea.
6. Mbuzi wanalala.
7. Kondoo wanapiga kelele.

8. Ngamia walisafirisha watu.
9. Njiwa wanapaa angani.
10. Batamzinga wanaatamia mayai.

## E. Tahajia na matamshi bora

### 1. Soma maneno yafuatayo kwa kuzingatia matamshi bora.

a) Ngamia

b) Ng'ombe

c) Mbuzi

d) Kondoo

e) Mbwa

### 2. Soma sentensi zifuatazo kwa usahihi.

a) Baba anakama ng'ombe.

b) Mama anamfunga punda.

c) Kaka anamlisha ndama.

d) Dada anamchinja kuku.

e) Babu anamtibu ngamia.

***Zoezi la imla***

Msikilize mwenzako vyema akusomee maneno (atakayopewa na mwalimu) kisha uyaandike kwa hati nzuri na maendelezo sahihi.

***Zoezi la ziada***

**Mazungumzo/mjadala**

Jadiliana na mwenzako kuhusu faida na hasara za wanyama wa kufugwa.

# Mifugo Wanaopatikana Nyumbani na Vivumishi vya Ngeli ya A–WA

## A. Michoro ya mifugo mbalimbali

**Tazama michoro ifuatayo kisha uwataje wanyama unaowaona katika umoja na wingi.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
|  |  |
|  |  |
|  |  |
|  |   |

**Soma sentensi zifuatazo katika umoja na wingi.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Ngamia mkubwa anakuja. | 1. Ngamia wakubwa wanakuja. |
| 2. Mbwa mkali anabweka. | 2. Mbwa wakali wanabweka. |
| 3. Kondoo mchanga amelala. | 3. Kondoo wachanga wamelala. |

| | |
|---|---|
| 4. Paka mjanja anashika panya. | 4. Paka wajanja wanashika panya. |

*Zoezi la kusikiliza na kuzungumza*

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni sentensi 1–4 zilizo hapo juu (katika umoja na wingi) kwa sauti na kwa zamu. Mwambie mwenzako maneno yaliyopigwa mistari ni ya aina gani? Sasa yatamke bila kutamka sentensi nzima. Zingatia matamshi mema ya kila neno.**

*Zoezi*

Wabainishie wenzako matumizi ama maana ya maneno yaliyopigiwa mstari. Tumia sentensi fupi fupi na uzingatie ngeli ya A–WA.

## B. Msamiati kuhusu mifugo na vivumishi vya ngeli ya A-WA

Soma kifungu kifuatacho kuhusu wanyama wa kufugwa na vivumishi vya ngeli ya A–WA.

Huyu ni baba na mama. Wao ni wafugaji. Wana ng'ombe wanne. Ng'ombe wao ni wanono. Pia wana punda. Punda ni mkubwa. Ngamia wao ni mkubwa na mrefu. Anabeba mizigo mingi. Baba ana mbwa mkali. Mbwa mwenyewe ni mwembamba. Mbuzi wao ni mmoja. Yeye ni mchanga. Mama anapenda paka. Paka huyo ni mdogo. Hajui kuwinda panya. Tena wana njiwa. Njiwa wao ni mweupe pepepe!

*Zoezi la ufahamu*

**Soma tena kifungu kilicho chini ya mada ya 'Msamiati'. Katika daftari lako, andika maneno yanayofaa kujaza nafasi wazi katika sentensi hizi. Shirikiana na wenzako pale unapopata matatizo.**

1. Taarifa yenyewe ni juu ya ____________ na ____________ ambao ni watu.
2. Baba na mama wana ____________ wanne.
3. Ng'ombe wao ni ____________.
4. Pia wana ____________.

5. Punda wao ni ___________.

6. ___________ ni mrefu.

7. Baba ana mbwa ___________.

8. Mbwa mwenyewe ni ___________.

9. Mbuzi wao ni ___________.

10. ___________ ni mchanga.

***Kazi ya makundi***

**Kwa ushirikiano na mwenzako, tumia kamusi kueleza maana ya maneno mtakayosomewa na mwalimu kisha myatungie sentensi.**

***Zoezi***

**Tunga sentensi zako mwenyewe kwa kutumia maneno haya:**

mdogo, mnono, mweusi, mweupe, mmoja, mkali, mchanga, mkubwa, wanne, mrefu

## C. Sarufi

### Ngeli ya A–WA na vivumishi vimilikishi

Soma sentensi zifuatazo kwa makini. Sasa waeleze wenzako unachoelewa kuhusu maneno yaliyopigwa mstari.

1. Bibi <u>yake</u> amepona. - Kina bibi <u>zao</u> wamepona.
2. Dada <u>yako</u> atakuja. - Kina dada <u>zenu</u> watakuja.
3. Baba <u>yangu</u> ni mkulima. - Kina baba <u>zetu</u> ni wakulima.
4. Mama <u>yake</u> anapika. - Kina mama <u>zao</u> wanapika.
5. Babu <u>yako</u> ametuzwa. - Kina babu <u>zenu</u> wametuzwa.
6. Nyanya <u>yangu</u> anaimba. - Kina nyanya <u>zetu</u> wanaimba.

### Maelezo muhimu

Vivumishi ni maneno yanayotumika kusifu mtu au kitu. Kumiliki ni kuwa mwenye kitu. **Kivumishi kimilikishi** ni kivumishi kinachoonyesha kuwa sifa ni ya mtu fulani au kitu fulani. Maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi zilizo hapo juu ndiyo vivumishi vimilikishi.

### Mifano zaidi ya vivumishi vimilikishi:

- Mwiko wangu umevunjika.
- Ng'ombe wenu amekunywa maji.
- Nyumba yake imejengwa.
- Sebuleni mwangu mna maua.
- Kitanda changu kina godoro jipya.
- Kikombe chake kimejengwa.
- Stuli yake imeuzwa.

### *Zoezi la 1*

**Tunga sentensi kwa kushirikiana na wenzako kudhihirisha uhusiano wa kifamilia na vivumishi vimilikishi.**

**Mfano:**

a) Kaka yangu ni mkubwa.

b) Nyanya yake ni mrefu.

### *Zoezi la 2*

Tumia vimilikishi vifuatavyo kutunga sentensi katika ngeli ya A–WA na majina ya uhusiano wa kifamilia.

yangu, yako, yake, yetu, yenu, yao

**Zoezi la 3**

Tungeni sentensi kumi sahihi kwa kutumia nomino za vifaa vya nyumbani na vivumishi vimilikishi katika ngeli ya A–WA.

**Mfano:** Kisu chako ni butu.

## D. Tahajia na matamshi bora

1. **Kwa ushirikiano na wenzako, someni sentensi zifuatazo kwa sauti. Zingatieni matamshi sahihi.**

   a) Kisu changu ni kikali.

   b) Kochi langu ni kubwa.

   ch) Paa la nyumba yake ni bovu.

   d) Kijiko chako kimepotea.

   e) Mwiko wake uko hapa.

   f) Sebule yangu ni safi.

   g) Meza yako ni kubwa.

   h) Runinga yake iko wapi?

   i) Redio yangu inatangaza.

   j) Kaka yangu anakuja.

   k) Dada yake anaenda.

   l) Kikombe chake ni kipya.

2. **Kwa kujitegemea, andika sentensi hizi kwa hati nzuri katika daftari lako.**

   a) Baba yangu anafyeka nyasi.

   b) Bata wangu anaogelea majini.

   ch) Kuku wao anataga mayai.

d) Kaka yake ananunua shati.

e) Nyanya yako anapika wali.

**NI VIZURI KWA FAMILIA KUISHI KWA AMANI**

# Majina Yanayohusishwa na Watu na Uhusiano Wao Kijamii Pamoja na Vivumishi

## Michoro na sentensi zenye vivumishi vionyeshi na viulizi

Tazama michoro ifuatayo kwa makini. Zungumza na wenzako kuhusu michoro na maneno yaliyokolezwa rangi katika sentensi zilizo hapo chini.

| | |
|---|---|
| **1.**  Kuku | **2.**  Chupa |
| **3.**  Sahani | **4.**  Kalamu |

1. Kuku **yupi** atachinjwa? - Kuku **wepi**_watachinjwa?
2. Chupa **hii** ina dawa. - Chupa **hizi** zina dawa.
3. Sahani **gani** itatumika? - Sahani **gani** zitatumika?
4. Kalamu **ipi** itanunuliwa?- Kalamu **zipi** zitanunuliwa?

## A. Mazungumzo

**Soma mazungumzo yafuatayo baina ya kaka na dada.**

**Dada:** Hujambo kaka?

**Kaka:** Sijambo dada. U hali gani?

**Dada:** Njema. Kiti chako kimevunjika?

**Kaka:** Ndiyo. Niliona ule mto wako nje.

**Dada:** Ule haukuwa wangu. Shemeji yetu anakuja leo.

**Kaka:** Amekaribishwa. Sebule yetu imepangwa? Hii nyumba inataka kufagiliwa.

**Dada:** Nitaipiga deki. Wewe mwangalie huyo mbuzi asikate kamba.

**Kaka:** Vyema. Mlango ule unahitaji kusafishwa pia.

**Dada:** Kweli. Hata lile dirisha. Basi wewe mfunge huyu mbwa.

**Kaka:** Mbwa yupi? Ama huyu Tom?

**Dada:** Enhe!

*(Wanaondoka)*

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena kwa sauti halafu kimyakimya mazungumzo baina ya dada na kaka. Baada ya kusoma, jibu maswali haya ya ufahamu kwa kushirikiana na wenzako. Andika majibu katika daftari lako.**

1. ____________ ndiye aliulizwa kama kiti chake kilikuwa kimevunjika.
2. Niliona ____________ mto wako nje.
3. ____________ imepangwa?

4. Wewe mwangalie ____________ mbuzi asikate kamba.
5. Mlango ____________ unatakiwa kusafishwa pia.
6. Mbwa ____________ anastahili kufungwa?
7. Nitapiga nyumba ____________.
8. Ama ____________ ndiye anayestahili kufungwa?
9. Dirisha ____________ linastahili kusafishwa.
10. U hali ____________ dada?

***Zoezi la kuigiza***

Igizeni mazungumzo baina ya dada na kaka kwa kushirikiana katika kundi la wanafunzi wawili wawili.

### Maigizo ya mazungumzo

Igiza tena mazungumzo hayo baina ya kaka na dada kwa sauti. Zingatia matamshi bora na maana ya maneno yaliyotumika. Tumia kamusi ya Kiswahili sanifu kupata maana.

## B. Msamiati wa vifaa vya nyumbani

***Zoezi***

**Rejelea mifano ya sentensi zifuatazo. Sasa tungeni sentensi zenu binafsi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.**

1. Kiti hiki chako kimevunjika.
2. Ule mto wake uko nje?
3. Sebule hii yetu imepangwa vizuri?
4. Nyumba hii inataka kufagiliwa.
5. Wewe mwangalie mbuzi huyo.
6. Mlango ule unataka kusafishwa.

7. Funga dirisha lile.

8. Wewe mfunge mbwa huyu.


9. Paka yupi amekula?

10. Ni chumba gani unachokitaja?

## C. Sarufi

### Ngeli ya A–WA na vivumishi vya kuulizia na kuonyesha

Tazama michoro ifuatayo kwa makini. Je, unaweza kusema nini kuhusu michoro hiyo na maandishi yaliyopo chini yake?




| (a) | (b) |
|---|---|
| 1. Huyu mjomba wangu ni mpole. | Hawa wajomba wetu ni wapole. |
| **(c)** | **(d)** |
| 2. Sikio la binamu huyo halijapona. | Masikio ya mabinamu hao hayajapona. |

| (e) | (f) |
|---|---|
| 3. Kitabu cha dada yule ni kipya. | Vitabu vya kina dada wale ni vipya. |

## Maelezo muhimu

- Vivumishi vionyeshi huonyesha iwapo kitu kipo karibu, mbali kidogo ama mbali sana.

**Mfano:**

| Karibu | Mbali kidogo | Mbali sana |
|---|---|---|
| 1. Kiti hiki | Kiti hicho | Kiti kile |
| 2. Baba huyu | Baba huyo | Baba yule |
| 3. Mbuzi huyu | Mbuzi huyo | Mbuzi yule |
| 4. Dirisha hili | Dirisha hilo | Dirisha lile |
| 5. Nguo hizi | Nguo hizo | Nguo zile |

- Vivumishi viulizi huuliza maswali, kwa mfano:

| | |
|---|---|
| a) Mjukuu gani? | b) Paa lipi? |
| c) Mbuzi gani? | d) Runinga ipi? |
| e) Mtu gani? | f) Kaka yupi? |

### *Zoezi la 1*

**Kwa ushirikiano na wenzako, tungeni sentensi sahihi kwa umoja na wingi kwa kutumia sifa zifuatazo:**

a) huyu, huyo, yule

b) hiki, hicho, kile

c) humu, humo, mle

d) changu, chako, chake

e) mkubwa, mdogo, mweusi, mnene

### *Zoezi la 2*

**Soma sentensi zifuatazo. Katika vikundi vya wanafunzi watatu watatu, eleza maana ya maneno yaliyopigwa mstari.**

1. Mama yangu anafagia.
2. Mbuzi mnono amesimama.
3. Nyumba kubwa inajengwa.
4. Binamu huyo atakuja.
5. Hii ni sahani yake.
6. Sebuleni kuna kochi jipya.
7. Mlango ule haufunguki.
8. Babu yupi analisha ng'ombe?
9. Dada gani atapewa zawadi?

### *Zoezi la ziada*

**1. Kwa kujitegemea, tunga sentensi kwa kutumia nomino kumi za vifaa vinavyopatikana nyumbani.**

**2. Sahihisha sentensi zifuatazo:**

**Kwa mfano:** **Kijiko hiki ni kisafi.**

**Jibu:** **Kijiko hiki ni safi.**

a) Ng'ombe imezaa.

b) Kaka changu ni mkubwa.

c) Mbuzi hiki ni changu.

d) Mlango huu ni pana.

e) Nyumba mdogo imejengwa.

## D. Tahajia na matamshi bora

**Soma sentensi zifuatazo bila kusitasita kwa kuzingatia matamshi sahihi.**

1. Kaka yangu anafagia nyumba.
2. Mbwa yupi anabweka?
3. Meza yake imevunjika.
4. Bibi yako amekusalimu.
5. Helena na Juma ni ndugu zangu.
6. Kuku wake anataga mayai.
7. Punda mzuri anabeba mizigo.
8. Ngamia mkubwa atauzwa.
9. Nyanya yako anaitwa nani?
10. Kikombe kizuri kimelindwa.


*Somo la Tano*

# Uhusiano wa Kifamilia Pamoja na Vivumishi vya Ngeli ya A–WA

## A. Michoro ya watu katika jamii

Tazama michoro ifuatayo kisha utumie vivumishi vimilikishi ulivyojifunza katika ngeli ya A-WA kutunga sentensi sahihi. Kwa mfano:

Baba yangu ni mpole.

| | |
|---|---|
|  Baba **1.** |  Mama **2.** |
|  Dada **3.** |  Kaka **4.** |
|  Babu **5.** |  Nyanya **6.** |



Baba, mama na watoto

**7.**



Mjomba

**8.**



Shangazi

**9.**

## B. Kifungu kuhusu uhusiano wa kifamilia

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni kifungu kifuatacho kuhusu uhusiano wa kifamilia.**

Ngabo amemwoa Neza. Gasimba ni kaka mdogo wa Bw Ngabo na Mihigo ni kakake mkubwa. Bw Ngabo ana dada anayeitwa Mutesi. Watoto wa Bw Ngabo na Bi Neza ni Mutoni na Gahigi. Mutoni ni msichana na Gahigi ni mvulana. Bi Neza ana dada anayeitwa Uwase. Gahigi amemwoa Keza na wana binti anayeitwa Gatako. Gatako ameolewa na Mugisha. Mtoto wao ni Mugabo. Gasore ni kaka ya Uwase na Neza.

Ndugu wa kike huitwa dada. Mutoni ni dada yake Gahigi.

Ndugu wa kiume huitwa kaka. Gahigi ni kaka yake Mutoni.

Mtu aliyekuoa utamwita mume wako. Bw Ngabo ni mume wa Bi Neza.

Mtu uliyemwoa utamwita mke wako. Bi Neza ni mke wa Bw Ngabo.

Ndugu ya mke wako au ndugu ya mume wako utamwita shemeji. Gasimba na

Bi Neza wanaitana shemeji. Pia Mihigo na Bi Neza wataitana shemeji.

Kaka ya baba anaitwa baba mkubwa au baba mdogo. Gasimba ni baba mdogo wa Mutoni na Gahigi. Gasimba ni kaka ya baba yao (Bw Ngabo).

Mtoto wa mwanao anaitwa mjukuu. Gahigi ni mtoto wa Bi Neza na Mitaako ni mtoto wa Gahigi, hivyo Mitaako ni mjukuu wa Bi Neza.

**Majina mengine ya ukoo ni:**

Mtoto wa mjukuu anaitwa kitukuu.

Mtoto wa kitukuu anaitwa kilembwe.

Mtoto wa kilembwe anaitwa kilembwekeza.

Baba ya mume wako anaitwa baba mkwe.

Mama ya mke wako anaitwa mama mkwe.

Mama ya baba au mama anaitwa nyanya.

Baba ya mama au baba anaitwa babu.

Dada ya baba yako anaitwa shangazi.

***Zoezi la ufahamu***

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jadili majibu sahihi kwa maswali yanayofuata kisha myanakili katika madaftari yenu.**

1. Mama ya mama yangu anaitwa ______________________.
2. Ndugu wa kike wa baba yangu anaitwa ______________________.
3. Baba ya mume wangu anaitwa ______________________.
4. Mtoto wa mjukuu anaitwa ______________________.
5. Baba ya baba yangu anaitwa ______________________.

## C. Kusikiliza na kuzungumza

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni mifano ifuatayo kwa sauti na kwa matamshi sahihi. Jadili maana za maneno yaliyokolezwa rangi.**

1. **Baba** yangu amefika.
2. Mama yake amepika chakula.
3. Dada yako atakuja.
4. Kaka yangu ni mchezaji hodari.
5. Kina babu zetu ni matajiri.
6. Nyanya yake ni mgonjwa.
7. Familia yao ni ya watu sita.
8. Mjomba wangu anaandika.
9. Shangazi yako hajaondoka.

**Soma mazungumzo yafuatayo baina ya mzazi na mtoto kuhusu ugomvi na majirani.**

**Mzazi:** Habari Mutoni?

**Mtoto:** Nzuri baba.

**Mzazi:** Kwa nini unagombana na mtoto wa jirani?

**Mtoto:** *(Anasita)* Ni yeye alianza kunitusi.

**Mzazi:** Unajua matusi ni mabaya? Kwa nini unaleta chuki?

**Mtoto:** Pole baba. Nitazingatia amani.

**Mzazi:** Vyema. Usiyarudie makosa hayo.

**Mtoto:** Ndiyo baba.

**Mzazi:** Kaka yako yuko wapi?

**Mtoto:** Anachunga mbuzi na ng’ombe.

**Mzazi:** Sawa. Paka wangu yuko wapi?

**Mtoto:** *(Akitabasamu)* Huyo hapo.

### *Zoezi la kuigiza*

Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, igizeni mazungumzo baina ya mzazi na mtoto kuhusu kuleta amani katika familia.

### *Zoezi la utafiti*

Tambueni na kuorodhesha maneno yote mapya katika mazungumzo baina ya mzazi na mtoto. Jaribu kuyatamka kwa sauti sahihi kulingana na sauti za Kiswahili. Pia, shirikiana na wenzako kupata maana yake katika kamusi ya Kiswahili ama kwa kurejelea muktadha wa matumizi.

### *Zoezi la kusikiliza na kuzungumza*

Katika daftari lako, jaza mapengo katika sentensi hizi. Zingatia mazungumzo baina ya Mzazi na Mtoto.

1. Mazungumzo ni baina ya ____________ na ____________.
2. Mtoto anaitwa ____________.
3. Jibu la 'Habari' ni ____________.
4. Mutoni aligombana na mtoto wa ____________.
5. ____________ ni mabaya.
6. Kwa nini unaleta ____________?
7. ____________ baba.
8. Nitafanya ____________.
9. ____________ yako yuko wapi?
10. Anachunga ____________ na ____________.

### *Zoezi la mjadala*

Jadilianeni namna mnaweza kudumisha amani na upendo shuleni na nyumbani.

## D. Msamiati wa familia

**Soma mazungumzo baina ya mzazi na mtoto mara nyingine tena. Kwa kutumia maana ya maneno mapya mliyopata, tunga sentensi fupi fupi na sahihi. Tafiti zaidi kwenye kamusi ya Kiswahili iwapo bado hamna uhakika.**

***Zoezi la ubunifu***

**Someni kwa pamoja mifano ya sentensi zifuatazo kisha tungeni sentensi nyingine kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari.**

1. Kwa nini unagombana na jirani?
2. Matusi ni mabaya.
3. Pole baba.
4. Usirudie makosa.
5. Kaka yako yuko wapi?
6. Anachunga mbuzi na ng'ombe.
7. Huyo hapo!
8. Nitazingatia amani.
9. Kwa nini unaleta chuki?
10. Huyu ni paka wangu.

## E. Sarufi

**1. Tambua vivumishi vimilikishi katika sentensi hizi kwa kujitegemea.**

a) Bibi yetu ameketi sebuleni.

b) Paa la nyumba yangu ni bovu.

c) Mbuzi mnono ni wako.

d) Mbwa anayebweka ni wake.

e) Sufuria yenu ni safi.

### Maelezo muhimu

Kivumishi kimilikishi ni neno ambalo huonyesha mtu au kitu fulani ni cha nani au kinamilikiwa na nani. Hutumika pamoja na nafsi tatu zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili. Mifano ya vivumishi vimilikishi ni:

| | |
|---|---|
| -angu | -etu |
| 1. Mtoto wangu amefika. | Watoto wetu wamefika |
| 2. Mwalimu wangu ameondoka. | Walimu wetu wameondoka. |
| -ako | -enu |
| 3. Mbwa wako anabweka. | Mbwa wenu wanabweka. |
| 4. Kuku wako anataga mayai mengi. | Kuku wenu wanataga mayai mengi. |
| -ake | -ao |
| 5. Paka wake amelala. | Paka wao wamelala. |
| 6. Ng'ombe wake anakula nyasi. | Ng'ombe wao wanakula nyasi. |

**2. Kwa ushirikiano na wenzako, chagua sentensi sahihi pekee kati ya hizi.**

a) Kondoo imezaa leo.

b) Ngamia ulibeba mizigo.

c) Paka changu anakula panya.

d) Kochi langu ni zuri.

e) Babu yake anafanya kilimo.

f) Mama chake ni daktari.

g) Dada yako anacheza kandanda.

h) Tumia pesa hii vyema.

i) Jirani yako ni ndugu yangu.

j) Paka wangu amelala.

### Maelezo muhimu

Sentensi huwa sahihi kwa misingi ya usahihi wa upatanisho wa kisarufi wa ngeli mbalimbali.

**3. Ongeza kivumishi cha sifa mbele ya kila nomino. Sasa mwambie mwenzako akosoe jawabu lako kwa njia ya kushirikiana wawili wawili.**

**Mfano:** Sufuria nzuri

a) Kochi ____________
b) Mlango ____________
ch) Meza ____________
d) Shangazi ____________
e) Mjomba ____________
f) Kijiko ____________
g) Dirisha ____________
h) Dada ____________
i) Ami ____________
j) Binamu ____________

**4. Ongezea kiulizi kutegemea nomino kisha watajie wenzako jawabu lako. Tumia *gani* ama *yupi*.**

**Mfano:** Baba ____________?

**Jibu:** Baba yupi?

a) Sufuria ____________?
b) Mama ____________?
c) Kaka ____________?
d) Kikombe ____________?
e) Mbuzi ____________?

## F. Tahajia na matamshi bora

### *Zoezi la tahajia na matamshi bora*

**1. Tamka maneno yafuatayo kwa sauti sahihi ya Kiswahili kwa ushirikiano na wenzako.**

a) Sufuria
b) Kochi
c) Dirisha
d) Shangazi
e) Binamu
f) Ami

**2. Andika maneno yafuatayo kwa hati nzuri.**

a) Usirudie makosa.
b) Matusi ni mabaya.
c) Kaka yako yuko wapi?
d) Anachunga mbuzi na ng'ombe.
e) Mbuzi mnono ni wako.

## Faharasa

**Nyumba:** makao ya binadamu ya kukaa ndani

**Mgeni:** mtu anayetembelea mahali kwa mara ya kwanza; mwalikwa

**Chai:** kinywaji kinachotokana na majani ya mchai

**Ndugu:** neno la heshima la kumwita mtu wa kike au kiume; jamaa ya mtu

**Mabati:** aina ya madini ambayo hutengenezwa ili kuezekea paa la nyumba

**Paa:** sehemu ya juu ya nyumba (ndani)

**Msonge:** nyumba ya mviringo; imejengwa kwa miti, udongo na nyasi

**Ghorofa:** nyumba iliyojengwa juu ya nyingine

**Mawe:** umoja wa 'jiwe'; kipande cha mwamba ambacho ni kigumu

**Kasri:** jumba la mfalme

**Nyumba ya mawe:** makao ya binadamu yaliyotengenezwa kwa mawe katika kuta zake

**Babu:** baba yake mama au baba

**Nyanya:** mama yake mama au baba

**Mpwa:** mtoto wa kaka yangu

**Shangazi:** dada ya baba

**Ami:** kaka ya mama

**Dari:** sakafu ya juu ya nyumba

**Sakafu:** sehemu ya chini ya nyumba

**Ukuta:** sehemu mojawapo ya upande wa nyumba iliyojengwa wima

**Mlango:** nafasi ya kuingilia ndani ya nyumba

**Dirisha:** sehemu ndogo ya uwazi kwenye nyumba ya kuleta mwangaza ndani ya nyumba

**Mbu:** mdudu anayesababisha ugonjwa wa malaria

**Kunguni:** mdudu anayekaa vitandani na kunyonya damu

**Kiroboto:** mdudu anayeuma na anapenda vumbi

**Ugonjwa:** maradhi; ukosefu wa afya mwilini

**Vumbi:** ungaunga wa mchanga

**Ngeli:** kundi la majina (nomino) yanayofanana

**Jogoo:** kuku wa kiume

**Malaika:** kiumbe wa mbinguni (kidini)

**Shetani:** kiumbe wa mbinguni anayeaminika kudhuru binadamu

## Mada Kuu:
# Msamiati wa Mazingira Mbalimbali

## Mada Ndogo:
# Msamiati wa Mazingira ya Utawala

| | |
|---|---|
| **Somo la Kwanza:** | i) Nchi yangu |
| | ii) Dira ya Dunia |
| **Somo la Pili:** | Ofisi ya tarafa yangu |
| **Somo la Tatu:** | Utawala bora |

# Nchi Yangu

## A. Ramani ya nchi ya Rwanda

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tazameni ramani hii kisha mueleze mnachokiona.




**Soma kifungu cha habari kinachofuata kuhusu 'Nchi Yangu.'**

***(Munezero ni Mnyarwanda na anapenda sana nchi yake ya Rwanda.)***

Jina langu ni Munezero. Nchi yangu ni Rwanda. Rwanda ni mojawapo ya nchi za Bara la Afrika. Mimi ninapenda sana nchi yangu. Rwanda ina mikoa minne na mji wa Kigali. Kigali ni mji mkuu wa Rwanda. Mji wa Kigali una mitaa mbalimbali. Kuna mitaa ya biashara ndogo ndogo na mitaa ya biashara kubwa kubwa. Mimi ninaishi katika wilaya ya Kamonyi.

Rwanda imezungukwa na nchi nne. Sehemu ya kusini kuna nchi ya Burundi. Sehemu ya kaskazini kuna nchi ya Uganda. Sehemu ya mashariki kuna nchi

ya Tanzania na sehemu ya magharibi kuna nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Rais wa Rwanda na viongozi wengine wanapenda wananchi wote. Wao wanashirikiana na raia katika shughuli za kuendeleza nchi na kudumisha amani.

Nchini Rwanda kuna wabunge wanaosimamia raia wote na kuandaa sheria nzuri. Mawaziri wanaunda serikali ya Rwanda, wakuu wa mikoa wanaongoza vizuri mikoa yao. Wakuu wa wilaya na halmashauri zao wanashirikiana kuendeleza miradi ya wilaya zao. Wakuu wa tarafa na Halmashauri za Tarafa wanatoa mchango mkubwa katika shughuli za kimaendeleo za tarafa zao.

Wakuu wa kata na wakuu wa vijiji nao ni ngazi muhimu za uongozi bora nchini Rwanda. Mimi ninapenda wimbo wa taifa na bendera ya taifa langu. Viongozi wazuri wanashirikisha wananchi wao kupanga shughuli za kuendeleza nchi yangu; kujenga barabara nzuri, kujenga shule, kujenga vituo vya afya na hospitali, kupanda miti, kuchimba mifereji ya maji safi, na kadhalika. Mimi ninajivunia nchi yangu. Mimi ninapenda nchi yangu, Rwanda.

## B. Msamiati mpya kuhusu nchi ya Rwanda

Soma tena kifungu cha habari kilicho hapo juu kisha uandike msamiati ulio mpya kwako.

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni maana za msamiati huo. Tumia kamusi ya Kiswahili pale panapohitajika.**

**Kwa mfano:**

**Mkoa - jimbo la utawala; eneo la utawala lenye wilaya kadhaa**

*Zoezi la 1*

**Kwa kuzingatia mifano ya sentensi zilizotolewa hapa chini, jaribu kutunga sentensi moja moja kwa kutumia maneno yaliyotiwa rangi ya chungwa na kupigwa mstari.**

1. **Bara** la Afrika limeundwa na nchi nyingi. Kwa mfano: Rwanda, Burundi, Uganda, Tanzania, Namibia, Zimbabwe, na kadhalika.
2. **Rais** wa Rwanda anaongoza nchi ya Rwanda na anahimiza usawa wa kijinsia kwa Wanyarwanda wote.
3. **Wilaya** ya Musanze inawaelimisha wananchi wake namna ya kujikinga

dhidi ya ugonjwa wa malaria.

4. Mimi ni **mwananchi** wa Rwanda; wazazi wangu ni Wanyarwanda na ninaishi nchini Rwanda.
5. Baada ya miaka mitano Wanyarwanda hupiga kura na kujichagulia **wabunge** wao.
6. Ni vizuri kutoa **mchango** wako kwa kulipa ushuru ili kuendeleza nchi yako.
7. **Mtaa** wa biashara kubwa unapatikana katika tarafa ya Nyarugenge, mjini Kigali.
8. **Barabara** ya Kigali-Huye imetengenezwa vizuri sana.
9. **Hospitali** ya Kabgayi ina madaktari wengi. Wao wanatibu wagonjwa wote vizuri.
10. Ni muhimu kushiriki katika shughuli za **kimaendeleo**; kujenga barabara, miji, shule, hospitali na kadhalika.
11. **Jamhuri** ya Rwanda inashirikisha Wanyarwanda wote katika uongozi wao; walemavu, wanawake, wanaume na vijana.
12. **Serikali** ya Rwanda inahimiza umoja na ushirikiano wa Wanyarwanda.
13. **Sheria** ya Rwanda inakataa kutumia watoto kufanya kazi ngumu.

### *Zoezi la 2*

Jipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha mhusishe sentensi zilizo hapo chini na kinachoendelea katika picha zifuatazo.

| I. | II. | III. |
|---|---|---|
|  |   |  |

a) Wanyarwanda wote hukutana na kusafisha mazingira, kuchimba

mifereji ya maji, kutengeneza barabara, na kadhalika. Shughuli hizi zinajulikana kwa jina la *'Umuganda'*.

b) Kushirikiana katika kazi ni miongoni mwa shughuli za kuendeleza nchi yangu.

c) Bendera ya taifa la Rwanda imepandishwa mbele ya wanafunzi wa shule yetu. Bendera pia inaonekana katika ofisi ya mkuu wa mkoa wa kusini.

### *Zoezi la 1*

**Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadili kuhusu shughuli mbalimbali za kimaendeleo zinazofanywa katika vijiji vyenu.**


### *Zoezi la 2*

**Jibu maswali yafuatayo kuhusu uongozi na maeneo mbalimbali.**

1. Nchi yangu ni ____________________.
2. Bara langu ni _______________.
3. Rwanda imezungukwa na nchi mbalimbali: Kusini kuna ____________ Kaskazini kuna _______________, Mashariki kuna ____________ na Magharibi kuna_________________.
4. Mkoa wangu ni _____________, wilaya yangu ni _____________, tarafa yangu ni _______________ na kata yangu ni _______________.
5. Wananchi wa Rwanda wanaitwa _______________. Wananchi wa Burundi wanaitwa _______________. Wananchi wa Uganda ni _____________ na wananchi wa Kenya ni _______________.
6. Rais wa nchi yangu anaitwa ______________.
7. Watu wanaowawakilisha Wanyarwanda na kuandaa sheria nzuri ni _______________.
8. Shughuli zinazoendelezwa katika nchi yangu ni _______________.
9. Mkuu wa mkoa wangu anaitwa ______________. Mkuu wa wilaya yangu ni _______________. Mkuu wa tarafa yangu anaitwa _______________. Mkuu wa kata yangu ni _______________ na Mkuu wa kijiji changu anaitwa _______________.
10. Kwa kujichagulia viongozi wazuri wananchi wa _______________ ya Rwanda wanashirikiana wote.

## C. Dira ya dunia

Tazama mchoro ufuatao kisha utoe maoni yako kuhusu sehemu mbalimbali unazoziona kwa kuzilinganisha na maelezo yaliyo hapo chini.




1. Kaskazini
2. Kaskazini Mashariki
3. Mashariki
4. Kusini Mashariki
5. Kusini
6. Kusini Magharibi
7. Magharibi
8. Kaskazini Magharibi

### Maelezo muhimu

1. Dira ni chombo ambacho hutumiwa kuwaelekeza wasafiri katika pande za Dunia.
2. Pande nne kuu za Dunia ni: Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi.
3. Jua huchomoza kutoka upande wa Mashariki. Wakati huu huitwa macheo.
4. Jua hutua upande wa Magharibi. Wakati huu huitwa machweo.

### Zoezi la 3

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadili maswali yaliyo hapa chini kisha myanakili katika madaftari yenu.

1. Taja upande ulio kati ya Kaskazini na Magharibi.
2. Taja upande ulio kati ya Mashariki na Kusini.
3. Lango la shule yenu liko upande upi kutoka darasa lenu?

### i) Msamiati wa siku za wiki

Jigaweni katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha mzitaje siku za wiki mnazozifahamu.

### Tathmini

a) Siku za wiki huwa ngapi? Zitaje.

b) Aghalabu siku za mapumziko kwa ajili ya shughuli za kidini huwa zipi?

### Maelezo muhimu

a) Wiki pia huitwa juma.

b) Wiki moja ina siku saba ambazo ni: Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.

c) Wanafunzi katika shule nyingi huhudhuria masomo kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Ijumaa, Jumamosi na Jumapili wanafunzi Waislamu na Wakristo huhudhuria ibada zao tofauti tofauti.

### Matumizi katika sentensi

1. Tutafanya mtihani Jumatatu ijayo.
2. Baba yangu hupenda kucheza kandanda Alhamisi.
3. Kaka yangu atasafiri Ijumaa asubuhi.
4. Sisi huenda kanisani kila Jumapili.
5. Mama hupenda kufua nguo zetu Jumamosi.

*Zoezi la Mjadala*

**Jadili mbele ya wanafunzi wenzako shughuli zako za kila siku kuanzia Jumatatu hadi Jumapili.**

### ii) Miezi ya mwaka

Andika katika daftari lako miezi yote iliyo katika kalenda ya mwaka ambayo unaifahamu.

### Tathmini

1. Taja mwezi wa kwanza wa mwaka.
2. Taja mwezi wa nne wa mwaka.
3. Taja miezi miwili iliyo katikati ya mwaka.
4. Taja mwezi wa mwisho wa mwaka.

Jigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha mjibu maswali ya tathmini yaliyo hapo juu.

### Maelezo muhimu

Mwaka ni jumla ya miezi kumi na miwili ya kalenda ambayo ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Januari | 2. Februari | 3. Machi | 4. Aprili |
| 5. Mei | 6. Juni | 7. Julai | 8. Agosti |
| 9. Septemba | 10. Oktoba | 11. Novemba | 12. Disemba |

### Matumizi katika sentensi:

1. Tutafungua shule Januari tarehe tano.
2. Likizo ya mama huwa mwezi wa Aprili.
3. Mhubiri mashuhuri atakuja kanisani kwetu Agosti.
4. Sikukuu ya Krismasi husherehekewa Disemba.

**Soma kifungu kifuatacho:**

Sikukuu ya Noeli (Krismasi) husherehekewa mwezi wa Disemba tarehe ishirini na tano kila mwaka. Huu huwa wakati wa Wakristo kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu Kristo wanayemwamini kuwa Mkombozi wao. Tarehe ishirini na sita Disemba kila mwaka huwa siku ya mapumziko ambapo watu hupeana na kupokea zawadi za Krismasi. Hii huwa ishara ya kukumbuka Yesu Kristo alivyopewa zawadi alipozaliwa.

Tarehe moja mwezi wa Januari, watu wengi hufurahia kumaliza mwaka na kuanza mwaka mpya. Sikukuu ya Mashujaa wa Rwanda huadhimishwa tarehe ya kwanza ya mwezi wa Februari. Hii huwa siku ya kuwasherehekea mashujaa katika nchi yetu. Mashujaa ni watu mashuhuri ambao wamechangia katika maendeleo, ukombozi na marudiano katika nchi yetu ya Rwanda. Tarehe saba ya mwezi wa Aprili huwa siku ya makumbusho ya mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi yaliyofanyika mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na nne.

Sikukuu ya Wafanyakazi huwa tarehe moja ya mwezi wa Mei. Hii huwa siku ya kuwasherehekea wafanyakazi wote nchini mwetu. Sikukuu ya Uhuru huwa tarehe moja ya mwezi wa Julai. Tarehe nne ya mwezi wa Julai huwa sikukuu ya Ukombozi. Siku ambayo inaaminika Maria alienda mbinguni (*Assumption*) husherehekewa tarehe kumi na tano mwezi wa Agosti. Sikukuu ya Watakatifu wote husherehekewa tarehe moja ya mwezi wa Novemba. Sikukuu za Pasaka, Ijumaa kuu na *Idi-ul-fitri* ni sherehe za kidini zisizokuwa na tarehe maalumu mwakani.

Mwezi wa Machi, mwezi wa Aprili na mwezi wa Mei ni msimu wa mvua nyingi nchini Rwanda. Miezi ya Juni, Julai na Agosti ni kipindi kirefu cha jua kali. Miezi ya Septemba, Oktoba, Novemba na Disemba pia ni kipindi kirefu cha mvua kiasi nchini kote.

### *Zoezi la 1*

1. Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, andika majina ya miezi ya mwaka yaliyojitokeza katika kifungu kilicho hapo juu.
2. Yapange majina hayo ya miezi kuanzia mwezi wa kwanza wa mwaka hadi mwezi wa mwisho wa mwaka.

### *Zoezi la 2*

Soma tena kifungu kilicho hapo juu. Baada ya kusoma, dhihirisha vipindi vya misimu mbalimbali vinavyopatikana nchini Rwanda.

### Zoezi la 3

Nakili maswali haya katika daftari lako kisha ujaze nafasi zilizo wazi kwa majibu sahihi.

1. Ni mwezi upi ulio katikati ya Mei na Julai? ____________________
2. Siku ya wafanyakazi duniani husherehekewa mwezi upi? _______________
3. Taja mwezi wa saba katika kalenda ya mwaka _______________.
4. Mwezi wa kwanza katika kalenda ya mwaka ni upi? _______________

## D. Sarufi

### Umoja na wingi wa majina katika ngeli ya I-ZI

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tungo zifuatazo **katika umoja na wingi**, kisha mjadili mabadiliko yanayojitokeza.

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Nchi inaendelea sana. | Nchi zinaendelea sana. |
| 2. | Nguo itashonwa. | Nguo zitashonwa. |
| 3. | Sahani imevunjika. | Sahani zimevunjika. |
| 4. | Nyumba imebomoka. | Nyumba zimebomoka. |
| 5. | Ngozi imepakwa mafuta. | Ngozi zimepakwa mafuta. |

### Tathmini:

Umegundua nini kutokana na sentensi zilizo hapo juu?

### Maelezo muhimu

Katika upatanisho wa kisarufi, majina katika ngeli ya I-ZI hutumia kiambishi 'i-' katika umoja na kiambishi 'zi-' katika wingi. Tazama sentensi 1-5 zilizo hapo juu.

**Majina katika ngeli ya I-ZI huwa hayabadiliki katika umoja na wingi. Hubaki vilevile. Kwa mfano:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Nyumba | Nyumba |
| Kofia | Kofia |
| Karatasi | Karatasi |
| Sahani | Sahani |
| Taa | Taa |
| Saa | Saa |

### *Zoezi la 1*

Katika makundi ya wanafunzi watatu:

a) Andika majina kumi katika ngeli ya I-ZI katika umoja na wingi.

b) Tunga sentensi kumi katika umoja na wingi katika ngeli ya I-ZI.

### *Zoezi la 2*

**Linganisha maneno katika kila kifungu cha sentensi ulizosoma katika umoja na wingi.**

### *Zoezi la 3*

**Andika sentensi zifuatazo katika wingi.**

**Mfano:** Bendera ile inapepea.
**Jibu:** Bendera zile zinapepea.

1. Shule ile imefunguliwa.
2. Ngazi iliyonunuliwa imevunjika.
3. Saa yake imeuzwa.
4. Kofia ya baba imepotea.
5. Taa ile itazimika.

## E. Mazoezi ya marudio

### *Zoezi la 1*

**Katika daftari lako, kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiambishi cha ngeli kinachofaa.**

**Mfano:** Nchi ya Burundi ___ napakana na nchi ya Tanzania.

**Jibu:** Nchi ya Burundi inapakana na nchi ya Tanzania.

1. Jamhuri ya Rwanda ___napakana na Jamhuri ya Burundi huko Kusini.
2. Wilaya za Rubavu na Ngororero ___najitokeza katika jimbo la Magharibi.
3. Jamhuri za bara la Afrika ___nashirikiana katika maendeleo ya wananchi wake.
4. Nchi za Afrika Mashariki ___natumia lugha ya Kiswahili.
5. Tarafa ya Nyarugenge ___mejengwa katikati mjini Kigali.
6. Nchi za Ubelgiji na Ufaransa ___najitokeza barani Ulaya.
7. Nchi ya Marekani ___na raia wengi.
8. Nchi ya Uchina ___na teknolojia nzuri.
9. Shule yangu __na walimu wenye bidii lakini shule ya Muneza na shule ya Musana __na walimu wavivu.
10. Karatasi zangu ___meanguka chini.

### *Zoezi la 2*

**Andika umoja au wingi wa sentensi zifuatazo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika daftari lako.**

Mfano: Likizo yake itaanza kesho

Jibu: Likizo zao zitaanza kesho.

| | **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|---|
| 1. | Nyumba yangu inajengwa. | - | ______________________ |
| 2. | ______________________ | - | Kalamu zenu zinaandika vizuri. |
| 3. | Sauti yako inapendeza sana. | - | ______________________ |
| 4. | Baiskeli yake imeharibika. | - | ______________ __________ |
| 5. | ______________________ | - | Suruali zao zimechafuka sana. |

6. ______________________ - Ndege zao zimeanguka.

7. Mama anafua nguo yake. - ______________________

8. Wewe unapaza sauti yako. - ______________________

9. Kampuni yao imestawi tena. - ______________________

10. ______________________ - Barabara zetu zinajengwa vijijini.

### *Zoezi la 3*

**Sentensi hizi zina makosa. Zisahihishe.**

1. Nguo nyake imechanika.
2. Kaka wako anavuka mpaka wa Gatuna kuenda nchi ya Uganda.
3. Dada wangu na kaka wetu wanasoma vizuri.
4. Mama wetu wanalima shamba na baba wetu wanavuna.
5. Mtoto mwangu anaenda kwenye ofisi ya wilaya wetu.
6. Tarafa zangu ina miradi ya kuendeleza wananchi.
7. Baiskeli yetu imetengezwa.
8. Kalamu kangu zinaandika vizuri.
9. Nyumba nyetu inajengwa mjini Kigali.
10. Nchi nyao inatajirika siku baada ya siku.

### *Zoezi la Kuigiza*

Mbele ya wanafunzi wenzako, jitambulishe kwa kueleza jina lako, mkoa au jimbo lako, wilaya yako, tarafa yako, kata yako na kijiji chako.

**Mfano:** Mimi ninaitwa *Amahoro*, ninaishi mkoa wa *Kaskazini* nchini Rwanda.

### *Zoezi la Imla*

Funga kitabu chako, kisha katika daftari lako, andika kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno utakavyosomewa na mwalimu wako.

# Ofisi ya Tarafa Yangu

### Tazama picha hii:




***Zoezi la makundi***

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi kwa kueleza mnachokiona katika picha iliyo hapo juu.

### Mazungumzo kuhusu ofisi za kiutawala

Soma mazungumzo yaliyo hapo chini kati ya Sugira, Uwera na Mpigapicha. (*Sugira anamkuta Uwera kwenye tarafa yao ya Nyarubaka na kuanza kuzungumza. Sugira anahitaji kitambulisho na Uwera anataka kumwona Afisa wa Elimu ili atoe ombi lake kuhusu kubadilisha shule.)*

**Sugira:** Habari za siku nyingi Uwera?

**Uwera:** Nzuri. Kumbe wewe pia uko hapa?

**Sugira:** Ndiyo. Ninataka kitambulisho.

**Uwera:** Wewe una umri wa kupata kitambulisho?

**Sugira:** Ndiyo. Ninataka kupiga picha ya kuweka kwenye kitambulisho. Je, na wewe pia unahitaji kitambulisho?

**Uwera:** Hapana. Mimi ninataka kumwona Afisa wa Elimu. Ninataka kubadilisha shule.

**Sugira:** Unataka kuendeleza masomo yako katika shule gani?

**Uwera:** Ninataka kuendeleza masomo yangu katika shule ya Sekondari ya Nyamabuye. Shangazi yangu anaishi mjini Muhanga. Yeye ananisaidia katika masomo yangu.

**Sugira:** Sawa. Shule ya Nyamabuye ni nzuri na ina walimu wazuri. Je, likizo hii ilikuwa vipi?

**Uwera:** Likizo hii ilikuwa nzuri. Mimi nilimtembelea nyanya yangu na kumsaidia katika kazi za kilimo.

**Sugira:** Je, nyanya yako ana mashamba karibu na mabonde ya maji? Msimu huu ni wa jua kali.

**Uwera:** Kweli. Wakulima wengi hulima sana kuanzia mwezi wa Septemba hadi mwezi wa Novemba kila mwaka. Lakini, yeye hupanda mimea tofauti karibu na Mto Mukungwa.

*(Sugira anaangalia upande ambapo kuna Mpiga picha. Anaona kuwa ni zamu yake ya kupigwa picha.)*

**Sugira:** Ah! Sasa ninaona kuwa ni zamu yangu ya kupigwa picha. Acha niende.

**Uwera:** Sawa. Na mimi ninaenda kumwona Afisa wa Elimu ili anihudumie.

**Sugira:** Sawa. Tutaonana.

**Mpiga picha:** Sugira!

**Sugira:** Abeee!

**Mpiga picha:** Kuja hapa. Jipange vizuri. Kaa vizuri nikupige picha.

**Sugira:** Sawa.

*(Sugira anapigwa picha)*

**Mpiga picha:** Fika Jumatatu wiki ijayo upate kitambulisho chako.

**Sugira:** Asante sana.

**Mpiga picha:** Karibu. Safari njema.

**Sugira:** Asante.

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena mazungumzo kati ya Uwera, Sugira na Mpiga picha. Sasa jibu maswali yanayofuata.**

1. Uwera na Sugira wanakutania wapi?
2. Sugira anatafuta nini?
3. Uwera, anataka kumwona nani?
4. Uwera anahitaji huduma gani?
5. Uwera anataka kuendeleza masomo yake katika shule gani?
6. Katika likizo, Uwera alifanya nini?
7. Katika msimu wa mvua wakulima hupanda nini?
8. Msimu wa mvua hujitokeza lini?
9. Wanyama wanakosa nyasi za kula katika kipindi gani?
10. Sugira atarudi kupata kitambulisho lini?

## A. Msamiati kuhusu ofisi za kiutawala

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena kifungu cha mazungumzo yaliyo hapo juu. Jaribuni kutafuta maana za msamiati mpya. Zingatieni matumizi ya msamiati huo katika kifungu cha mazungumzo husika. Tumieni kamusi ya Kiswahili pale panapohitajika.

**Kwa mfano:**

***Kitambulisho*:** cheti au kadi yenye picha inayotumika kumtambulisha mtu au kujulisha mtu fulani ni nani

### *Zoezi la maigizo*

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jaribu kuigiza mazungumzo kati ya Uwera, Sugira na Mpinga picha.

### *Zoezi la 1*

Kwa kuzingatia mifano ya sentensi zilizotolewa hapa chini, jaribu kutunga sentensi moja moja kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari.

- Nchini Rwanda kuna msimu wa mvua nyingi kuanzia mwezi wa Septemba hadi Disemba. Msimu wa jua kali huanzia mwezi wa Juni hadi mwezi wa Agosti.
- Afisa wa kilimo katika tarafa yangu anahimiza wananchi kupanda mbegu nzuri za mahindi.
- Wakulima katika nchi yangu wanapanda mimea mbalimbali: maharagwe, mahindi, mihogo na kadhalika.
- Mwezi wa kwanza wa mwaka ni Januari.
- Mkuu wa Tarafa yangu anahudumia raia vizuri na kutatua shida zao.
- Ni lazima kuonyesha afisa wa benki kitambulisho chako ili uweze kulipwa kutoka benki.
- Kitambulisho changu kina picha nzuri.
- Mto wa Mukungwa unapita katika wilaya za Gakenke na Musanze.

### *Zoezi la 2*

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia moja ya maneno yafuatayo kwa kila pengo:**

mimea, picha, kitambulisho, mwezi, mpaka, msimu, kuhudumia,

imekamilika, zamu, Afisa wa Elimu, mwaka

**Mfano:** Kamana anaingia ofisini ili ahudumiwe. Sasa ni __________ yake ya kumwona Mkuu wa Tarafa.

**Jibu:** Kamana anaingia ofisini ili ahudumiwe. Sasa ni **zamu** yake ya kumwona Mkuu wa Tarafa.

1. Katika ___________ wa Aprili kuna mvua nyingi sana.
2. Nchini Rwanda, ___________ una vipindi viwili vya mvua na vipindi viwili vya jua.
3. Sasa ni ___________ yangu ya kuonana na mkuu wa wilaya.
4. Kuanzia Juni hadi Agosti ni ___________ wa jua kali.
5. Mkuu wa shule yangu anatuomba kuleta ___________ za kuweka kwenye vitambulisho vya shule.
6. ___________ mingi inapandwa wakati wa mvua.
7. Mto Akanyaru unapitia kwenye ___________ wa nchi za Rwanda na Tanzania.
8. Mkuu wa Kata ya Rwigerero anapenda ___________ wananchi na kutatua shida zao.
9. Gasore anatoka kuomba ___________ kwenye ofisi ya mkuu wa tarafa yake.
10. ___________ anapenda kuchunguza usafi shuleni.

## B. Sarufi: Ngeli ya U-I

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni sentensi zifuatazo. Jaribuni kutambua sifa zake za umoja na za wingi.

**Umoja:** **Mw**aka **u**naanza kwa tarehe ya kwanza ya mwezi wa Januari.

**Wingi:** **Mi**aka **i**naanza kwa tarehe za kwanza za miezi ya Januari.

**Umoja:** **Mw**ezi **u**na siku nyingi.

**Wingi:** **Mi**ezi **i**na siku nyingi.

**Umoja:** **M**mea **u**napandwa shambani.

**Wingi:** Mimea inapandwa mashambani.

**Umoja:** Mto unafurika katika msimu wa mvua.

**Wingi:** Mito inafurika katika misimu ya mvua.

**Umoja:** Mguu unatembea haraka.

**Wingi:** Miguu inatembea haraka.

### *Zoezi la 1*

**Linganisha maneno yaliyopigiwa mstari katika kila kifungu cha sentensi hapo juu.**

**Mfano:**

**Umoja:** **Mguu unatembea** haraka.

**Mmea unapandwa** shambani.

**Jibu:**

Mguu unatembea/mmea unapandwa: kiambishi ***'u-'*** katika kitenzi **unatembea** ni sawa na kiambishi ***'u-'*** katika kitenzi **unapandwa.**

- ***'u-'*** ni kiambishi cha nafsi katika vitenzi **unatembea** na **unapandwa**.
- Kiambishi hiki ***'u-'*** kinawakilisha nafsi za majina **mguu** katika sentensi ya kwanza na **mmea** katika sentensi ya pili.

**Mguu** - **u +** natembea

**Mmea** - **u +** napandwa

### *Zoezi la 2*

**Andika sentensi zifuatazo katika wingi, kisha ulinganishe maneno yaliyopigiwa mstari.**

1. Mkeka unatandazwa chini.
2. Mtego unanasa wanyama.
3. Mgongo unasafishwa vizuri.
4. Mwezi unaanza leo.

5. Mwaka unatosha kukamilisha miradi yote.

## Tazama:

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| a) **Mwaka** **u**naanza katika mwezi wa Januari. | **Miaka** **i**naanza katika miezi ya Januari. |
| b) **Mwezi** **u**na wiki nne. | **Miezi** **i**na wiki nne. |
| c) **Msimu** wa jua **u**naanza katika mwezi wa Juni. | **Misimu** ya jua **i**naanza katika miezi ya Juni. |

Sehemu za maneno zilizopigiwa mstari ni viambishi nafsi vya vitenzi. Viambishi hivyo ni '***u-***' katika umoja na '***i-***' katika wingi. Katika sentensi (a) jina ***mwaka*** ndilo linarejelewa na kiambishi '***u-***' katika umoja na kiambishi '***i-***' kinarejelea jina ***miaka*** katika wingi. Katika sentensi (b) kiambishi '***u-***' kinarejelea jina ***mwezi*** katika umoja na kiambishi '***i-***' kinarejelea jina ***miezi*** katika wingi. Katika sentensi (c) kiambishi '***u-***' kinarejelea jina ***msimu*** katika umoja na kiambishi '***i-***' kinarejelea jina ***misimu*** katika wingi.

### *Zoezi la 3*

**Andika sentensi hizi katika umoja au wingi.**

**Mfano:** Mkono unaniuma. (*Umoja*)

**Jibu:** Mikono inatuuma. (*Wingi*)

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mchango umetolewa. | ________________ |
| 2. ________________ | Miguu inanenepa. |
| 3. ________________ | Mipapai inachumwa. |
| 4. Mtama unalimwa. | ________________ |
| 5. Mgomba umepandwa. | ________________ |
| 6. Mnanasi umeuzwa. | ________________ |

7. ______________________ Migongo inapendeza.

8. ______________________ Milango imefungwa.

9. Msitu unatisha. ______________________

10. Mto umefurika. ______________________

11. ______________________ Misumari imenichoma.

12. Mwili umesafishwa. ______________________

13. ______________________ Miti imeanguka.

14. Mchungwa umekatwa. ______________________

15. ______________________ Mikeka imeharibika.

### *Zoezi la 4*

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni sentensi zinazofuata. Baada ya kusoma, tungeni sentensi zenu zinazofanana nazo:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mimi nina **m**chungwa.<br>**M**chungwa **wa**ngu una machungwa. | Sisi tuna **mi**chungwa.<br>**Mi**chungwa **ye**tu ina machungwa. |
| Wewe una **m**chungwa.<br>**M**chungwa **wa**ko unamea. | Nyinyi mna **mi**chungwa.<br>**Mi**chungwa **ye**nu inamea. |
| Yeye ana **m**chungwa.<br>**M**chungwa **wa**ke unakatwa. | Wao wana **mi**chungwa.<br>**Mi**chungwa **ya**o inakatwa. |

**Tafakari:**

- Maneno kama ***wangu, wako, wake, yetu, yenu*** na ***yao*** yanaonyesha kuwa kitu kinachotajwa ni cha mtu fulani au mali ni ya mtu fulani na hutumiwa pamoja na majina yenye kuwakilishwa na ***'u-'*** katika vitenzi (umoja) na ***'i-'*** katika vitenzi (wingi).

### *Zoezi la ziada*

**Kamilisha sentensi zinazofuata kwa kutumia kivumishi kikamilishi au kiambishi kinachofaa.**

**Mfano:** Afisa wa kilimo amenipendekeza kupanda mti _________ (*wa mimi*) katika shamba hili.

**Jibu:** Afisa wa kilimo amenipendekeza kupanda mti ***wangu*** katika shamba hili.

1. Muhire na Mukamunana wanatandika mikeka _________ (*ya wao*) katika chumba cha wageni.
2. Msumari _________ (*wa wewe*) unapigiliwa ndani ya mti _________ (*wa yeye*).
3. Ni lazima watoto wasafishe miguu _________(*ya wao*).
4. Mji wa Kigali ___meimarisha usafi. Wageni wote wanasema kuwa ni mji mzuri sana.
5. Mkoa wa Kaskazini ___natunza wanyama vizuri.
6. Mikono _________ inafanya kazi vizuri (*ya wao*)
7. Mguu _________ (*wa wewe*) unatibiwa sasa hivi.
8. Milima _________ (*ya mimi*) ina miti mirefu.
9. Miti _________ (*ya wewe*) inapatikana sana wakati wa kiangazi.
10. Miji _________ (*ya nyinyi*) inajengwa nchini Rwanda.

**ELIMU NI MUHIMU KWA VIJANA**

## Somo La Tatu

# Utawala Bora

**Tazama picha hii:**



Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tungeni sentensi kueleza kinachoendelea katika picha iliyo hapo juu.

### *Zoezi la mazungumzo*

Soma kifungu cha mazungumzo kinachofuata kati ya Keza na Simbi.

*(Wao wanakutana njiani. Keza anaelekea kwenye ofisi ya tarafa yake kuomba kazi ya muda mfupi na Simbi anaelekea nyumbani. Wao wanaanza kuzungumzia miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika tarafa yao.)*

**Keza:** Habari gani Simbi?

**Simbi:** Nzuri. Mbona una haraka sana?

**Keza:** Ninataka kufika kwenye ofisi ya tarafa yangu.

**Simbi:** Unataka kufanya nini huko?

**Keza:** Ah! Kuna tangazo la kazi ya muda mfupi.

**Simbi:** Kazi gani hiyo?

**Keza:** Viongozi wetu wanapanga shughuli za kusajili watu wote

wasiojiweza.

**Simbi:** Ala! Ninakumbuka…Katika mradi wa *Gira inka Munyarwanda*.

**Keza:** Katika kijiji changu, viongozi na wananchi wanafanya mkutano leo.

**Simbi:** Sawa. Ni mkutano wa kuandaa orodha ya watu hao wenye uwezo wa chini?

**Keza:** Ndiyo. Wanakijiji wote wanashiriki kuandaa orodha hiyo.

**Simbi:** Mradi huu ni mzuri sana. Wananchi wengi wanapata faida kubwa kutokana na mradi huu.

**Keza:** Ndiyo! Huu ni mradi mmoja kati ya miradi mingine mizuri inayowasaidia wananchi.

**Simbi:** Ndiyo. Lakini mimi napenda sana mradi wa ushirika wa wananchi katika bima ya afya ili kupambana na magonjwa mbalimbali.

**Keza:** Kweli kabisa! Huu nao ni mradi mzuri pia.

*(Simbi anatazama kwenye saa yake)*

**Simbi:** Eh! Acha niende sasa hivi. Mamangu ananingoja.

**Keza:** Sawa. Kwaheri. Wasalimie nyumbani.

**Simbi:** Sawa. Kwaheri ya kuonana.

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena mazungumzo yaliyo hapo juu kati ya Keza na Simbi, kisha kamilisha sentensi zinazofuata kwa kutumia maneno haya:**

mfupi, tajiri, mradi, bima, kujitibisha, magonjwa, kazi, Rwigerero, mkutano, wananchi, maskini, kufika

1. Keza ana haraka kwa sababu anataka __________ kwenye ofisi ya tarafa yake.
2. Keza amesoma tangazo la __________ ya muda __________.
3. Viongozi wamepanga shughuli za __________wasiojiweza.
4. Wasiojiweza ni watu _________.

5. ____________ wa *Gira Inka Munyarwanda* unasaidia sana ___________.
6. ___________ wa viongozi na wananchi umefanywa.
7. Katika kijiji cha ___________ wananchi wote wamejitokeza kuandaa ___________ ya watu maskini.
8. Watu wanaopatwa na magonjwa wanaweza ___________ kwa urahisi.
9. Ushirika katika ___________ ya afya ni muhimu sana.
10. Watu wanajiepusha na ___________ kwa kuwa na miili safi.

## A. Msamiati wa utawala

**Soma mazungumzo hayo kwa kuandika msamiati ulio mpya kwako. Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jaribu kupata maana za msamiati huo kupitia mazungumzo mliyoyasoma. Mnaweza kutumia pia kamusi ya Kiswahili.**

**Kwa mfano:**

**Tangazo:** jambo lililotangazwa; jambo lililoelezwa ili watu walifahamu

### Maelezo muhimu

Ifuatayo ni orodha ya maeneo ya kiutawala nchini Rwanda:

Nchi - Mkoa - Wilaya - Tarafa - Kata - Kijiji/Kitongoji

### *Zoezi la 1*

**Soma mifano ya sentensi zilizotolewa hapa chini. Sasa jaribu kutunga sentensi moja moja kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari.**

- Watu walemavu wamejiendeleza nchini Rwanda. Wao hawaishi kwa <u>kuomba</u> misaada kutoka kwa watu wengine tena.
- Ni vizuri kuwa viongozi wetu <u>wanajali</u> mahitaji ya wananchi wote na kuwasaidia kutatua matatizo yao.
- Rais wa Rwanda anahimiza Wanyarwanda kufanya kazi vizuri ili wasiendelee kutegemea <u>misaada</u> kutoka nchi zilizoendelea.
- Kimana ni mtoto mwenye <u>afya</u> nzuri. Mama yake anamlisha chakula kizuri sana.

- Serikali ya Rwanda inasaidia wananchi maskini kwa kuwagawia ng'ombe katika mradi wa *Gira Inka Munyarwanda*.
- Ili kupambana na malaria, watu wanalala katika chandarua cha kuzuia mbu.
- Bwana Kagabo amepewa msaada wa ng'ombe. Sasa ng'ombe wake amezaa na yeye ametajirika.

### *Zoezi la 2*

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia moja kati ya maneno yaliyo kwenye mabano.**

1. Baba yangu anafanya __________ (masomo/shughuli) za biashara mjini Kigali.
2. Si vizuri kuendeleza tabia za kuomba __________ (misaada/umuhimu) kutoka nchi zilizoendelea.
3. Leo tunafanya __________ (mkutano/msaada) na mkuu wa shule yetu.
4. Watu wasiojiweza wanasaidiwa na __________ (serikali/shule) ya Rwanda ili watoke katika hali yao ya umaskini.
5. Nchi yangu ina __________ (maisha/mradi) wa kufundisha raia wote umuhimu wa kilimo bora.
6. Nchi yangu ina __________ (miradi/nyumba) mbalimbali: kujenga barabara, kujenga vituo vya afya na hospitali.
7. Wanakijiji wanafanya __________ (mkutano/muda) na mkuu wa kijiji ili kupanga miradi ya maendeleo ya kijiji chao.
8. Mimi nimetoa __________ (ombi/msaada) langu kwa mkuu wa shule ili anipe ruhusa.
9. Mukamwiza ni __________ (tajiri/maskini) sana. Yeye anafuga ng'ombe wa kisasa.
10. Mkuu wa tarafa yangu anafanya kazi nzuri kwa __________(kuendeleza/kusoma) tarafa yake.

## B. Sarufi: Ngeli ya U-I na vivumishi vya sifa

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni sentensi zinazofuata. Baada ya kusoma, tungeni sentensi zenu zinazofanana nazo.**

| | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|
| 1. | **M**saada **m**zuri umeletwa. | - | **Mi**saada **mi**zuri imeletwa. |
| 2. | **M**radi **m**zuri umetekelezwa. | - | **Mi**radi **mi**zuri imetekelezwa. |
| 3. | **M**kutano **m**dogo umefanywa. | - | **Mi**kutano **mi**dogo imefanywa. |
| 4. | **M**saada uliopangwa ni **m**kubwa sana. | - | **Mi**saada iliyopangwa ni **mi**kubwa sana. |

### Tafakari

- Maneno kama ***mzuri, mrefu, mkubwa, mbovu,*** yanaongeza sifa kwa kitu kinachotajwa na huweza kutumiwa pamoja na majina yenye kuwakilishwa na kiambishi ***'u-'*** katika vitenzi (*umoja*) na kiambishi ***'i-'*** katika vitenzi (*wingi*).

**Mifano:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. **M**gomba **m**refu **u**napendeza. | **Mi**gomba **mi**refu **i**napendeza. |
| 2. **M**radi **m**zuri **u**natekelezwa. | **Mi**radi **mi**zuri **i**natekelezwa. |
| 3. **M**to **m**dogo **u**mefurika. | **M**ito **m**idogo **i**mefurika. |
| 4. **M**sumari **m**baya **u**nanichoma. | **M**isumari **m**ibaya **i**natuchoma. |
| 5. **N**yumba **n**defu **i**mejengwa. | **N**yumba **n**defu **zi**mejengwa. |
| 6. Kalamu **n**zuri **i**naandika. | Kalamu **n**zuri **zi**naandika. |

| | |
|---|---|
| 7. **M**zazi **m**zuri **a**napenda watoto. | **Wa**zazi **wa**zuri w**a**napenda watoto. |
| 8. **Mw**anafunzi **m**baya anapiga kelele. | **W**anafunzi **wa**baya wanapiga kelele. |

**Lakini:**

| **Usitumie** | | **Tumia** |
|---|---|---|
| *__M__tu __m__maskini | - | __M__tu maskini |
| *__M__tu __m__tajiri | - | __M__tu tajiri |
| *__M__lima __m__safi | - | __M__lima safi |
| *__N__chi __n__safi | - | __N__chi safi |
| *__N__chi __n__tajiri | - | __N__chi tajiri |
| *__N__chi __n__maskini | - | __N__chi maskini |

### *Zoezi la 1*

**Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia viambishi sahihi.**

**Mfano:** **Mguu wake ni -zito.**
**Jibu:** **Mguu wake ni mzito.**

1. Mti huu ni _____refu lakini miti ile ni _____fupi.
2. Miguu yake ni _____zuri.
3. Mlima wa Kigali ni _____refu sana lakini milima mingine ni _____fupi.
4. Mimea hii ni _____zuri.
5. Miradi _____kubwa imepangwa na serikali ya nchi yangu.
6. Mlango _____dogo umefunguliwa.
7. Misaada _____zuri inatolewa kwa nchi zinazoendelea.
8. Mchango wa viongozi ni _____kubwa katika maendeleo ya nchi.
9. Mgomba _____refu umepandwa.
10. Migomba _____refu imepandwa.

## Zoezi la 2

**Andika sentensi hizi katika umoja au wingi.**

**Mfano:** **Mkoba mzuri umepotea.**

**Jibu:** **Mikoba mizuri imepotea.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mchungwa mrefu umekatwa. | ____________________ |
| 2. Mgomba mbovu umeungua. | ____________________ |
| 3. ________________________ | Milango mibovu imefungwa. |
| 4. ________________________ | Mikate mitamu imetupwa. |
| 5. ________________________ | Miguu midogo inauma. |
| 6. Mgongo mzuri unasafishwa. | ______________________ |
| 7. Mti mdogo umechomwa. | ______________________ |
| 8. Mto mchafu umefurika. | ______________________ |
| 9. Mlima mrefu unaonekana. | ______________________. |
| 10. Mnanasi mkubwa umezaa mananasi. | ______________________. |

## Zoezi la 3

**Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia kiambishi sahihi.**

1. Mwaka __na miezi mingi.
2. Miguu yake __nauma.
3. Mlima huu __na miti __refu.
4. Misumari __refu __meletwa.
5. Penseli zako __mepotea.

6. Shule yenu __na wanafunzi na walimu wazuri.
7. Miradi __kubwa __mepangwa na serikali ya nchi yangu.
8. Nchi yangu __nasaidia wananchi.
9. Misaada __zuri inatolewa kwa wananchi.
10. Mchango wa viongozi ni __kubwa katika maendeleo ya nchi.

***Zoezi la 4***

**Sentensi hizi zina makosa. Zisahihishe kwa kuziandika upya katika daftari lako.**

1. Mtoto baya anakimbia.
2. Walimu mzuri anafundisha.
3. Migomba mbovu imepandwa.
4. Mtu msafi anatembea.
5. Watoto wasafi wanasoma Kiswahili.
6. Nyumba zirefu zinasafishwa.
7. Mwanafunzi anaandika kwa kutumia kalamu kazuri.
8. Kalisa na Mutoni wanapanda milima refu.
9. Mwalimu huyu ni mtajiri.
10. Kamana amesaidia mtu mmaskini.

## C. Kusikiliza na kuzungumza

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, zungumzia miradi mbalimbali inayosaidia wananchi kutoka katika umaskini na kuingia katika utajiri.

***Zoezi la imla***

**Funga kitabu chako. Katika daftari lako, andika kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno utakavyosomewa na mwalimu wako.**

## Faharasa

**Afya:** kuwa bila magonjwa

**Bara:** kontinenti, eneo kubwa la ardhi ya dunia lililozungukwa na bahari: Asia, Afrika, Marekani ya kaskazini, Antaktika, Marekani ya kusini, Uropa (ulaya) na Australia

**Barabara:** njia ya magari, pikipiki na vyombo vingine vya usafiri

**Bonde:** sehemu iliyo baina ya milima na ambapo maji huteremkia

**Bora:** kitu kinachopendeza, kizuri sana

**Bunge:** baraza la kutunga sheria linaloundwa na watu walioteuliwa na wananchi

**Chagua:** teua kitu miongoni mwa vitu vingine, kupiga kura

**Dunia:** ulimwengu, eneo ambapo watu wote, mimea na wanyama huishi

**Faidika:** nufaika, kupata faida

**Haraka:** upesi

**Hospitali:** mahali ambapo wagonjwa huenda kuona madaktari na kupata dawa au matibabu

**Hudumia:** toa msaada kwa mtu mwingine, kusikiliza matatizo ya mtu au shida zake ili kumsaidia

**Ishi:** kaa mahali fulani, kuwa na maskani, kuwa na uhai

**Jali:** weka kwenye mawazo mema

**Jamhuri:** nchi huru inayotawaliwa na rais wa kuchaguliwa na wananchi

**Karibia:** sogelea, kuwa karibu na kitu au mahali fulani

**Kitambulisho:** cheti au kadi yenye picha inayotumika kumtambulisha mtu. Kadi hiyo inaweza kuhitajika mahali pa kazi, kwenye benki au katika huduma nyingine

**Kura:** uchaguzi wa kumpata mtu mmoja kati ya wengine katika nafasi ya uongozi

**Magonjwa:** maradhi

**Maisha:** muda wa kuishi, uzima, uhai

**Malizika:** kufika mwisho, kuisha, kukamilika

**Mbalimbali:** tofauti

**Mbegu:** punje ambayo hupandwa ili kutoa mmea

**Mchango:** vitu vyovyote vinavyotolewa, shughuli yoyote inayofanywa kwa ajili ya jambo maalum kama vile kujenga shule, hospitali, barabara, na kadhalika

**Mkulima:** mtu anayefanya kazi ya kulima shamba, mtu mwenye shamba na anayelilima

**Mkutano:** mkusanyiko wa watu kwa lengo maalum

**Mmea:** kitu chenye mizizi, shina, matawi na majani ambacho kinatoa mbegu

**Mradi:** mpango wa kufanya jambo fulani

**Msaada:** usaidizi kwa mtu mwingine

**Msimu:** kipindi maalumu katika mwaka ambapo jambo fulani hutokea

**Mtaa:** sehemu ya mji inayojitenga na sehemu nyingine ya mji kulingana na shughuli zinazofanywa au ujenzi wa mji wenyewe

**Muhimu:** kitu chenye maana

**Mwananchi:** mtu ambaye amezaliwa na kuishi katika nchi fulani

**Mwezi:** umbo la mviringo linaloangaza usiku, moja kati ya vipindi 12 katika mwaka

**Ombi:** jambo analotaka mtu

**Orodha:** mfululizo wa vitu fulani

**Picha:** sura ya kitu au mtu iliyopigwa au kuchorwa

**Punguka:** kuwa chache katika idadi au hali

**Raia:** mtu ambaye ana haki za kisheria za kuishi katika nchi fulani

**Rais:** kiongozi wa jamhuri fulani

**Sajili:** andikisha kwenye kitabu teule

**Serikali:** mfumo wenye utawala katika nchi

**Sheria:** kanuni zilizotungwa

**Wasiojiweza:** watu wenye upungufu wa mapato

## Mada Kuu

# Msamiati wa Mazingira Mbalimbali

## Mada Ndogo

# Msamiati wa Mazingira ya Sokoni

**Somo la Kwanza:** i) Mnunuzi na Muuzaji

ii) Alama za hesabu

iii) Vipimo na matumizi yake katika hesabu

**Somo la Pili:** Biashara Mbalimbali

**Somo la Tatu:** Mazingira ya Sokoni

Somo la Kwanza

# Mnunuzi na Muuzaji

**Tazama picha hii:**

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni kinachoendelea katika picha iliyo hapo chini.



## A. Mazungumzo kati ya muuzaji na mnunuzi

### *Zoezi la kusoma*

Soma kifungu cha mazungumzo kinachofuata kati ya mnunuzi na muuzaji.

*(Mnunuzi anataka kununua vitu mbalimbali sokoni. Muuzaji anampokea vizuri. Yeye anamuonyesha vitu tofauti anavyoviuza na kumuomba anunue.)*

**Muuzaji:** Karibu mteja wangu, karibu sana hapa! Kila kitu ni bei rahisi sana. Karibu!

**Mnunuzi:** Asante.

**Muuzaji:** Unataka nini? Angalia vizuri. Kila kitu kipo.

**Mnunuzi:** Mbona leo hujaleta machungwa?

**Muuzaji:** Machungwa hayapatikani sana siku hizi.
Lakini, tazama vizuri. Kuna vitu vingine na hata matunda mengine yapo: mananasi, maembe na maparachichi.

**Mnunuzi:** Ninataka maembe matatu, nyanya, sukari kilo tatu na chumvi kilo moja na nusu.

**Muuzaji:** Sawa. Embe moja ni faranga hamsini, sukari ni faranga mia saba, chumvi kilo na nusu ni faranga mia mbili. Fungu moja la nyanya ni faranga mia moja.

**Mnunuzi:** Mbona unapandisha bei! Punguza kidogo! Huoni kwamba sukari inapatikana siku hizi! Nyanya zina bei rahisi vilevile. Tafadhali, punguza kidogo!

**Muuzaji:** Sawa. Nyanya unataka mafungu mangapi?

**Mnunuzi:** Mafungu matatu.

**Muuzaji:** Wewe ni mteja wangu wa kawaida. Leta sabini kwa fungu moja.

**Mununuzi:** Sawa. Na sukari?

**Muuzaji:** Sukari? Leta mia sita na hamsini basi.

**Mnunuzi:** Asante sana. Nipimie kila kitu. Pesa ziko hapa.

**Muuzaji:** Asante sana. Ngoja nikuwekee katika mkoba huu.

**Muuzaji:** Sawa. Niwekee.

*(Muuzaji anamwekea bidhaa katika mkoba, kisha anampatia)*

**Muuzaji:** Kila kitu kipo tayari.

**Mnunuzi :** Asante sana.

**Muuzaji:** Karibu. Karibu tena.

**Mnunuzi:** Sawa. Kwaheri.

**Muuzaji:** Kwaheri ya kuonana.

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena mazungumzo yaliyo hapo juu kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Kwa sababu gani muuzaji hana machungwa?

2. Mnunuzi anataka kununua nini?

3. Embe moja ni faranga ngapi?

4. Muuzaji anauza matunda ya aina gani?
5. Mnunuzi anataka maembe mangapi?
6. Mnunuzi anataka kununua mafungu mangapi ya nyanya?
7. Mnunuzi ananunua kilo moja ya sukari kwa faranga ngapi?
8. Mnunuzi ananunua chumvi kwa faranga ngapi?
9. Fungu moja la nyanya analinunua kwa faranga ngapi?
10. Muuzaji anamwekea mnunuzi bidhaa wapi?

***Zoezi la kuigiza***

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, igizeni mazungumzo yaliyo hapo juu kati ya muuzaji na mnunuzi.

***Zoezi la imla***

Funga kitabu chako. Katika daftari lako, andika kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno utakavyosomewa na mwalimu wako.

## B. Msamiati wa uuzaji na ununuzi

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, tafuteni maneno mapya katika mazungumzo mliyosoma. Yatoleeni maana kulingana na matumizi yake katika mazungumzo. Tumia kamusi ya Kiswahili pale panapohitajika.

***Zoezi la 1***

**Soma sentensi zifuatazo kisha utunge sentensi zako binafsi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari.**

1. <u>Bei</u> ya chumvi imepunguka siku hizi; kilo moja ni faranga mia moja.
2. Mutoni anauza vitu vingi kwa bei <u>rahisi</u> sana. Watu wengi wanapenda kununua kwake.
3. Kamali anafanya <u>biashara</u> katika soko la Kimironko. Yeye anauza madaftari, kalamu, viatu, shati na kadhalika.
4. Baba yangu amenipa faranga mia tatu. Mimi ninaenda <u>kununua</u>

kalamu, penseli na madaftari.

5. Angalia juu ya meza hii; mama ametuwekea mkate mmoja.

6. Shati hili linauzwa kwa bei ghali sana. Muuzaji ananiambia nimpe faranga elfu tatu.

7. Ninataka kununua mafungu mawili ya nyanya. Kila fungu ni faranga hamsini.

8. Bei ya mafuta ya kupikia imepanda. Lita moja ni faranga elfu moja na mia tano.

9. Gasana anapunguza bei ya maharagwe. Kilo moja anauza kwa faranga mia mbili.

10. Katika soko la Muhanga kunapatikana vitu vingi sana kwa bei rahisi.

11. Kila wiki ananunua kilo tatu za mchele katika duka la Bigirimana. Yeye ni mteja wake.

12. Sisi tuko tayari kutoka sasa hivi; njoo twende pamoja.

13. Pesa ni za aina tofauti: nchini Rwanda tunatumia faranga na nchini Uganda, wanatumia shilingi.

14. Ninaweka nyanya katika mkoba mzuri. Mimi ninatoka sokoni na mkoba wangu.

### *Zoezi la 2*

**Kamilisha sentensi zinazofuata kwa kutumia moja kati ya maneno yaliyo kwenye mabano.**

**Mfano:** Baba yangu ana koti zuri. Yeye amenunua koti hilo kwa ________ (bei/shule) ghali sana.

**Jibu:** Baba yangu ana koti zuri. Yeye amenunua koti hilo kwa **bei** ghali sana.

1. Kaka yangu ________ (anauza/ananunua) magari mjini Kigali. Watu wengi wananunua kwake magari mazuri ya aina ya Nissan.

2. Muuzaji huyu ameleta ________ (sabuni/matunda) mengi. Yeye anauza maembe, ndizi, mananasi na machungwa.

3. Muuzaji anaweka vitu vya ________ (mwalimu/wateja) wake katika ________ (mikoba/madarasa) mizuri.
4. Mjini Musanze kuna ________ (soko/vitabu) la matunda mengi sana.
5. Mwanamke huyu ana ________ (pesa/masomo) nyingi. Yeye ni mfanyabiashara.
6. Kuna watu ________ (mmoja/wengi) wanaonunua viazi vitamu.
7. Mukamana ni ________ (mteja/mwalimu) wa kaka yangu. Kila siku, yeye ananunua vitu vingi katika duka lake.
8. Muuzaji huyu ________ (amepunguza/amepandisha) bei ya kilo moja ya vitunguu kutoka faranga mia moja hadi faranga hamsini.
9. Mchele umekosekana mjini Huye na bei yake________ (imepanda/imepunguka) hadi mia tisa kwa kilo moja.
10. Mama yangu ananituma sokoni. Mimi ninaenda sokoni kununua ________ (mafungu/kalamu) mawili ya nyanya.

## C. Kuhesabu tarakimu

### Soma kwa usahihi tarakimu zinazofuata:

| | | |
|---|---|---|
| 1 - moja | 2 - mbili | 3 - tatu |
| 4 - nne | 5 - tano | 6 - sita |
| 7 - saba | 8 - nane | 9 - tisa |
| 10 - kumi | 11 - kumi na moja | 12 - kumi na mbili |
| 13 - kumi na tatu | 14 - kumi na nne | 15 - kumi na tano |
| 16 - kumi na sita | 17 - kumi na saba | 18 - kumi na nane |
| 19 - kumi na tisa | 20 - ishirini | 21 - ishirini na moja |
| 22 - ishirini na mbili | 29 - ishirini na tisa | 30 - thelathini |
| 40 - arubaini | 50 - hamsini | 60 - sitini |
| 70 - sabini | 80 - themanini | 90 - tisini |
| 100 - mia moja | 101 - mia moja na moja | 109 - mia moja na tisa |

| | | |
|---|---|---|
| 110 - mia moja na kumi | 112 - mia moja na kumi na mbili | 120 - mia moja na ishirini |
| 126 - mia moja na ishirini na sita | 130 - mia moja na thelathini | 140 - mia moja na arubaini |
| 150 - mia moja na hamsini | 160 - mia moja na sitini | 170 - mia moja na sabini |
| 180 - mia moja na themanini | 190 - mia moja na tisini | 200 - mia mbili |
| 300 - mia tatu | 400 - mia nne | 500 - mia tano |
| 600 - mia sita | 700 - mia saba | 800 - mia nane |
| 900 - mia tisa | 1000 - elfu moja | |

### *Zoezi la 1*

**Hesabu kuanzia moja hadi mia moja.**

### *Zoezi la 2*

**Andika tarakimu zinazofuata kwa maneno:**

99, 77, 219, 349, 440, 677, 798, 888, 933, 988, 88, 54, 255, 333, 506, 705, 832, 894, 967, 999

### *Zoezi la 3*

**Andika tarakimu hizi kwa nambari.**

| | |
|---|---|
| 1. sitini na tisa | 2. hamsini na tano |
| 3. sabini na saba | 4. themanini na nne |
| 5. tisini na tano | 6. mia moja na themanini na moja |
| 7. mia moja na arubaini na nne | 8. mia mbili na mbili |
| 9. mia mbili na sabini na tisa | 10. mia tatu na kumi na tisa |
| 11. mia nne na nne | 12. mia nne na arubaini na nne |
| 13. mia nne na themanini na tatu | 14. mia tano na hamsini na saba |
| 15. mia sita na sitini | 16. mia sita na thelathini na tatu |
| 17. mia sita sitini na saba | 18. mia nane na themanini na nne |

| | |
|---|---|
| 19. mia tisa na sitini na sita | 20. mia tisa na tisini na tisa |

## D. Vipimo na matumizi yake katika hesabu

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni kifungu kifuatacho kuhusu vipimo mbalimbali na matumizi yake katika hesabu.**

Neza ni mtoto mtiifu na mwenye bidii. Jumamosi aliamka mapema na kumsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani. Alipomaliza kusafisha vyombo alitumwa sokoni. Soko lao lina umbali wa kilometa moja kutoka nyumbani kwao. Mamake Neza alimwandikia orodha ya bidhaa za kununua sokoni. Alimwagiza Neza anunue: kilo moja na nusu ya sukari, lita tatu za mafuta ya kupikia, gramu mia nne za nyama, galoni moja ya maziwa, mafungu mawili ya nyanya, fungu moja la vitunguu, kilo mbili za mchele, mililita mia tano ya soda ya fanta, pakiti moja ya chumvi na mkate mmoja.

Neza alichukua mkoba wake na kufululiza moja kwa moja hadi sokoni. Alinunua vitu vyote alivyoagizwa na mamake. Alitafuta mwendeshaji pikipiki mmoja ambaye alimbeba hadi nyumbani. Neza alipofika nyumbani, mamake alikagua bidhaa zote alizokuwa amenunua. Neza hakuwa amesahau chochote. Mamake alifurahi sana.

### *Zoezi la ufahamu*

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, jibu maswali yafuatayo katika madaftari yenu.

1. Neza alitumwa sokoni baada ya kufanya nini?
2. Neza alitumwa sokoni kununua kiasi gani cha mafuta ya kupikia na mchele?
3. Neza alitumwa kununua galoni moja ya nini?
4. Sokoni kwa kina Neza ni umbali upi kutoka nyumbani kwao?
5. Mamake Neza alimtuma Neza akanunue kiasi gani cha soda?

### Maelezo muhimu

Kipimo ni kiasi, kimo au kadiri. Kuna vipimo vya aina tofauti kama ifuatavyo:

**i) Mifano ya vipimo vya umbali au urefu ni:**

- Kilometa (km)
- Meta (m)
- Sentimeta (sm)
- Milimeta (mm)

**ii) Mifano ya vipimo vya ujazo ni:**

- Lita (l)
- Mililita (ml)

**iii) Mifano ya vipimo vya tungamo ni:**

- Tani (tn)
- Kilogramu (kg)
- Gramu (g)
- Miligramu (mg)

***Zoezi***

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, soma tena kifungu kuhusu vipimo kisha mjibu maswali yafuatayo:

1. Kwa kurejelea vipimo vya umbali, taja mfano mmoja kutoka katika kifungu hicho.
2. Neza alitumwa bidhaa zipi zenye vipimo vya ujazo?
3. Taja bidhaa zenye vipimo vya tungamo ambazo Neza alitumwa kununua sokoni.

## E. Alama za hesabu

Katika hesabu, alama zifuatazo hutumika:

| Alama | Maana | Mfano | Maneno |
|---|---|---|---|
| + | jumlisha | 2+2=4 | Mbili jumlisha mbili ni sawasawa na nne. |
| - | toa | 8-3=5 | Nane toa tatu ni sawasawa na tano. |
| x | zidisha/mara | 2x3-6 | Mbili mara tatu ni sawasawa na sita. |
| / | gawanya | 4/2 | Nne gawanya kwa mbili ni sawasawa na mbili. |
| < | ndogo kuliko | 3<5 | Tatu ni ndogo kuliko tano. |
| > | kubwa kuliko | 8>4 | Nane ni kubwa kuliko nne. |

***Zoezi***

Andika kwa maneno:

a) 4+10 = 14

b) 15<17

c) 44/11 = 4

d) 10 x 10 = 100

e) 90>60

**BEI YA BIDHAA MUHIMU HAIFAI KUPANDISHWA**

## *Somo la Pili*

# Biashara Mbalimbali

**Tazama picha hizi:**





**Baada ya kutazama picha zilizo hapo juu, taja vitu unavyoviona katika picha hizo.**

**Mfano: Ninaona rafu zenye vitabu.**

### *Zoezi la kusoma*

**Soma kifungu cha habari kinachofuata kuhusu biashara za Mukamana na Muneza mjini Karongi.**

***(Wao wana maduka yao kando ya soko kubwa mjini Karongi. Wanafanya biashara zao kwa kupokea vizuri wateja wao. Wao wana tabia nzuri na watu wengi wanawapenda sana.)***

Mukamana ni mfanyabiashara mzuri. Yeye anafanya biashara ya kuuza bidhaa mbalimbali. Anauza vifaa vya shule: daftari, rula, vitabu vya kusoma na kalamu. Pia anauza penseli, karatasi, vifutio na chaki. Yeye huwapokea vizuri wateja wake. Yeye huwasimamia wafanyabiashara wengine mjini Karongi. Katika mkutano na wafanyabiashara wengine, yeye huwaomba wafanyabiashara wenzake kuheshimu wateja wao. Anawaomba pia waache kuwaibia na kuwanyang'anya wateja pesa zao. Watu wengi huko Karongi wanampenda sana. Wafanyabiashara wote wanampenda na kumheshimu sana.

Muneza ni mfanyabiashara mzuri pia mjini Karongi. Yeye anafanya biashara

ya kuuza bidhaa zinazohusiana na utamaduni wa Rwanda. Hupata faida ya faranga elfu tano kila siku. Yeye hupokea wateja elfu kumi kwa mwaka na biashara yake ina thamani kubwa. Wateja wake wanatoka katika nchi za Afrika ya Mashariki: Kenya, Tanzania, Uganda na Burundi. Yeye ana idhini ya kufanya biashara hiyo. Baadhi ya wateja wake wanazungumza Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ina dhima kubwa katika shughuli za kibiashara. Muneza hadharau wateja wake na biashara yake inastawi vizuri. Mtoto wake Muneza anasoma katika kidato cha sita katika shule ya sekondari ya Nyarusange. Mtoto wa Muneza anadhamiria kumaliza masomo yake na kuanzisha pia biashara yake mjini Kigali.

### *Zoezi la ufahamu*

***Soma tena kifungu cha habari kilicho hapo juu. Sasa jibu maswali yafuatayo kwa kuandika majibu yako katika daftari lako.***

1. Mukamana anafanya biashara yake wapi?
2. Msimamizi wa wafanyabiashara huko Karongi ni nani?
3. Msimamizi anawaomba wafanyabiashara wafanye nini?
4. Mukamana anafanya biashara ya aina gani?
5. Muneza anauza nini huko Karongi?
6. Muneza anapata faida gani katika biashara yake?
7. Wengi wa wateja wa Muneza wanatoka wapi?
8. Wengi wa wateja wa Muneza wanazungumza lugha gani?
9. Mtoto wake Muneza anataka kufanya nini baada ya kumaliza masomo yake?

## A. Msamiati wa biashara

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, orodhesha msamiati mpya mlioupata katika kifungu hiki. Tafuteni maana za msamiati huo kwa kuzingatia matumizi yake katika kifungu mlichokisoma. Tumieni kamusi ya Kiswahili pale panapohitajika.

**Mfano:**

Mfanyabiashara: mtu ambaye anafanya shughuli za kununua na kuuza bidhaa ili kupata faida

### *Zoezi la 1*

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni sentensi zifuatazo. Baada ya kusoma, tungeni sentensi zenu kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari.**

1. Baadhi ya wafanyabiashara hawalipi ushuru. Wao wanapata adhabu kali kutoka kwa Taasisi ya Kukusanya Ushuru nchini.
2. Baba ana idhini ya kuanzisha kampuni ya kuuza magari mjini Kigali.
3. Usiwadharau walemavu kwa kupuuza uwezo wao. Wengi wao wanafanya biashara na kupata pesa nyingi sana.
4. Wakristo na Waislamu wote wanapaswa kuacha kufanya dhambi. Ni lazima wote watii amri za Mungu.
5. Dhima ya kujua kuhesabu ni kufanya biashara na kutajirika.
6. Mama yangu ana nyumba nzuri mjini Karongi. Nyumba yake ina thamani kubwa.
7. Mimi ninauza bidhaa mbalimbali: viatu vya aina tofauti na mavazi mbalimbali.
8. Mtoto wangu anadhamiria kuwa dereva. Yeye anasoma masomo ya kuendesha magari.
9. Gatera ameshikwa na polisi kwa kosa la kunyang'anya watu kwa kuwaibia pesa zao.
10. Wanyarwanda wana utamaduni mzuri: kusalimiana, kusaidiana, kushirikiana na kuheshimiana.

### *Zoezi la 2*

**Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia moja kati ya maneno yaliyo kwenye mabano.**

**Mfano:** Nyumba hii ina _________ (dhambi/thamani) kubwa. Mwenye nyumba hii anataka kuiuza kwa faranga nyingi sana.

**Jibu:** Nyumba hii ina **thamani** kubwa. Mwenye nyumba hii anataka

kuiuza kwa faranga nyingi sana.

1. Katika mji huu kuna ________ (biashara/somo) ya kuuza bidhaa za aina nyingi.
2. Jiepushe na kufanya ________ (idhini/dhambi) kwa kunyang'anya watu wasiojiweza.
3. Wanafunzi wote ________ (wanadhamiria/wanadharau) kupata alama nzuri katika somo la Kiswahili.
4. Wafanyabiashara wabaya ________ (wanaheshimu/wanadharau) wateja wao.
5. Yeye ana ________ (idhini/shule) ya kuanzisha shule ya sekondari kule kijijini Bugarama.
6. Shangazi yangu ana ________ (duka/gari) la mavazi mjini Muhanga. Yeye anapata faida kubwa.
7. Rais wa Jamhuri ya Rwanda anaomba Wanyarwanda kudumisha amani ili uchumi uweze ________ (kudhamiria/kustawi) vizuri.
8. Kiswahili kina ________ (dhima/somo) kubwa katika mawasiliano. Kinatumika sana katika shughuli za kibiashara Afrika ya Mashariki.
9. Utamaduni wa Wanyarwanda una ________ (thamani/idhini) kubwa na unavuta wageni wengi wanaokuja nchini.
10. Acha ________ (kusaidia/kunyang'anya) watu pesa zao. Sheria ya Rwanda inaweza kukupa adhabu kali.

### *Zoezi la majadiliano*

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadilianeni kuhusu 'tabia za mfanyabiashara mzuri'. Baada ya majadiliano, jitokeze mbele ya darasa na kuwaelezea wenzenu.

### *Zoezi la kujieleza*

Eleza wenzako kazi unayodhamiria kufanya baada ya kumaliza masomo yako.

## B. Tarakimu

**Soma kwa usahihi tarakimu hizi:**

| | |
|---|---|
| 1000 : elfu moja | 1001 : elfu moja na moja |
| 1010 : elfu moja na kumi | 1014 : elfu moja na kumi na nne |
| 1020 : elfu moja na ishirini | 1026 : elfu moja na ishirini na sita |
| 1030 : elfu moja na thelathini | 1039 : elfu moja na thelathini na tisa |
| 1040 : elfu moja na arubaini | 1050 : elfu moja na hamsini |
| 2000 : elfu mbili | 3000 : elfu tatu |
| 4000 : elfu nne | 5000 : elfu tano |
| 6000 : elfu sita | 7000 : elfu saba |
| 8000 : elfu nane | 9000 : elfu tisa |
| 10000 : elfu kumi | |

### *Zoezi la 1*

**Andika tarakimu hizi kwa kutumia maneno.**

| | | |
|---|---|---|
| 1. 1666 | 2. 2021 | 3. 2095 |
| 4. 6961 | 5. 7658 | 6. 5219 |
| 7. 1236 | 8. 1748 | 9. 2036 |
| 10. 2569 | 11. 8369 | 12. 6428 |
| 13. 4765 | 14. 1360 | 15. 1469 |
| 16. 2070 | 17. 3348 | 18. 9612 |
| 19. 5974 | 20. 3973 | |

### *Zoezi la 2*

**Kwa ushirikiano na wanafunzi wenzako watatu, andikeni tarakimu hizi kwa nambari.**

1. Elfu tatu mia tano na hamsini na tano
2. Elfu saba mia tisa na tisini na tatu

3. Elfu sita na themanini na mbili
4. Elfu nne na arubaini na nne
5. Elfu mbili mia mbili na mbili
6. Elfu tatu na thelathini na tisa
7. Elfu nne na themanini na nane
8. Elfu sita mia tisa na tisini na tisa
9. Elfu tano mia saba sabini na mbili
10. Elfu tisa mia tisa themanini na nne

**Maelezo muhimu**

**Tarakimu ni alama ya hesabu ambayo hutumiwa kuonyesha idadi; nambari**

## C. Kusikiliza na kuzungumza

### i) Soma maneno haya kwa usahihi. Tofautisha herufi *th* na *dh*.

| | |
|---|---|
| Thelathini | Bidhaa |
| Themanini | Dhamiria |
| Thibitisha | Dharau |
| Thamani | Dhambi |
| Tathmini | Dhima |

### ii) Soma kwa usahihi maneno haya. Tofautisha herufi *d/* na *dh*.

| | |
|---|---|
| Dada | Dhaifu |
| Debe | Dhehebu |
| Dini | Idhini |
| Duka | Dhulumu |
| Dari | Dhambi |
| Dawa | Dhati |
| Daftari | Tafadhali |

### iii) Soma kwa usahihi maneno haya. Tofautisha herufi t na th.

| | |
|---|---|
| Tia | Thibiti |
| Tibu | Thibitisha |
| Tiketi | Theluthi |
| Tamaa | Thamani |
| Kitanda | Thamini |
| Mti | Thibitisho |
| Teua | Themanini |

### *Zoezi la imla*

Funga kitabu chako. Katika daftari lako, andika kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno utakavyosomewa na mwalimu wako.

Somo la Tatu

# Mazingira ya Sokoni

**Tazama picha hii:**



Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, elezeni mnachoona katika picha iliyo hapo juu.

Mfano: Mimi ninaona machungwa.

## *Zoezi la kusoma*

**Soma kwa makini kifungu cha habari kinachofuata kuhusu 'Biashara ya mama yangu'.**

*(Mama yangu anafanya biashara sokoni Nyamasheke na anatupenda sana kama watoto wake. Yeye anafanya biashara yake vizuri. Anapata faida kubwa na kutunza familia yake vizuri.)*

Mimi ninaitwa Mugenzi. Mama hurudi nyumbani jioni na kutuamkia wote kwa kutuuliza tulivyoshinda mchana. Mimi na ndugu zangu tunampenda sana mama. Kila jioni, yeye hutuletea sambusa tatu, mkate mmoja na machungwa mawili. Pia hutuletea mapera manne, ndizi mbili, nanasi moja na mapapai

mawili. Sisi sote nyumbani hula nanasi, mkate na papai lakini mimi ninapenda sana sambusa. Dada yangu Mukamusoni na kaka yangu Iradukunda wanapenda machungwa na mapera. Mimi huchukua sambusa moja na wao huchukua sambusa mbili, kila mmoja. Mimi sipendi kula machungwa. Dada yangu na kaka yangu hula machungwa mawili nami hula pera moja.

Wakati wa kulala, mimi na Iradukunda hulala juu ya kitanda kimoja. Dadangu hulala pia juu ya kitanda chake. Nyumbani tuna vitanda vitano lakini vitanda viwili ni vya wageni. Asubuhi, mama hurudi sokoni na kupanga vizuri bidhaa zake. Juu ya meza moja huweka mafungu kumi na matano ya vitunguu. Pia huweka mafungu kumi na mawili ya nyanya. Katika fungu moja la vitunguu, mama huweka vitunguu vitano. Anauza fungu moja kwa faranga mia moja. Juu ya meza nyingine, mama hutandaza mafungu saba ya ndimu. Pia huweka mafungu matano ya mapera na maparachichi mengi. Mama huuza parachichi moja kwa faranga thelathini. Kwa siku moja mama anaweza kuuza maparachichi ishirini na manne.

## A. Ufahamu

**Soma tena kifungu cha habari kilicho hapo juu kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Mama ya Mugenzi anafanyia biashara yake wapi?
2. Yeye hurudi nyumbani wakati gani?
3. Yeye huleta nini nyumbani?
4. Mama huuza parachichi moja kwa faranga ngapi?
5. Nyumbani kuna vitanda vingapi?
6. Vitanda vya wageni ni vingapi?
7. Mama huleta mikate mingapi?
8. Mama huleta mananasi mangapi?
9. Katika fungu la vitunguu, mama huweka vitunguu vingapi?
10. Mugenzi ana ndugu wangapi?

## B. Msamiati wa sokoni

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, orodhesha msamiati mpya mliokumbana nao katika kifungu hiki. Tafuteni maana za msamiati huo kwa kuzingatia matumizi yake katika kifungu mlichokisoma. Tumieni kamusi ya



Kiswahili pale panapohitajika.

**Mfano:**

Parachichi: tunda ambalo lina kokwa ndani na lenye nyama ya kijani

### *Zoezi la 1*

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, husisheni majina yaliyopangwa hapo chini na picha zifuatazo.**

| | | |
|---|---|---|
|  **(a)** |  **(b)** |  **(c)** |
|  **(d)** |  **(e)** |  **(f)** |
|  **(g)** |  **(h)** |  **(i)** |

| | |
|---|---|
|  (j) |  (k) |

1. Embe    2. Mkate    3. Viatu    4. Nanasi

5. Ndizi    6. Nyanya    7. parachichi    8.Viazi vitamu

9. Viazi mbatata    10. Unga    11. Tufaha

**Mfano:** **1** → **(e)**

**Embe** → **(e)**

## C. Matumizi ya lugha ya sokoni

Soma sentensi zifuatazo kisha ufanye zoezi linalofuata.

11. Mama anarudi nyumbani na **fungu moja** la vitunguu. Mama anarudi nyumbani na **ma**fungu **ma**ngapi?
12. **Kitunguu kimoja** anakinunua faranga ishirini. Kitunguu kimoja ni faranga ngapi?
13. Mama akirudi nyumbani analeta sambusa tatu. Mama akirudi nyumbani analeta sambusa ngapi?
14. Mama anauza **matunda mengi** sokoni. Mama anauza **ma**tunda **ma**ngapi sokoni?

### *Zoezi la 1*

**Kwa kuzingatia sentensi ulizosoma hapo juu, uliza maswali mengine kwa kutumia kivumishi '*-ngapi*'.**

**Mfano:** Shule yetu ina walimu wawili wa Kiswahili.

**Jibu:** Shule yetu ina walimu wangapi wa Kiswahili?

1. Watoto hawa wanakula pamoja mapera **matatu**.

2. Wanyarwanda **wengi** wametoa mchango wao katika akiba ya kujiendeleza ya AGACIRO.
3. Mwanafunzi mbaya amepoteza vitabu **viwili**.
4. Baba amepanda minanasi **mingi**.
5. Nyumbani tuna wageni **watano.**
6. Darasa letu lina wanafunzi **ishirini na watano**.
7. Mamangu amenunua nyumba **moja**.
8. Mkulima huyu ana faranga **nyingi** katika Benki ya Kigali.
9. Mimi ninapeleka faranga zangu **elfu kumi** katika chama cha ushirika *UMURENGE SACCO TWITEZIMBERE.*
10. Wanaume **wengi** wanaelewa umuhimu wa usawa wa kijinsia.

**Tafakari:**
Kivumishi ***'-ngapi'*** kinatumiwa kuulizia swali kuhusu idadi ya watu au vitu vinavyotajwa au kuzungumziwa.

**Mfano:** Mimi nina machungwa ***ma***wili. Mimi nina **ma**chungwa **mangapi**?

### *Zoezi la 2*

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tungeni sentensi kumi kuonyesha matumizi ya neno ***'-ngapi'.*** Tangulia na sentensi yenye kutumia **idadi** na kuendelea na sentensi inayouliza **swali** kuhusu idadi.

**Mfano:** **a)** Wafanyabiashara wadogo wanalipa kodi ya faranga **elfu sitini** kwa mwaka.

**b)** Wafanyabiashara wadogo wanalipa kodi ya faranga **ngapi** kwa mwaka?

## D. Sarufi: Vivumishi vya idadi

### Shughuli za makundi

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, someni tena kifungu cha habari kilicho hapo juu ('Biashara ya mama yangu'). Andika vifungu vya maneno vyenye majina pamoja na idadi zinazoelezea kiasi cha vitu vinavyozungumziwa.

### *Zoezi la utafiti*

**Jaribuni kuchunguza jinsi kila kifungu kinavyojitokeza kwa kuonyesha sifa za kila kifungu.**

**Mfano**: Mkate mmoja

**Jina:** Mkate

**Idadi:** Mkate ni **mmoja**

### *Zoezi la 1*

**Someni sentensi zinazofuata kwa kudhihirisha sifa za vifungu vilivyopigiwa mstari.**

1. <u>Mtoto mmoja</u> anasoma kitabu kimoja.
2. <u>Watoto wawili</u> wanasoma vitabu viwili.
3. <u>Watoto watatu</u> wanasoma vitabu vitatu.
4. <u>Watoto wanne</u> wanasoma vitabu vinne.
5. <u>Watoto watano</u> wanasoma vitabu vitano.
6. <u>Watoto sita</u> wanasoma vitabu sita.
7. <u>Watoto saba</u> wanasoma vitabu saba.
8. <u>Watoto wanan</u>e wanasoma vitabu vinane.
9. <u>Watoto tisa</u> wanasoma vitabu tisa.
10. <u>Watoto kumi</u> wanasoma vitabu kumi.
11. <u>Watoto kumi na mmoja</u> wanasoma vitabu kumi na kimoja.
12. <u>Watoto kumi na wawili</u> wanasoma vitabu kumi na viwili

### *Zoezi la 2*

**Kwa kuzingatia mifano ya sentensi zilizo hapo juu, tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

*moja, mbili, tano, tatu, nane, tisa, saba, nne, sita, kumi*

**Tafakari:**

Maneno yanayoelezea idadi ya vitu vinavyotajwa na jina yanaitwa vivumishi vya idadi. Vivumishi vya idadi vinachukua viambishi vinavyofanana na viambishi vya majina.

**Mfano:** ***Ma***chungwa ***ma***wili.

**Lakini:** Idadi ***sita, saba, tisa*** na ***kumi*** hazichukui viambishi hivyo.

**Mfano:** ***Ma***chungwa ***sita*** ***yameoza.***

*Machungwa tisa yameuzwa.*

*Machungwa kumi yataliwa.*

### *Zoezi la 3*

**Andika sentensi zinazofuata kwa kutumia maneno katika idadi zilizoonyeshwa kwa nambari.**

**Mfano:** Hospitalini kuna wagonjwa ***123***.

**Jibu:** Hospitalini kuna wagonjwa **mia moja na ishirini na watatu.**

1. Mugabo anauza vitanda ***19***.
2. Mama yangu ameuza mafungu ***33*** ya nyanya.
3. Baba yangu ana magari ***2***.
4. Wanafunzi ***2351*** wanasoma Kiswahili.
5. Shule yangu ina majengo ***7*** mazuri.
6. Watoto ***6978*** wamefaulu mitihani yote.
7. Mkulima amepanda miti ***1531.*** Yeye anatunza vizuri miti yake.
8. Mfanyabiashara mzuri ameuza viatu ***3678*** katika mwezi huu.
9. Nyumba ya baba yangu ina milango ***3*** na madirisha ***4***.
10. Walimu ***5*** wa darasa langu wanafundisha masomo ***10***.

### *Zoezi la Imla*

**Funga kitabu chako, kisha katika daftari lako, andika kwa usahihi sentensi utakazosomewa na mwalimu wako**

## Faharasa

**Angalia:** tazama

**Bei:** kiasi cha fedha kinachotumiwa kununua na kuuza kitu

**Biashara:** kazi ya kununua na kuuza bidhaa, uchuuzi

**Dari:** sakafu ya juu ya nyumba

**Dawa:** kitu anachopewa mgonjwa ili apone

**Debe:** chombo cha bati cha kutilia vitu vya majimaji

**Dhaifu:** kitu chenye ubaya, kilichodhoofika, kisicho na nguvu

**Dhambi:** kosa linalovunja sheria za dini

**Dhamiria:** taka kufanya jambo fulani, nuia, fikiria, kusudia kufanya jambo

**Dharau:** vunjia mtu heshima

**Dharura:** shughuli au jambo la haraka bila kupangwa

**Dhati:** moyo usiositasita

**Dhehebu:** kikundi cha dini fulani

**Dhima:** wajibu mkubwa pamoja na uwezo wa kufanya jambo, kazi ya mtu

**Dhulumu:** onea, fanya isiyo haki, nyang'anya

**Fungu:** rundo dogo la vitu

**Ghali:** bei kubwa, bei isiyo rahisi

**Idhini:** ruhusa

**Mfanyabiashara:** mtu anayefanya kazi ya biashara, mchuuzi

**Mteja:** mtu anayeenda sokoni au dukani ili auziwe bidhaa

**Nunua:** toa fedha ili kupata kitu kinachouzwa

**Panda:** enda juu

**Pesa:** sarafu na noti zinazotumiwa katika nchi fulani kama fedha ili kununulia bidhaa

**Punguza:** fanya bei iwe ya chini zaidi

**Rahisi:** kitu chenye bei ya chini

**Tamaa:** hamu kubwa ya kufanya kitu

**Tathmini:** angalia kitu kwa undani ili kuangalia ubora wake

**Tayari:** kwa hali kamili au ya kujiandaa kufanya kitu

**Thamani:** ubora wa kitu kutokana na kuhitajika na watu wengi, gharama ya kitu, umuhimu mkubwa wa kitu

**Thamini:** tia bei ya kitu, heshimu

**Theluthi:** sehemu moja ya kitu kilichogawanywa katika sehemu tatu zilizo sawa

**Thibiti:** kuwa ya kweli

**Thibitisha:** hakikisha

**Tia:** ingiza kitu ndani ya kitu kingine

**Tibu:** patia mtu dawa ili aweze kupona maradhi

**Tiketi:** karatasi maalum anayopewa mtu baada ya kulipa fedha ili aweze kusafiri au kuingia mahali fulani

**Tunda:** zao la mmea, kama vile: chungwa, fenesi, nanasi, papai, ndizi, tufaha, zabibu

**Uza:** toa kitu kwa ajili ya kupewa fedha

**NI VIZURI KUHIFADHI PESA ZETU BENKINI**

**Mada Kuu:**

# Matumizi ya Lugha Katika Mazingira Mbalimbali

**Mada Ndogo:**

## Matumizi ya Msamiati Kuhusu Usafi wa Mwili

| | |
|---|---|
| **Somo la Kwanza:** | i) Maana ya usafi wa mwili |
| | ii) Magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa usafi |
| **Somo la Pili:** | Msamiati wa mwili na mazingira |
| **Somo la Tatu:** | Usafi wa mwili na mazingira |

# Maana ya Usafi wa Mwili

**Tazama michoro ifuatayo kwa makini:**


1.


2.


3.


4.


5.


6.

**Baada ya kuangalia michoro iliyo hapo juu, unaweza:**

a) Kusema ulichokiona?

b) Kueleza watu hawa wanafanya nini?

c) Kuhusisha picha na shughuli kama hizo nyumbani?

**Linganisha majibu yako na mazungumzo yafuatayo:**

**Mwalimu:** Mahoro!

**Mwanafunzi:** Abee mwalimu.

**Mwalimu:** Kwa nini hujachana nywele na kuzikata kucha zako?

**Mwanafunzi:** Sina kichanuo. Nitazikata kucha zangu kesho. Pia, nitakumbuka kunawa mikono yangu kwa maji safi na sabuni.



| | |
|---|---|
| | Samahani mwalimu. |
| **Mwalimu:** | Sawa basi. Pia, jaribu kuzinyoa nywele hizo. |
| **Mwanafunzi:** | Sawa mwalimu. |
| **Mwalimu:** | Umepiga mswaki? |
| **Mwanafunzi:** | Ndiyo mwalimu. Pia, nimeoga kwa sabuni. Nilizifua nguo zangu na kakangu akazipiga pasi. |
| **Mwalimu:** | Unastahili kufahamu kuwa usafi wa mwili ni muhimu. |

## *Zoezi la kuigiza*

**Kwa ushirikiano na wanafunzi wenzako, igizeni mbele ya darasa lenu mazungumzo kati ya mwalimu na mwanafunzi.**

## *Zoezi la matamshi*

**Tamka kwa ufasaha maneno yaliyoambatanishwa na michoro ifuatayo:**

| | |
|---|---|
|  Mswaki |  Kichanuo |
|  Sabuni |  Nyoa |
|  Oga | |

## A. Kusikiliza na kuzungumza

**Soma kimyakimya msamiati ufuatao unaohusu usafi wa mwili.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Nawa mkono wako. | Naweni mikono yenu. |
| Chana nywele zako. | Chaneni nywele zenu. |
| Oga mwili wako. | Ogeni miili yenu. |
| Kata ukucha wako. | Kateni kucha zenu. |

**Maelezo muhimu**

**Kila mtu anafaa kuzingatia usafi wa mwili wake wote kuanzia kichwani hadi unyayoni.**

***Zoezi la kuigiza***

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, eleza jinsi unavyousafisha mwili wako. Taja shughuli zote za usafi ambazo wewe huzingatia.**


**Baada ya kusoma msamiati na sentensi fupi zilizo hapo juu kuhusu usafi wa mwili, unaweza kueleza:**

a) Ni sehemu gani za mwili zilizotajwa katika sentensi fupi zilizo hapo juu?

b) Eleza umuhimu wa sehemu hizo za mwili kwa binadamu.

## B. Msamiati wa usafi wa mazingira

**Tazama mchoro ufuatao kisha usome maelezo ya msamiati ulioorodheshwa baada ya mchoro huu.**




1. **Usafi:** Hali ya kutokuwa na uchafu. Kwa mfano; kuokota takataka
2. **Kuoga:** Kuondoa uchafu mwilini kwa kutumia maji na sabuni
3. **Sabuni:** Mchanganyiko wa mafuta asilia na madini na hutumiwa kuondoa uchafu mwilini au katika nguo, nyumba na vyombo
4. **Kichanuo:** Kitu chenye njiti nyingi kinachotumiwa kuchana nywele. Pia; kichana
5. **Nywele:** Umoja wa unywele; singa zinazoota kwenye mwili hasa kichwani
6. **Nyoa:** Ondoa nywele mwilini, hasa kwenye kichwa kwa kutumia kitu chenye ncha kali
7. **Mswaki:** Kijiti ama brashi ya kusugulia meno
8. **Nguo:** Chochote cha kujisetiri. Kwa mfano; kitambaa, rinda, shati
9. **Kichwa:** Sehemu ya mwili inayoshikana na shingo ambayo ina macho, pua, mdomo, ubongo na kadhalika.
10. **Mwili:** Umbo zima la mtu, kutoka kichwani hadi miguuni.

### *Zoezi la 1*

**Jaza mapengo yafuatayo kwa kutumia msamiati ufuatao:**

kichwani, mkono, mswaki, sabuni, nywele, mwili

**Mfano:** Ni sehemu kuanzia kichwani hadi miguuni ____________.

**Jibu:** Mwili

1. Nakitumia kushika na kufanya kazi _____________.
2. Macho, mdomo, pua na nywele vipo hapo _____________.
3. Ni mchanganyiko wa vitu na hutumika kuoga na kuosha ____________.
4. Nikikosa kukitumia hufanya mdomo unuke _____________.
5. Nikikosa kutengeneza naambiwa mimi ni mchafu na nimebeba msitu kichwani _____________.

### Zoezi la 2

Kamilisha maswali yafuatayo kwa msaada wa wanafunzi wenzako.

**Mfano:** Asubuhi tunapiga? _____________ (sabuni, mswaki)

**Jibu:** Mswaki

1. Kunyoa? ___________. (nywele, mikono)
2. Unaoga? ___________. (mwili, mswaki)
3. Kuchana? ___________. (nywele, kichwa)
4. Kata? ___________. (kucha, mikono)
5. Fua? ___________. (mwili, nguo)

## C. Wimbo kuhusu sehemu za mwili wa binadamu

**Tazama mchoro ambao unahusu mwili wa binadamu tena kwa makini. Sasa soma wimbo ufuatao kuhusu sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu kwa makini. Baada ya kusoma na kuelewa, jibu**

maswali yanayofuata kwa ushirikiano na wenzako.

**Wimbo**

*Miguu ya kutembea*

*Mikono ya kukamatia*

*Macho ya kuonea*

*Kichwa cha kufikiria*

*Pua ya kupumulia*

*Mdomo wa kulia*

*Kifua nguvu yangu*

*Mabega ya kubebea*

*Tumbo la kuhifadhi chakula*

*Mgongo wa kusimama*

*Nywele za kuzuia baridi*

*Masikio ya kusikia*

*Paja, miguuni*

*Kipaji usoni*

*Utosi kichwani*

*Kiwiko mkononi*

*Unyayo mguuni*

**Tathmini:** Waeleze wenzako wimbo huu unazungumzia nini.

### *Zoezi la ufahamu*

1. Kazi ya sikio ni ___________ sauti.
2. Kazi ya miguu ni ___________.
3. Kazi ya macho ni ___________.
4. Kazi ya nywele ni ___________.
5. Pua hufanya kazi ya ___________.
6. Mikono ina kazi ya ___________.
7. ___________ kinapatikana kichwani.
8. ___________ kinapatikana pamoja na mkono.
9. Kipaji kinapatikana kwenye ___________.
10. Unyayo unapatikana kwenye ___________.

### *Zoezi la mjadala*

**Kwa kuongozana nyinyi wenyewe, jadili faida ya kuoga mwili na hasara ya kukataa kuoga.**

## D. Sarufi

### Umoja na wingi wa viungo vya mwili

Tazama kiwiliwili cha binadamu kilicho hapo juu tena. Sasa soma kimyakimya viungo vifuatavyo vya mwili katika umoja na wingi.

| Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|
| 1. kichwa | vichwa | 2. kidole | vidole |
| 3. mkono | mikono | 4. ukucha | kucha |
| 5. jicho | macho | 6. unyayo | nyayo |
| 7. mguu | miguu | 8. pua | pua |
| 9. mwili | miili | 10. udevu | ndevu |
| 11. kwapa | makwapa | 12. kidevu | videvu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. kifua | vifua | 14. utosi | utosi |
| 15. kiuno | viuno | 16. kipaji | vipaji |
| 17. unywele | nywele | 18. utaya | taya |
| 19. sikio | masikio | 20. kiwiko | viwiko |
| 21. mdomo | midomo | 22. kinywa | vinywa |

### *Zoezi la 1*

**Katika daftari lako, andika maneno haya katika wingi.**

**Mfano:** Jicho

**Jibu:** Macho

1. Mkono
2. Kidole
3. Udevu
4. Kinywa
5. Mguu

### *Zoezi la 2*

**Katika daftari lako, andika maneno haya katika umoja.**

**Mfano:** Masikio - Sikio

1. Pua
2. Utosi
3. Nywele
4. Vifua
5. Midomo

**Mifano ya sentensi zenye sehemu za mwili katika umoja na wingi:**

| | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ninaoga **mwili**. | - | Tunaoga **miili**. |
| 2. | Ninaosha **mguu**. | - | Tunaosha **miguu**. |
| 3. | Ninanyoa **udevu**. | - | Tunanyoa **ndevu**. |

4. Ninachana **unywele**. - Tunachana **nywele**.
5. Ninapenga **pua**. - Tunapenga **pua**.
6. Ninanawa **mkono**. - Tunanawa **mikono**.

### *Zoezi la ubunifu*

**Tunga sentensi fupi fupi kisha uzisome mbele ya wanafunzi wenzako kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Kucha
2. Uso
3. Meno
4. Maji
5. Nguo

## E. Magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa usafi

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadili kuhusu magonjwa mbalimbali ambayo huwakumba binadamu ambayo husababishwa na ukosefu wa usafi.**

### Tathmini:

1. Taja magonjwa ambayo husababishwa na ukosefu wa usafi wa mwili wa binadamu.
2. Taja magonjwa ambayo husababishwa na ukosefu wa usafi wa mazingira anamoishi binadamu.

### Maelezo muhimu

**Magonjwa ni maradhi. Kuwa mgonjwa ni kuugua au kutokuwa na afya. Magonjwa huweza kusababishwa na viini, bakteria au hata virusi mbalimbali.**

### *Zoezi la utafiti*

**Tafiti kuhusu magonjwa ambayo husababishwa na ukosefu wa usafi mwilini. Yataje magonjwa hayo.**

**Baadhi ya magonjwa haya ni:**

1. **Malaria:** Huu ni ugonjwa unaosababishwa na mbu. Mazingira yenye maji yaliyotuama, nyasi ndefu huwa makao ya mbu ambao huzaana na kuishi humo.
2. **Kichocho:** Ugonjwa unaosababishwa na wadudu wanaoishi katika miili ya konokono. Mazingira yenye konokono wengi hupelekea ugonjwa huu kusambaa sana.
3. **Tauni:** Ugonjwa unaosababishwa na viroboto vya panya. Mazingira yasiyo safi huvutia panya wengi.
4. **Kipindupindu:** Ugonjwa wa kuendesha tumbo sana. Husababishwa na kula chakula kisicho safi au kunywa maji yasiyo safi.
5. **Keya:** Ugonjwa wa kupasukapasuka nyayo (miguu) hasa kwenye visigino. Husababishwa na kutoisafisha miguu vizuri au kutovaa viatu.
6. **Upele:** Ugonjwa wa kujikunakuna ngozi na kuwa na vipele vingi vingi mwilini. Aghalabu husababishwa na kuvaa nguo zisizo safi au kutooga mwili.
7. **Malale:** Husababishwa na kuumwa na mdudu aitwaye mbung'o. Mazingira yasiyo safi yanaweza kuwa makao ya wadudu hawa hatari.

***Zoezi***

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadili kuhusu magonjwa mengine ambayo yanasababishwa na ukosefu wa usafi wa mwili wa binadamu pamoja na mazingira anamoishi.**

**USAFI NI AFYA NA USAFI HUTUPATANISHA NA WATU WENGINE.**

# Msamiati wa Mwili na Mazingira

**Tazama michoro ifuatayo kwa makini na vitendo vinavyofanyika.**



## Tathmini

1. Michoro iliyo hapo juu inahusu nini?
2. Waeleze wanafunzi wenzako kinachoendelea kwenye michoro kuhusu:

    a) Afya ya mwili

    b) Magonjwa

## A. Kusikiliza na kuzungumza

**Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, someni mazungumzo yanayofuata. Linganisheni maoni yenu na yale ya vikundi vingine.**

**Kijana:** Hujambo daktari?

**Daktari:** Sijambo. U hali gani?

**Kijana:** Naugua. Tumbo linanisokota!

**Daktari:** Unakunywa maji safi?

**Kijana:** Ndiyo. Tena ya mvua.

**Daktari:** Unayachemsha maji hayo kwanza?

**Kijana:** La. Huwa sioni haja ya kuyachemsha. Ni safi kabisa.

Pia, kichwa kinaniwanga!

**Daktari:** Kwani una malaria?

**Kijana:** Sina uhakika. Labda ni homa ya matumbo.

**Daktari:** Ni bora nikupime. Je, unafyeka mazingira yako?

**Kijana:** La! Kuna mbu wengi.

**Daktari:** Ni muhimu kufyeka nyasi katika mazingira ya nyumbani. Pia, ufungue mitaro yote ya maji ili yasituame na kuwa makao ya mbu. Usijali nitakutibu.

**Kijana:** Asante daktari. Nitafuata maagizo yako.

**Daktari:** Karibu.

**Je, unadhani mazungumzo haya yanahusu nini?**

### *Zoezi la ufahamu*

**Soma tena mazungumzo kati ya Kijana na Daktari kisha ujibu maswali yafuatayo kwa ushirikiano na wanafunzi wenzako.**

1. Kijana anaugua nini? ______________
2. Daktari alimuuliza kijana iwapo anakunywa ____________.
3. Kijana hunywa maji ya ____________.

4. Ni vizuri ku ____________maji ya kunywa.
5. Mbu ni aina ya ____________.

### Tathmini

Mambo muhimu yaliyojitokeza katika mazungumzo baina ya Daktari na Kijana:

1. Tunafaa kufyeka nyasi zilizo karibu na makazi yetu.
2. Ni muhimu kuchemsha maji ya kunywa.
3. Malaria ni ugonjwa hatari.
4. Homa ya matumbo ni ugonjwa wa kuendesha tumbo.
5. Ni muhimu kuifungua mitaro ya maji ili maji yasituame na kuhifadhi mbu.
6. Mbu husababisha ugonjwa wa malaria.
7. Ni muhimu kila mara tunywe maji yaliyo safi.

### *Zoezi la mjadala*

Jadiliana na wenzako jinsi yaliyotajwa hapo juu yanahusiana na afya zetu na mazingira.

### *Zoezi la kuigiza*

Katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili, igizeni wahusika mbalimbali wa afya kama vile:

a) Muuzaji wa mboga/matunda na mnunuzi
b) Daktari na mgonjwa
c) Mshauri wa afya nyumbani
d) Mtu anayejenga nyumba

## B. Msamiati wa mwili na mazingira

**Soma msamiati ufuatao kwa sauti.**

| | |
|---|---|
| 1. Maji | 2. Malaria |
| 3. Homa | 4. Homa ya matumbo |
| 5. Mbu | 6. Fyeka |
| 7. Nyasi | 8. Daktari |
| 9. Mazingira | 10. Chemsha |
| 11. Kunywa | 12. Tibu |

***Zoezi la 1***

**Je, unaweza kuelezea maana ya baadhi ya maneno hayo? Basi waeleze wanafunzi wenzako. Zingatia jinsi maneno hayo yalivyotumika katika mazungumzo kati ya Daktari na Kijana.**

***Zoezi la 2***

**Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadili maana ya vifungu hivi.**

1. Tibu mgonjwa
2. Fyeka nyasi
3. Kunywa maji
4. Ua mbu
5. Chemsha maji

***Zoezi la ziada***

**Jibu maswali haya kwa kuchagua majibu sahihi kutoka kwenye mabano. Andika majibu yako kwenye daftari lako.**

1. Chagua kifungu chenye maradhi pekee.
    a) (Malaria, homa ya matumbo, kipindupindu)
    b) (Nyasi, malaria, homa ya matumbo, kipindupindu)
2. Mdudu anayeleta malaria ni ____________. (mbu, chawa)
3. Tunachemsha ____________. (maji, magonjwa)
4. Tunafyeka ____________. (nyasi, mbu)
5. Ni vitu vyote ambavyo vinatuzunguka. __________ (maji, mazingira)

*Zoezi la mjadala*

Jadiliana na wanafunzi wenzako kuhusu faida za kusafisha shule yenu.

## C. Sarufi

**Soma sentensi hizi zinazotumia viungo vya mwili na maradhi katika umoja na wingi.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Funza anang'ata mguu. | Funza wanang'ata miguu. |
| 2. Mbu anafyonza damu. | Mbu wanafyonza damu. |
| 3. Kichwa kinaniwanga. | Vichwa vinatuwanga. |
| 4. Tumbo linanisokota. | Matumbo yanatusokota. |
| 5. Kifua changu kina uchungu. | Vifua vyetu vina uchungu. |

*Zoezi la 1*

**Andika maneno haya katika wingi.**

1. Bega
2. Kiuno
3. Udevu
4. Kidole
5. Kichwa

*Zoezi la 2*

**Kwa kushirikiana na mwanafunzi mwenzako, andika maneno haya katika umoja.**

1. Meno
2. Mapaja
3. Vinywa
4. Pua
5. Ndevu

## D. Matamshi na tahajia bora

**1. Tamka kwa sauti maneno na sentensi zifuatazo mbele ya darasa lako.**

a) Chemsha maji
b) Fyeka nyasi
c) Tibu malaria
d) Fua nguo
e) Oga mwili

**2. Katika daftari lako, andika maneno yafuatayo kwa hati nzuri:**

a) Malaria
b) Kipindupindu
c) Kichocho
d) Kifua kikuu
e) Ukimwi
f) Homa ya matumbo
g) Funza
h) Mbu
i) Chawa
j) Kunguni

### *Zoezi la ziada*

**Kwa njia ya wimbo na uigizaji, tumia viungo vya mwili kukamilisha mahadhi ya wimbo huu.**

**Mfano:** Mimi ni kinywa. Kazi yangu ni ***kula***.

1. Mimi ni mguu. Kazi yangu ni _______________.
2. Mimi ni mkono. Kazi yangu ni _______________.
3. Mimi ni jicho. Kazi yangu ni _______________.
4. Mimi ni pua. Kazi yangu ni _______________.

**Sasa badilishaneni nafasi:**

a) Wewe ni kifua. Kazi yako ni _______________.
b) Wewe ni shingo. Kazi yako ni _______________.
c) Wewe ni wayo. Kazi yako ni _______________.
d) Wewe ni mgongo. Kazi yako ni _______________.


**Haya badilishaneni nafasi tena:**

i) Yeye ni kiwiko. Kazi yake ni _______________.
ii) Yeye ni nyonga. Kazi yake ni _______________.
iii) Yeye ni koromeo. Kazi yake ni _______________.
iv) Yeye ni kidole. Kazi yake ni _______________.

**Mazingira mabaya yanaathiri afya pamoja na tabia zetu**

# Usafi wa Mwili na Mazingira

### Tazama kwa makini michoro ifuatayo.

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |
| **1.** | **2.** | **3.** |

Baada ya kutazama kwa makini michoro iliyo hapo juu, waeleze wanafunzi wenzako unachokiona katika michoro hiyo. Je, unaweza kuhusisha michoro hiyo na hali ya kila siku katika jamii?

### Maelezo muhimu

Mazingira yoyote ni muhimu kwa binadamu; nyumbani, shuleni, kazini, siasa na afya.

### Tathmini

**Angalia michoro iliyo hapo juu kisha ujaribu kujibu maswali haya ya tathmini.**


a) Michoro hiyo inahusu nini?

b) Toa maoni yako kuhusu magonjwa yanayosababishwa na mazingira machafu.

**Maelezo muhimu**

Mazingira ni hali na vitu vinavyotuzunguka.

Tazama michoro ifuatayo kisha uilinganishe na maelezo yaliyo hapo chini.

| | |
|---|---|
| <br>**A.** | <br>**B.** |
| <br>**C.** | <br>**D.** |

A → Kichaka ni hifadhi ya wadudu hatari kwa binadamu.

B → Takataka zitupwe kwenye jaa.

C → Matumizi ya dawa za kulevya hudhuru afya.

D → Maji yaliyotuama husababisha magonjwa kama malaria na kipindupindu.

## A. Kuzikiliza na kuzungumza

Kwa ushirikiano na wanafunzi wenzako, tazama tena michoro ya mwanzoni mwa somo hili na ile iliyo hapo juu. Soma maelezo kuhusu michoro hiyo kwa kuzingatia:

1. Matamshi bora
2. Kusoma kwa sauti
3. Kusahihishana matamshi yasiyo sahihi

*Zoezi la mjadala*

**Je, kuna uhusiano wa mazingira, afya ya mwili na magonjwa? Jadili kwa ushirikiano na wanafunzi wenzako.**

## B. Msamiati wa usafi wa mwili na mazingira

**Shirikiana na wanafunzi wenzako kueleza unachojua kuhusu msamiati ufuatao:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mazingira | Mazingira |
| Maji machafu | Maji machafu |
| Kichocho | Kichocho |
| Mdudu | Wadudu |
| Nzi | Nzi |
| Takataka | Takataka |
| Mbu | Mbu |
| Funza | Funza |
| Malaria | Malaria |
| Mgonjwa | Wagonjwa |

**Matumizi katika sentensi.**

1. Usinywe maji machafu.
2. Baba atachoma takataka hizi.
3. Kaka anatumia dawa kuwaangamiza wadudu hawa.
4. Mbu husababisha ugonjwa wa malaria.
5. Tujitahidi kuzuia magonjwa.

**Zoezi la 1**

**Jaza mapengo yaliyo hapo chini kwa kuteua majibu sahihi baada ya kusoma swali kwa makini. Andika majibu kwenye daftari lako.**

1. Mazingira ni __________________ na __________________ vinavyotuzunguka.
2. Andika wingi wa 'mdudu' __________________.
3. Maji machafu yanaleta __________________.
4. Je, funza ni mdudu ama ni uchafu?
5. Chagua kauli ambayo ni sahihi kati ya hizi:

   a) Ugonjwa unaua.

   b) Ugonjwa ni afya.

**Zoezi la 2**

**Tunga sentensi kwa kutumia msamiati ufuatao huku ukizingatia maana yake.**

*mazingira, magonjwa, wadudu, funza, maji, takataka*

**Mfano:** Ondoa takataka nyumbani.

## C. Msamiati wa magonjwa

**Soma maneno yafuatayo kwa makini. Maneno haya ni majina ya magonjwa mbalimbali.**

1. Kipindupindu
2. Kichocho
3. Malaria
3. Homa ya matumbo
4. UKIMWI
5. Kifua kikuu
6. Kisonono
7. Funza

**Tathmini**

1. Je, umegundua nini kuhusu magonjwa hayo?
2. Je, unaweza kueleza kwa nini magonjwa ya UKIMWI na kisonono

yameorodheshwa hapo?

**Maelezo muhimu**

- Magonjwa hayo yanatokana na mazingira machafu.
- Tabia mbaya ya kibinadamu inaweza kuharibu uhusiano na mazingira ya kijamii. Haya yanawezekana kwa kuambukizana magonjwa na kuibua uadui na pia kusababisha vifo.

### *Zoezi la ufahamu*

**Kwa ushirikiano na wanafunzi wenzako, jibu maswali yafuatayo.**

1. Ni magonjwa mangapi yametajwa hapo juu?
2. Malaria husababishwa na wadudu gani?
3. Funza hukaa wapi?
4. Kifua kikuu ni ugonjwa wa aina gani?
5. Ugonjwa wa kuendesha sana na kupoteza maji unaitwaje?

### *Zoezi la mjadala*

Kwa ushirikiano na wenzako, jadili kuhusu 'hatari za mazingira machafu'.

## D. Sarufi

### Umoja na wingi

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, someni maneno yafuatayo. Mmoja asome neno katika umoja huku mwingine akisoma neno hilo katika wingi.**

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| 1. Mazingira | - | Mazingira |
| 2. Mgonjwa | - | Wagonjwa |
| 3. Dawa ya kulevya | - | Dawa za kulevya |
| 4. Uchafu | - | Uchafu |

5. Mdudu - Wadudu

6. Usafi - Usafi

7. Funza - Funza

**Matumizi katika sentensi**

1. Kila mtu atunze mazingira yake.
2. Ni bora kuzuia magonjwa kuliko kuyatibu.
3. Dawa za kulevya zina madhara mengi.
4. Mama atafagia uchafu wote.
5. Wadudu hatari wanastahili kuangamizwa.
6. Kila mtu adumishe usafi.
7. Funza ni wadudu hatari.

***Zoezi la 1***

**Kwa ushirikiano na wanafunzi wenzako, andika msamiati ufuatao katika wingi.**

**Mfano:** Mazingira - Mazingira

1. UKIMWI
2. Mdudu
3. Ugonjwa
4. Funza
5. Usafi

***Zoezi la 2***

**Andika sentensi zifuatazo katika umoja.**

**Mfano:** Vaeni nguo safi. - Vaa nguo safi.

1. Kunyweni maji safi.
2. Ueni wadudu.
3. Badilisheni tabia zenu.
4. Fagieni nyumba zenu.
5. Osheni vyombo vichafu.

### *Zoezi la ziada*

**Katika daftari lako, geuza kwa umoja ama wingi kwa kujaza mapengo yafuatayo kikamilifu.**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Uchafu | ______________ |
| 2. | ______________ | Miili |
| 3. | ______________ | Magonjwa |
| 4. | Mdudu | ______________ |
| 5. | ______________ | Mikono |
| 6. | Kichwa | ______________ |
| 7. | Mguu | ______________ |
| 8. | ______________ | Viuno |
| 9. | Jicho | ______________ |
| 10. | Pua | ______________ |

## E. Matamshi na tahajia bora

1. **Soma maneno yafuatayo na wenzako kwa kuzingatia matamshi bora.**

   a) Ukimwi unaua  b) Chemsha maji  c) Zoa takataka

   d) Fyeka nyasi  e) Tunza mazingira  f) Uzinifu

   g) Dawa za kulevya  h) Uchafu  i) Usafi

   j) Kula vyema

2. **Kwa kujitegemea, andika vifungu hivi kwa hati nzuri.**

a) Tunza mwili wako
b) Epuka uzinifu
c) Tunza mazingira
d) Weka akiba
e) Usitupe takataka ovyo

## Faharasa

**Kunawa:** kusafisha kwa maji na sabuni

**Mkono:** kiungo cha mwili kuanzia begani kinachotumiwa kushikia vitu

**Fua:** safisha kwa maji na sabuni ili kuondoa uchafu

**Kucha:** umoja wa 'ukucha'; sehemu ngumu inayomea kwenye ncha ya kidole cha mtu, ndege na baadhi ya wanyama

**Nywele:** malaika au singa zinazoota mwilini na hasa sehemu ya kichwa

**Kunyoa:** kata; ondoa nywele kwenye kichwa kwa kutumia wembe ama makasi

**Kuchana:** tengeneza vizuri nywele kwa kutumia kichanuo

**Piga mswaki:** sugua meno kwa kutumia mswaki na dawa ya meno

**Sabuni:** mchanganyiko wa vitu vinavyotokana na mafuta na aina mojawapo ya madini ya magadi na ambayo hutumiwa kwa kufulia, kuogea ama kusafisha vitu

**Upele:** vipele vilivyozagaa katika mwili

**Kipindupindu:** ugonjwa wa kuambukiza wa kuhara na kutapika sana

**Malaria:** ugonjwa unaoambatana na homa kali ambao huletwa na mbu

**Homa ya matumbo:** ugonjwa wenye madhara kama ya malaria

**Kifua kikuu:** ugonjwa hatari wa kukohoa na unaambukizwa haraka

**Keya:** ugonjwa wa kupasuka miguu (hasa visigino) iwapo huisafishi miguu vizuri

**Kichwa:** sehemu ya mwili iliyo juu ya shingo yenye ubongo, nywele, macho, masikio na kadhalika

**Jicho:** kiungo cha mwili (kichwa) cha kuonea

**Kifua:** sehemu ya mbele ya mwili kati ya tumbo na shingo

**Mguu:** kiungo ambacho humsaidia binadamu kusimama na kutembea

**Udevu:** unywele unaoota kwenye kidevu

**Kidole:** kiungo kilicho kwenye ncha ya mkono na miguu

**Kinywa:** kiungo kinachotumiwa kwa kula na kunywa chenye ulimi na meno

**Koromeo:** umio

**Paja:** sehemu ya mguu iliyo kati ya goti na nyonga

**Bega:** sehemu ya mwili iliyoko kati ya mkono na shingo

**Kiko:** kiungo cha mkono kati ya kiwiko na bega

**Pua:** kiungo cha kupumulia na kuvuta hewa ndani

**Nyonga:** sehemu ya mwili iliyo baina ya paja na kiuno

**Kiuno:** sehemu iliyo kati ya mgongo na makalio

**Mgongo:** sehemu ya nyuma ya mwili wa mwanadamu kutoka shingoni hadi kiunoni

**Kiwiko:** kiungo kinachounganisha kiganja na sehemu ya juu ya mkono (panapovaliwa saa)

**Kwapa:** sehemu ya mkono iliyo chini ya bega

**Jino:** kiungo ambacho binadamu hutumia kukata na kutafuna kinachopatikana ndani ya mdomo

**Kinyesi:** choo ya binadamu; mavi

**Mboga:** majani yanayoliwa na binadamu baada ya kupikwa

**Tunda:** zao la mmea linalohifadhi mbegu ambalo hutokana na ua

**Mazingira:** hali ama vitu vinavyozunguka kiumbe; miti, nyasi, watu na kadhalika

**Funza:** mdudu kama kiroboto ambaye hupenya kwenye miguu ya watu kutokana na uchafu

**Kuua:** kuondoa uhai

**Kupasuka keya:** kukatika miguu (nyayo) kwa kukosa kuoga

**Kutibu:** kufanyia matibabu kwa kupeana dawa

**Kuchemsha:** kuweka motoni ili kupata moto (hasa kitu cha majimaji)

**Mjadala/mdahalo:** majadiliano kuhusu jambo fulani kwa kuunga mkono ama kupinga huku hoja zikitolewa

**Dawa za kulevya:** dawa ambazo humfanya anayezitumia kuchanganyikiwa na kupoteza fahamu na afya yake kuharibika, kwa mfano: pombe, miraa, kokeini na bangi.

**Makundi:** mkusanyiko wa wanafunzi

**Uzinifu:** uasherati

**USAFI WA MWILI, MAZINGIRA NA TABIA NI MUHIMU**

## MAREJELEO


Mbaabu I. (1992); *Sarufi ya Kiswahili*; Longman Nairobi, Kenya.

Ndalu A. (1997); *Mwangaza wa Kiswahili*; East African Educational Publishers; Nairobi, Kenya.

Sanja L. na Kusino M (2006); *Kurunzi ya Kiswahili*; Focus Publishers.

Sanja L. na Felix O. (2006); *Kiswahili Faridi*; Focus Publishers.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu;* Oxford University Press.

TUKI (2009); *Stadi za lugha ya Kiswahili;* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Waihiga G. na Wamitila K.W. (2003); *Chemchemi za Kiswahili, Kidato cha Kwanza*; Longhorn Publishers; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na Wamitila K.W. (2003); *Chemchemi za Kiswahili, Kidato cha Pili*; Longhorn Publishers; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na F. M. Kagwa (2005); *Darubini ya Kiswahili*; Phoenix Publishers; Nairobi, Kenya.

Wamitila K. (2002); *Kichocheo cha fasihi*. Focus Publishers.